**27 AGOSTI, 2026**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA NNE**

**Kikao cha Pili – Tarehe 27 Agosti, 2026**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Daniel B. Sillo) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tukae.

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:**

Maelezo ya Waziri wa Kilimo kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Kilimo wa Mwaka 2026 *[The Agricultural (Amendments) Bill, 2026]*.

**MHE. DICKSON N. LUTEVELE K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA, KILIMO NA MIFUGO:**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Kilimo wa Mwaka 2026 *[The Agricultural (Amendments) Bill, 2026]*.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mjumbe kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

**MASWALI KWA WAZIRI MKUU**

**NAIBU SPIKA:** Sasa ninamwita Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Tutaanza na Mheshimiwa *Engineer* Ramadhani Hamza Singano.

**MHE. RAMADHANI H. SINGANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Mheshimiwa Waziri Mkuu nchi yetu imekuwa inapiga hatua kiuchumi katika shughuli mbalimbali, ikiwemo sekta ya kilimo, madini na hata uvuvi, lakini maeneo hayo yamekuwa yanakabiliwa na tatizo la kutopata mawasiliano kupitia mitandao mbalimbali ya simu, hali inayokwamisha shughuli hizo. Je, Serikali ina mkakati gani madhubuti wa kushirikiana na kampuni mbalimbali za simu kuhakikisha kwamba, mawasiliano yanafika katika maeneo hayo muhimu ya kiuchumi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii, ili niweze kujibu swali la Mheshimiwa Singano, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Mbunge, ninaomba uniruhusu nitumie jukwaa hili kumpongeza sana Mheshimiwa Deogratius John Ndejembi kwa kuaminiwa na Mheshimiwa Rais, Kamati Kuu na Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi na kuteuliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pili, nampongeza sana Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa jicho lake la mwewe, kuweza

kumuona Mheshimiwa Deogratius John Ndejembi kuwa, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Deogratius John Ndejembi, kama kiongozi, ni kiongozi mahiri sana. Ni kiongozi makini, ni kiongozi mchapakazi, anayefanya kazi bila kupumzika, ili Wananchi wa Tanzania waweze kupata manufaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Deogratius John Ndejembi, *as a person,* ni mtu rahimu sana, ni mtu mnyenyekevu sana, Muisraeli kwelikweli, asiye na hiyana ndani yake. Mimi pamoja na Waheshimiwa Mawaziri wenzangu tunamhakikishia Makamu wa Rais kwamba, tupo mguu sawa kupokea maelekezo na kuyafanyia kazi, ili kumsaidia yeye kutimiza jukumu lake la kumsaidia Mheshimiwa Rais katika majukumu yake ya kuijenga nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maneno hayo ya utangulizi nirejee kwenye swali la Mheshimiwa Mbunge na ninampongeza sana kwa swali zuri alilouliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu ni moja ya nchi ambazo zimewekeza sana katika mawasiliano, tumepiga hatua kubwa sana. Ukichukua miaka 25, tuseme kabla ya dira hii iliyoisha na sasa, pana mabadiliko makubwa sana katika sekta ya mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kuanza kutekelezwa kwa dira hii iliyoisha, kwa wale wa rika langu na wakubwa zetu watakumbuka, tulikuwa kwenye sanduku la posta peke yake, lakini leo hii hata aliyeko machungani anaangalia Bunge linapojadili masuala ya nchi hii, lakini ni kweli, bado kuna maeneo ambayo yana changamoto za mawasiliano. Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imeendelea kuweka na kutenga fedha kwa ajili ya kuimarisha mawasiliano katika maeneo hayo ambayo yana uchumi mkubwa, lakini yanapata changamoto za kimawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya maeneo ni tumeongeza fedha kwenye Mfuko wetu wa Mawasiliano, lakini pia, tumeendelea kuwekeza Mkongo wa Taifa uweze kufika kila wilaya. Tunaendelea kuwekeza na kutenga fedha kila mwaka wa fedha, ili kuweza kuhakikisha maeneo kama haya, ambayo Mheshimiwa Mbunge ameyataja, yakiwemo ya pembezoni, yakiwemo maeneo yenye uchumi mkubwa, yakiwemo ya kwenye barabara zetu, yakiwemo ya milimani ambako kuna wakati ajali zinatokea na yakiwemo ya kwenye mtandao wa reli yetu ya kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, namhakikishia Mbunge na Bunge lako Tukufu kwamba, Serikali itaendelea kuweka mkazo, ili kuhakikisha Watanzania wote wanapata mawasiliano na kuongeza kasi ya uzalishaji katika maeneo yetu ya kiuchumi.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ado Shaibu Ado.

**MHE. ADO S. ADO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi, ili niweze kuuliza swali kwa Waziri Mkuu; Mheshimiwa Waziri Mkuu mimi ninatoka jimboni na hili ninalolileta siyo jambo geni Bungeni, ila ninalileta tena kwa sababu, hisia za wananchi jimboni zinaonesha kwamba, jambo hili linapaswa kupata kauli nzito ya Serikali. Jambo hili siyo la Tunduru Kaskazini peke yake, ni jambo la mikoa mingi ya Kusini; Lindi, Mtwara, Ruvuma na sehemu nyingi za Tanzania. Jambo lenyewe linahusu migogoro ya wafugaji na wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ambayo nimeikuta jimboni inaonesha kwamba, licha ya jitihada ambazo Serikali imekuwa inazichukua, ikiwemo hatua za kipolisi na kiusuluhishi, bado migogoro ya wakulima na wafugaji imeleta hali ya sintofahamu. Mazao ya watu yameharibiwa, mbaazi hazivunwi, korosho hazivunwi vizuri, watu wanauawa, watu wanaumizana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ipi Kauli ya Serikali ya hatua madhubuti ambazo inalenga kuzichukua na ambazo zimechukuliwa, ili jambo hili lisilete mifarakano mikubwa

inayoweza kuleta mauaji zaidi na hali ambayo itatishia usalama katika nchi yetu? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Mbunge, Ado Shaibu, kwa kulileta swali hili. Mimi niliwahi kupata heshima ya kuwa Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi na katika kutimiza majukumu yangu niliwahi kushuhudia haya mambo ambayo Mheshimiwa Mbunge anayasema.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeshuhudia mifugo ya wafugaji ikiwa imekatwa katwa, zaidi ya mifugo 150. Nimeshuhudia mapigano, ambapo mkulima mmoja anachomwa mkuki; nadhani kwenye mitandao na Waheshimiwa Wabunge watakumbuka. Jambo hili limeendelea kujitokeza, kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge amesema.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inachofanya ni; moja, tumegawanya hatua za kuchukua kwa sababu, tatizo hili ni kubwa na linaendelea kuwa kubwa. Sababu ya msingi ni kwamba, idadi ya watu inaongezeka, idadi ya mifugo inaongezeka na hata idadi ya wanyama katika baadhi ya maeneo ya hifadhi inaongezeka, lakini ardhi ni ile ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo pia, mabadiliko ya tabianchi inayoondoa ile hali ya kimazingira, ambayo ilikuwa inaruhusu hizi shughuli zote kuwanufaisha wananchi pasipo kuleta mgongano. Kwa hiyo, tuna tatizo la msingi ambalo sababu zake ni kama hizi nilizozisema.

Mheshimiwa Naibu Spika, nini Serikali inafanya?

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hatua za muda mfupi tumesema, kwanza lazima tukubaliane kuhusu matumizi bora ya ardhi. Hili ni kwenye hatua za haraka kwa sababu, ipo migogoro maeneo mengine, ambayo inasababishwa na kutokuzingatia matumizi bora ya ardhi, ikiwemo tabia za baadhi ya viongozi

katika baadhi ya maeneo kuuza maeneo, ambayo yalikuwa yametengwa, kwa ajili ya wakulima na kupelekwa kwa wafugaji kinyemela. Ama baadhi ya maeneo, ambayo yalikuwa yametengwa, kwa ajili ya malisho kuuzwa kinyemela kwa wakulima na matokeo yake kusababisha migongano kwa hiyo, nimeelekeza ni lazima hatua kali zichukuliwe yakitokea mambo ya aina hii, ambayo yanasababisha migogoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, inatokea eneo ambalo limewekwa kwa malisho lote linauzwa kwa mtu mmoja ama eneo liliwekwa, kwa ajili ya kilimo lote linauzwa kwa mtu mmoja. Tumesema ni lazima tuzingatie mipango ya matumizi bora ya ardhi, ili hizi shughuli zote ziweze kwenda sambamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hatua za muda wa kati na muda mrefu, tumesema ni lazima twende kwenye *transformation*. Nampongeza sana Waziri wa Mifugo, Mheshimiwa Balozi Dkt. Bashiru Ally Kakurwa, na Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Dkt. Daniel Chongolo, pamoja na Waziri wa Maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo ambalo sekta hizi zimekubaliana kufanya ni kuhakikisha kila mmoja wa sekta anapotekeleza mradi anatengeneza mazingira ya sekta nyingine kunufaika. Kwamba, pakijengwa bwawa la umwagiliaji kwenye bwawa lile pia, pawekwe matoleo ya maji, kwa ajili ya wafugaji, ili kuepusha mifugo kwenda kupata shida ya maji na pengine kulundikana eneo moja; vivyo hivyo kwa Wizara ya Maji, vivyo hivyo kwa Wizara ya Kilimo, vivyo hivyo kwa Wizara ya Mifugo. Tunaamini ushirikiano huu wa sekta hizi utaendelea kutupunguzia matatizo ya upotevu wa maji, ambayo yanasababisha mifugo itembee maeneo tofauti-tofauti na pengine kwenda mpaka maeneo ambayo ni ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine tumesema tuwekeze kwenye mageuzi kwenye sekta hii ya mifugo. Moja ya mageuzi ambayo nimeenda kwenye shughuli ya wafugaji, nimejionea, na nimeona wafugaji wa kawaida wanaanza kufanya hayo mabadiliko ya kupanda nyasi, kwa ajili ya malisho ya mifugo. Nina mfano wa mfugaji kule Morogoro, nina mfano wa mfugaji mmoja

kule Monduli, wamepanda nyasi na mifugo yao haihangaiki tena kwenda kwenye mashamba ya watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ambalo tunachukua hatua kali ni wale wanaofanya makosa haya kwa makusudi, hawa ni watu wanaohatarisha usalama wa nchi yetu. Kuchukua mifugo na kuiswaga kwenda kuchungia kwenye shamba la mtu kwa makusudi, huu ni uvunjifu wa sheria wa makusudi na Serikali haitavumilia makosa ya aina hiyo. Vivyo hivyo, tumesema utaratibu wa kuchukua sheria mikononi na wenyewe ni jambo ambalo linahatarisha amani ya nchi yetu, haliwezi likavumilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeendelea kuwaambia wafugaji na wakulima, wala asitokee mfugaji akaona mkulima ni adui yake na wala asitokee mkulima akaona mfugaji ni adui yake. Hapa tuna jambo la msingi ambalo tunatakiwa tulifanyie kazi na Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Waziri wa Mifugo na Uvuvi pamoja na Waziri wa TAMISEMI wameendelea kukaa. Ninaelekeza kamati zetu za ulinzi na usalama za Mikoa, pia, kuendelea kukaa na makundi haya, ili kuweza kuweka utaratibu ulio bora, ili kuepusha matatizo haya ya migogoro na kuondoa hili tatizo ambalo linajitokeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili pia tunaendelea kulitafutia utaratibu wa kudumu, ili tuweze kuona ni namna gani tutalimaliza, ili tusiende kwenye matatizo haya, ambayo Mheshimiwa Mbunge ameyasema. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Kassimu Amari Mbaraka.

Tunaendelea, Mheshimiwa Asha Juma Feruz.

**MHE. ASHA J. FERUZ:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali. Tunaona jitihada nzuri na kubwa zinazofanywa na Serikali katika kutengeneza miundombinu ya usafirishaji, ikiwemo stendi zetu. Mwaka 2024/2025 mpaka 2026 Serikali imetumia shilingi bilioni 231 katika ujenzi wa stendi

mbalimbali, lakini mwaka 2026/2027 tuna bajeti ya shilingi bilioni 159.5 kwenda kuendeleza stendi mbalimbali katika mikoa yetu, halmashauri za miji na manispaa zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninapenda kumuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu. Ni upi Mwongozo wa Serikali katika matumizi ya stendi, ambayo yatatupa tija kwa wananchi na kwa uwekezaji mkubwa, ambao Serikali imeufanya na kuleta maendeleo makubwa kwa sababu, zile stendi ni sehemu ya mapato ambayo tunayarudisha kwenye jamii yetu kwenda kujenga zahanati, shule na miundombinu mingine? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii na ninampongeza Mheshimiwa Mbunge Asha Feruz. Nakiri kabisa Asha ni jina la mama yangu mzazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge ameleta hoja ya msingi. Nimefuatilia, nimeona hata pamekuwa na sintofahamu katika baadhi ya maeneo. Kwa kweli, hii hoja aliyoileta ni ya msingi, hata Mwenyekiti wa Kamati aliileta, kama moja ya jambo ambalo ni *alarming*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mwenyekiti alipoileta, tulikaa mimi, Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi na Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, pamoja na Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Tumelijadili jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna jambo ambalo tumelifanya la mpito, ninaomba hata Waheshimiwa Wabunge na wadau wetu wa usafirishaji tuelewane vizuri. Ulipotokea mzozo wa Mashariki ya Kati bei ya mafuta ikapanda, tukaitana ndani ya Serikali, pamoja na Mheshimiwa Spika, kuangalia ni hatua gani za kuchukua, ili wananchi wasipate shida ya kupanda kwa gharama za maisha na za usafirishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya hatua ambazo tumelichukua za mpito, ilikuwa ni kuonda takwa la mabasi yale ambayo kwa muundo wake wa utengenezaji hayawezi kuweka mzigo unaopitiliza, tukasema yasipite kwenye mizani kwa sababu, foleni inapokuwa kubwa mafuta yanatumika, gharama inaongezeka. Kwa hiyo, tukasema, magari yale ambayo kwa utengenezaji wake imethibitika hayawezi kuweka mzigo unaopitiliza yasipite kwenye mizani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, yale mabasi ambayo yenyewe ni *model* za zamani; yanaweza yakaweka mzigo mkubwa, mengine yanaweza yakaweka magunia ya mkaa, mengine magunia ya mahindi na mengine, tukasema haya yatapita kwenye mizani, lakini yasilazimike kupita kila mizani. Tukasema yapite mizani ya kwanza yanapoanza safari na ya mwisho, kabla hayajafika mwisho wa safari yake. Hii yote ilikuwa ni katika namna ya kupunguza matumizi ya mafuta na kushusha gharama kwa wenzetu hawa wa usafirishaji, ili wasipandishe nauli kwa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ambalo tulisema ilikuwa ni, hatua ya kuondoa takwa la mabasi yanayosafiri kwenda mikoani kupita kila stendi ya halmashauri hata kama hayashushi abiria. Tukasema, ndiyo, kwenye halmashauri ni chanzo cha mapato, lakini kama haupakii na haushushi abiria, tukasema tuondoe huo ulazima wa kila basi kuingia kila stendi. Mantiki yake ilikuwa ni tupunguze gharama, ili tusipandishe nauli Watanzania wakapata shida na tulikuwa hatujui haya mambo ya kupanda kwa bei za mafuta yataishia wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo moja ambalo ninawaomba Watanzania wote tuelewane, kama Mbunge alivyosema, ni kweli tumefanya uwekezaji mkubwa sana kwenye stendi. Stendi kama hii hapa ya Ndugai ni uwekezaji mkubwa, ni fedha ambazo tungeweza kuzipeleka kwenye kujenga hospitali, kujenga shule na huduma nyingine, lakini tumewekeza kwenye stendi. Stendi ya Magufuli, pale Dar es salaam ni kubwa, ambayo imetumia mabilioni ya fedha; fedha hizo tungeweza kuzipeleka kwenye shughuli nyingine za maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vivyo hivyo stendi ya Morogoro, zipo mbili, Mwanza na maeneo mengine. Nini tulichosema, kama Serikali?

Mheshimiwa Naibu Spika, tumesema kwa maeneo ambayo stendi zipo na mabasi yanaanzia hapo, mabasi yaende kwenye stendi kwa sababu, hizi stendi tumezijenga kwa ajili ya mabasi, lakini pia, inatusaidia, kama nchi, kuwa na utaratibu na pia, inatusaidia masuala ya kiusalama. Kila gari likianzia nyumbani, hili limeanzia kule, hili limeanzia kule, huku tumeshasema mengine yasipite kwenye mizani, *control* ya kiusalama! Yanaweza yakabeba dawa za kulevya yakapitiliza moja kwa moja kule yanakokwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tumechukua hatua za muda na tumesema tutakutana mambo yakitengamaa, ninaamini kule kwenye mikoa wameanza kukaa. Ninaelekeza *sectors* zetu, pamoja na mikoa yetu, wakae waweke utaratibu ambao ni lazima stendi zitumike na wakati huohuo tuendelee kuzingatia kutokuweka gharama ambazo zinaweza zikaepukika, ili tuweze kuwasaidia Watanzania wasipandishiwe nauli na gharama nyingine ambazo zinaweza kuleta shida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimewaelekeza wale wa Dar es salaam wakae haraka; nilipokuwa pale *NIT* kuangalia jambo linalohusiana na Stendi ya Magufuli, nimewaelekeza na nimeona Mkuu wa Mkoa amechukua hatua. Nimewaelekeza mikoa mingine wachukue hatua katika maeneo ambayo tuna stendi hizi kubwa na nimezitaja baadhi tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo maeneo mengine ambapo ujenzi wa stendi kubwa unaendelea, ninadhani, kama pale Moshi Mjini kuna ujenzi mkubwa sana wa stendi ya ghorofa. Kwa hiyo uwekezaji wa aina hii hatuwezi tukaacha ukawa *white elephants* na fedha za walipakodi hizo zikapotea. Lazima tutengeneze utaratibu ambao stendi ni kama *airport*, ni kama *station* ya *SGR;* tutakuwa na tunapoanzia, lakini lazima tuwe na *stations* ambazo zinatumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaendelea kusisitiza, sekta pamoja na wadau wakae kuangalia na kufanya mapitio kwenye haya yote ambayo tumeelekeza na Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI yupo hapa. Kama hivi ni kweli, basi ambalo halishushi na tulisema pasiwepo na kushusha abiria nje ya stendi, wala kupakia abiria nje ya stendi kwa hiyo, wale wa kupanda wapandie stendi na wale wa kushuka washushiwe stendi, lakini kwa yule ambaye hashushi tumesema hakuna ulazima wa kupita kwenye stendi za barabarani, kwa ajili tu ya kwenda kulipa *fees*.

Mheshimiwa Naibu Spika, *fees* za aina hiyo zinakuwa faini. Kwamba, kwa kuwa umepita kwetu lazima ulipe; tuliona hiyo inaweza ikaangaliwa, ili kupunguza gharama, lakini lile la stendi ninawaomba Watanzania, ninawaomba Waheshimiwa Wabunge, ninawaomba na wadau, huu ni uwekezaji wa fedha za walipakodi. Lazima wote tuwe na huruma na fedha ya walipakodi na matumizi yaliyokusudiwa yaweze kutumika. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa *Engineer* Johnston Johansen Mutasingwa.

**MHE. ENG. JOHNSTON J. MUTASINGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuuliza swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninakushukuru kwa kazi kubwa na njema unayoifanya. Vilevile, ninamshukuru Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya, hasa ya kupeleka pesa za maendeleo katika majimbo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia Serikali, Mamlaka ya Hali ya Hewa *(TMA)* imetoa tahadhari ya uwezekano wa kuwa na mvua kubwa juu ya kiwango cha mililita, yaani *El Nino,* yenye nguvu. Kwa uzoefu inaonesha mvua hizi zinapotokea zinaleta madhara, hasa katika upande wa miundombinu ya barabara na baadhi ya makazi ya wananchi hapa nchini. Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujua, je, Serikali imejipangaje endapo changamoto hii itatokea? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, Mheshimiwa J. J. swali zuri ameleta, linahusiana na tahadhari.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli tumepata tahadhari hiyo kutoka kwa wenzetu wa Mamlaka ya Hali ya Hewa, ambao wameelezea uwezekano wa kuwepo kwa mvua za *El Nino* na hazipo mbali, kwa mujibu wa wa utabiri huo. Mikoa ya Kanda ya Ziwa, kama Mwanza, inatarajiwa huenda mvua hizo zikaanza mwishoni mwa Septemba ama Oktoba na mikoa mingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imejipanga vyema kuhakikisha kwamba, maeneo hayo ambayo yanaweza kuwa na athari za mvua nyingi kutengeneza mifereji, maji yaweze kwenda kwenye njia zake, ili kuondoa uwezekano wa maji kulundikana. Ninalitaarifu Bunge lako Tukufu taarifa moja njema; Bunge lako lilitupitishia marekebisho ya sheria kwenye *Finance Bill,* yaliyoelekeza fedha za mifuko ya barabara na mifuko mingine kwenda moja kwa moja kwenye mifuko.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha pamoja na Mamlaka ya Mapato Tanzania, wametekeleza uamuzi huo kwa kuanza kupeleka fedha hizo moja kwa moja kwenye mifuko, ambapo kwa mwezi ni zaidi ya shilingi bilioni 320 zinaenda moja kwa moja kwenye mifuko na kuwezesha kukabiliana na mambo kama haya, ambayo Mheshimiwa Mbunge amesema. Kwa hiyo, tumeelekeza *TANROADS* na *TARURA* wapitie maeneo yote ambayo ni korofi; maeneo yote ambayo maji yanaweza yakafanya mlundikano na kuleta mafuriko watengeneze mifereji, lakini waendelee kuangalia barabara katika maeneo korofi, ili kuhakikisha kwamba, wananchi hawakosi miundombinu kutokana na mafuriko.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, ninatumia fursa hii pia, kutoa rai kwa Watanzania wote, kuwa na tahadhari na jambo hili ambalo tayari tumetahadharishwa. Ni wajibu wa kila Mtanzania kufanya tathmini ya aina hiyo pale anapoishi kwa kuangalia mazingira ya mahali na hali hii, ambayo tumetahadharishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo mengi tunayoishi tunajua historia ya maji huwa yanapita kwa namna gani endapo inatokea mvua kubwa. Tuendelee kuchukua tahadhari hizo, ili maafa yasitokee ilihali tumetahadharishwa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Sikudhani Yassini Chikambo.

**MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Awali ya yote kwanza napenda kutumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi nzuri anayoifanya katika Taifa letu. Tumekuwa tunashuhudia anafanya ziara katika mikoa mbalimbali, ziara zenye manufaa, kupita kuhakiki miradi ya maendeleo pamoja na kuchochea shughuli za maendeleo. Sisi tunakukaribisha Mkoa wa Ruvuma; tuna kauli yetu tunasema, mgeni aje, mwenyeji apone. Karibu sana Mkoa wa Ruvuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya ya utangulizi naomba niulize swali langu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu kwamba, Serikali yetu imekuwa inajitahidi sana kuhakikisha sisi wananchi wote tunapata vitambulisho vya *NIDA* Na tunafahamu kwamba, kuwa na kitambulisho cha *NIDA* ni utambulisho wa Taifa lako. Suala la *NIDA* ni jambo ambalo ni muhimu kwa kila mwananchi kwa sababu, sasahivi fursa nyingi zinataka lazima uwe na kitambulisho cha *NIDA,* lakini jambo hili limekuwa na changamoto katika baadhi ya maeneo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi bado hawapati vitambulisho wala namba za utambulisho wa *NIDA*. Mheshimiwa Waziri Mkuu, natamani kuuliza; ni nini sasa mkakati wa Serikali, kwa kutambua umuhimu wa *NIDA,* kuhakikisha wananchi wote wa Tanzania tunakuwa na vitambulisho vya *NIDA,* ili tusikose fursa zile muhimu? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi, ili niweze kujibu swali zuri la Mheshimiwa Sikudhani Chikambo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema katika swali la mifugo, nimewahi kupata heshima ya kuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Moja ya jambo ambalo limekuwa na *concern* nyingi za wananchi, hasa wa pembezoni, ni hili la Vitambulisho vya Taifa, almaarufu vitambulisho vya *NIDA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninatumia jukwaa hili kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tangu muda ule na sasa nchi yetu imepiga hatua kubwa kwenye jambo hili licha ya kwamba, bado kuna hizo changamoto ambazo Mheshimiwa Mbunge amezisema.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya hatua ambazo zimechukuliwa na ambazo Serikali inakusudia kuziendeleza kwa kasi zaidi, ili Mheshimiwa Mbunge akawaambie na wananchi wake, ni utaratibu huu ambao tunautumia wa kidigitali. Tumeona manufaa yake kwamba, kupitia njia za kidigitali sasa mwananchi anaweza akapata ile namba, anaweza akafanya ule utaratibu kupitia simu yake, tena simu hata ile ya kawaida, akakamilisha baadhi ya hatua, ili kupunguza ule mlolongo ambao ungeweza kujitokeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, Serikali inakusudia kuwafuata wananchi kule vijijini na maeneo mengine, ambayo kamati zetu za ulinzi na usalama zimejiridhisha. Serikali inakusudia kuanza kutoa namba hizo kwa mkupuo; kwamba, kijiji kizima wamemaliza kufanyiwa taratibu za masuala ya kamati za ulinzi na usalama, masuala ya kuwatambua, basi wanapewa vitambulisho vyao hivyo bila kupata usumbufu mkubwa ambao wamekuwa wakiupata.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaendelea kusogeza huduma hii iende kule kwa wananchi, ili kuwaondolea usumbufu. Vilevile, tumesema tutaongeza jitihada za ushirikiano kati ya Serikali za

Mitaa na vyombo vyetu vya ulinzi na usalama pamoja na wenzetu wa Uhamiaji, ili kuhakikisha tunapunguza mchakato.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninatoa rai kwa Watanzania wote, pamoja na nia njema ya Serikali kutaka Watanzania wapate vitambulisho kwa haraka. Pamoja na ukweli huu kwamba, Kitambulisho cha Taifa sasa ni kila kitu, ndicho kitakachotupeleka kwenye mikopo ya elimu, ndicho kitakachokupeleka kwenye utambuzi na kila kitu, ninawaomba Watanzania waridhie vyombo vyetu viendelee kuhakiki kwa kina *status* za wale wanaotakiwa kupewa Vitambulisho vya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu katika nyakati tofauti imeweza kupata vielelezo vya watu ambao siyo raia wa Tanzania kuweza kupenyapenya. Pengine katika dunia ya sasa ambayo masuala ya uhalifu yameongezeka ni jambo ambalo linaweza likawa la hatari, kuwekeza tu kwenye kuhakikisha tunafanya kwa uharaka bila kuzingatia umakini wa kuchuja na kujiridhisha kwamba, wale wanaopewa vitambulisho hivyo ni raia wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninamshukuru Mheshimiwa Mbunge na ninaomba niwahakikishie wananchi wako na Wabunge wote, Serikali imekusudia kuongeza kasi ya upatikanaji wa vitambulisho kwa kutambua umuhimu wa wake na umuhimu wa namba hiyo katika shughuli za kila siku za maisha ya Watanzania. Hata hivyo, tutaendelea kujiridhisha wale tunaowapatia vitambulisho hivyo wanakidhi vigezo kwamba, ni raia wa Tanzania. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Thomas Kampala Maganga.

**MHE. THOMAS K. MAGANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Mimi pia, ninampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi nzuri anayoifanya. Tunaendelea kumuombea kwa Mungu achape kazi na sisi Wabunge tuko pamoja na yeye.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivisasa Taifa letu linapitia changamoto kubwa ya mmomonyoko wa maadili na hii inasababishwa na mabadiliko ya tamaduni, malezi na mifumo ya kijamii. Kwa sasa kumekuwa na dhana ya kwamba, shule zetu zinazobeba wanafunzi wa jinsia moja nako kumekuwa na changamoto ya vitendo vya usagaji na ushoga. Je, Serikali haioni sasa umefika wakati wa kuondoa utaratibu huo, ili kukabiliana na changamoto hii? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza Mheshimiwa Mbunge, Kampala Thomas Kampala. Kweli yeye ni balozi anayechapa kazi kwenye masuala haya yanayohusu mmomonyoko wa maadili katika jamii yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili ambalo Mheshimiwa Kampala ameendelea kulisimamia ni jambo linaloigusa kila familia na nchi yetu. Bila maadili ya vijana wetu hatuna hatima njema, hatuna kesho ya Taifa letu. Kwa hiyo, ninakupongeza sana Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali. Serikali inaendelea kuweka mkazo na nimemuona Waziri wa sekta, Mheshimiwa Dkt. Dorothy Gwajima, pamoja na sekta zingine ambazo wanashirikiana nazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatilia mkazo mkubwa sana jambo hili kwa kuzingatia kwamba, limebeba hatima ya kesho yetu. Moja ya hatua ambazo tumechukua ni kubadilisha baadhi ya taratibu kwenye shule zetu hizi za bweni, ikiwemo kufuatilia kwa karibu masuala yanayohusu malezi kwa watoto, hasa wanapokuwa katika shule zetu. Vivyo hivyo, tumeongeza madawati yanayohusu kusimamia masuala haya ya maadili na ya kijinsia katika shule zetu zote, ili kuhakikisha kwamba, panapotokea jambo hili ama uhitaji wa uelimishaji, jambo hilo la uelimishaji liendelee kufanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimepita shule moja ya *private* nikakuta, wao kwa kukabiliana na jambo hili, wameweka utaratibu wa kuweka *camera* kwenye mabweni ya wanafunzi. Kwa kuwa, Mwanasheria Mkuu wa Serikali yupo, atatusaidia kuangalia kwenye upande wa kisheria kama huo ndiyo utaratibu unaofaa, kuweka *camera* kwenye makazi, madarasa na mabweni ya wanafunzi, ili kukabiliana na tatizo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema Mwanasheria Mkuu atatusaidia, lakini ninachosisitiza ni kwamba, hili tatizo analosema Mheshimiwa Mbunge ni kubwa. Zamani tulikuwa tunaelezewa tu kwamba, tumzingatie sana mtoto wa kike kwa sababu yuko hatarini sana na kampeni hiyo ikawa kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninatumia Bunge lako Tukufu kuwaomba Watanzania kwamba, sasa tuwazingatie watoto wote, hata watoto wa kiume kwa sasa wako hatarini sana. Wapo hatarini sana na pengine hatari ambayo wanaipata, watoto wa kiume kwa sasa, inaweza ikawa kubwa kuliko hata lile tulilokuwa tunaona ni tatizo kwa watoto wa kike. Kwa hiyo, jambo hili, pamoja na kwamba lina balozi, pamoja na kwamba lina Wizara, pamoja na kwamba Serikali inalisukuma, lakini nchi nzima kuanzia ngazi ya familia, taasisi za dini na za kijamii tutambue kwamba, hili ni jambo ambalo linahitaji mshikamano wa nchi nzima ili kukabiliananalo. Vinginevyo tutakuwa tunahatarisha hatima ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kama kiongozi wa Shughuli za Serikali ninaendelea kufanya uratibu wa sekta hizi zinazohusika pamoja na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ili kuhakikisha ni namna gani tunaongeza kasi ya kukabiliana na mambo ya aina hii. Serikali itaendelea kuchukua hatua kali kwa mambo yote yanayokiuka maadili, tamaduni na mila zetu, kama Watanzania, na Watanzania kwenye mambo haya wala tusione haya. Tuna mila zetu, tuna tamaduni zetu na tuna mambo ambayo ni ya kisheria tunayoyasimamia; lazima tuyasimamie bila kuona haya, ili kulinda Taifa letu na kizazi kijacho. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Bahati Keneth Ndingo.

**MHE. BAHATI K. NDINGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kupata fursa ya kumuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu swali. Mheshimiwa Waziri Mkuu, tunatambua Serikali imefanya uwekezaji mkubwa sana kwenye sekta ya kilimo nchini na hivyo kuhamasisha wananchi kujitokeza kwa wingi kufanya shughuli za uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa wakulima, wamezalisha kwa kiasi kikubwa kiasi kwamba, mazao yametosheleza mahitaji yao ya chakula na mengine kwa ajili ya biashara. Hali ya bei ya mazao nchini sasa, hususan mahindi na mpunga, iko chini sana; hali ambayo inasababisha wananchi kukosa soko la uhakika kupeleka bidhaa hizo. Je, Serikali ina kauli gani kuhakikisha kuwa, wananchi hawa wanapata soko la uhakika na bei yenye tija, ambayo itawawezesha kurudi mashambani na kutokatika kwa mitaji yao?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mbunge makini wa Mbarali, Mheshimiwa Bahati Ndingo, kwa swali zuri alilolileta. Ninajua kuwa, ungewaruhusu Waheshimiwa Wabunge wengine wengi wanaotokea kwenye maeneo hayo, kutoka Mkoa wa Kigoma, Katavi, Njombe, Ruvuma, Iringa na Mbeya, wangesema hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba, Serikali imewekeza pakubwa katika masuala ya uzalishaji, hasa hasa sekta ya kilimo, ikiwemo hatua ambazo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amezichukua za kupeleka ruzuku ya mbolea na kufanya *modernization* ya kilimo cha umwagiliaji katika maeneo mbalimbali. Kufuatia uwekezaji huo ni kweli kwamba, imejitokeza changamoto ya masuala ya masoko; mbali na uwekezaji huo mkubwa, changamoto nyingine ambayo imejitokeza imetokana na kuharibika kwa mnyororo wa masuala ya usafirishaji, pale ambapo umetokea mzozo wa mashariki ya kati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inavielekeza vyombo vyetu ambavyo vinasimamia mazao haya, ikiwemo *NFRA,* Bodi ya Mazao Mchanganyiko, pamoja na bodi zingine zinazosimamia masuala haya, kuongeza nguvu kwa kushirikiana na wenzetu wa Wizara ya Viwanda na Biashara, ili kuhakikisha mazao haya ya wakulima yanapata soko. Natumia fursa hii, baada ya swali zuri hili lililoletwa, kuwaelekeza Wizara ya Kilimo, Wizara ya Viwanda na Biashara, pamoja na Wizara ya Mambo ya Nje kukaa haraka, ili kuangalia ni namna gani tunanusuru jambo hili la bei za za mazao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninajua kwamba, *NFRA* huwa wana mfuko unaoweza kununua kiasi. Tupate tathmini tumefika hatua gani, lakini pia, tuangalie namna ambavyo tunaweza kupata masoko ya mazao haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kuwahamasisha wadau wa sekta binafsi kuchukua mazao haya na kuyapeleka nchi za jirani kwa sababu, uwekezaji na uzalishaji uliofanyika Tanzania, ni huohuo pia, huwa unalisha nchi za jirani. Kwa hiyo, tuendelee kutumia masoko hayo ya nchi za Jirani, ili kuhakikisha kwamba, wakulima wetu wanapata kipato na wanarejea tena kulima. Nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. Tunashukuru sana kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Ahsante sana Mheshimiwa. Tunakupongeza sana. *(Makofi)*

Ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge. Tunawashukuru.

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**NAIBU SPIKA:** Tunaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Ninamwita Mheshimiwa Kangi Alphaxard Lugola, Mbunge wa Mwibara, sasa aulize swali lake.

Na. 19

**Ujenzi wa Vituo vya Afya katika Kata za Jimbo la Mwibara**

**MHE. KANGI A. LUGOLA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga vituo vya afya katika Kata za Butimba, Nyamihyolo, Namhula, Chitengule, Igundu, Nansimo na Nampindi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Kangi Alphaxard Lugola, Mbunge wa Mwibara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kutafuta fedha, kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya kwenye kata zenye uhitaji kwa kuzingatia kigezo cha wingi wa watu, umbali na ugumu wa kufikika, ili kusogeza huduma za dharura na za upasuaji karibu na wananchi. Ukiacha Kata ya Butimba na Nyamihyolo, Kata za Namhula, Chitengule, Igundu, Nansimo na Nampindi zote zina wakazi zaidi ya 10,000 na hivyo, kukidhi vigezo vya kujengewa kituo cha afya. Aidha, Kituo cha Afya Chitengule ni moja kati ya vituo vya kimkakati 94, ambavyo fedha yake imeombwa Hazina na Wizara ya Fedha inashughulikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, vituo vingine vilivyobaki vya Namhula, Igundu, Nansimo na Nampindi vimewekwa kwenye

mpango wa ujenzi. Fedha zitakapopatikana zitapelekwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Bunda, kwa ajili ya ujenzi. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Kangi Lugola, swali la nyongeza.

**MHE. KANGI A. LUGOLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, majibu ambayo yanaleta matumaini kwa Wananchi wa Mwibara. Ninaamini Mheshimiwa Waziri ni miongoni mwa Mawaziri ambao wanatembea kwenye maneno yao na maono ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia majibu haya ambayo yana dhamira ya dhati, sioni haja ya kuuliza maswali mengine ya nyongeza zaidi tu ya kumpongeza Mheshimiwa Waziri na kumuomba atembelee jimbo langu, ili aone kiwanja ambacho tayari tumekitenga, kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya cha Chitengule.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Kangi Lugola. Namuahidi kwamba, baada ya mkutano huu nitahakikisha kwamba, ninatembelea jimboni kwake na kuendelea kufanya ufuatiliaji wa ujenzi wa vituo hivi vya afya.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Edifonsi, swali la nyongeza.

**MHE. EDIFONSI J. KANONI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa shughuli kubwa anayoifanya, kwa kutenga fedha, kwa ajili ya kujenga kituo cha afya katika Kata ya Ulumi. Katika bajeti iliyopita tumetengewa shilingi milioni 650.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna ahadi ya Waziri Mkuu Mstaafu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa, katika Kituo cha Afya cha

Kasanga ambacho hadi sasa hatujafanikiwa kukipata. Je, ni lini sasa mpango wa Serikali kuhakikisha kituo cha afya kile ambacho wananchi wamesubiri kwa muda mrefu katika Kata ya Kasanga kinajengwa au fedha zitapatikana, kwa ajili ya kutekeleza ujenzi wa Kituo cha Afya Kasanga?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Kanoni kwa kufuatilia suala hili la ujenzi wa vituo vya afya kwenye jimbo lake. Kama alivyosema mwewenye, Mheshimiwa Kanoni kwamba, kwa mwaka huu tayari ameona na tumekubaliana kwamba, tunapeleka shilingi milioni 650, kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Ulumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona kipo cha Kasanga. Ni kweli, tunafahamu kwamba, kuna ahadi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu aliyepita, tunachukua kituo hiki na tunaendelea kukifanyia kazi. Pindi tutakapopata fedha za ziada tutahakikisha kwamba, tunajenga kituo hiki cha afya, ili Wana-Kasanga waweze kupata huduma ya afya kwa ukaribu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, swali la nyongeza.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Wananchi wa Kata ya Machame Kaskazini, Kata ya Uroki na Kata ya Romu wamejichanga wakanunua eneo na wameanza kujenga zahanati, kwa maana ya eneo la Foo, Uroki na pale Romu. Je, Serikali ina mpango gani wa kuwaongezea wananchi, kuwaletea fedha, kama kuwaunga mkono, ili waweze kukamilisha ujenzi wa zahanati hizi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Saashisha, Mbunge wa Jimbo la

Hai, kwa namna anavyofuatilia shughuli za maendeleo, kwa ajili ya kupeleka huduma kwa wananchi wa Jimbo lake la Hai. Ni kweli kwamba, wananchi wa kata hizi tatu wamejiunga na kuanza ujenzi wa zahanati, kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba, Mheshimiwa Saashisha ame-*submit* barua, ambayo inaomba fedha, kwa ajili ya umaliziaji wa zahanati hizi. Ni kweli, tumepokea barua ile, tunaendelea kuifanyia kazi na *soon* kuna fedha tunazotegemea mahali, zikipatikana basi tutamalizia ujenzi wa maeneo yale. Naamuelekeza Mkurugenzi wa Hai, kutokana na mapato ya ndani wanayoyapata, aone ni namna gani angalau aanze kumalizia zahanati moja kati ya zile ambazo zinaendelea kujengwa.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Tunaendelea na swali linalofuata.

Mheshimiwa Bakari Bakari Shingo, Mbunge wa Ukonga, sasa aulize swali lake.

Na. 20

**Ujenzi wa Barabara Jimbo la Ukonga Chini ya Mradi wa *DMDP***

**MHE. BAKARI B. SHINGO** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga barabara za Jimbo la Ukonga chini ya Mradi wa *DMDP* kwa mwaka wa fedha 2026 – 2027?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kujibu swali la Mheshimiwa Bakari Bakari Shingo, Mbunge wa Ukonga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Uendelezaji wa Jiji la Dar es Salaam, Awamu ya Pili *(DMDP II),* unatekelezwa na Serikali kwa kipindi cha miaka sita, kuanzia mwaka 2024 hadi 2030, kupitia mkopo nafuu kutoka Benki ya Dunia wenye jumla ya Dola za Kimarekani milioni 385. Moja ya kipengele cha mradi ni ujenzi wa miundombinu himilivu ya usafiri kilichotengewa jumla ya kiasi cha Dola za Kimarekani milioni 205.20, ikijumuisha miundombinu ya barabara kwenye halmashauri za manispaa za Mkoa wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2026/2027, kupitia fedha za ndani, Serikali imetenga shilingi milioni 550, kwa ajili ya ukarabati wa Barabara za Jimbo la Ukonga ambazo ni Zingiziwa, Buyuni – *PSSSF*, Matumbi – Nyeburu, Zavara, Urusulain, Nguvukazi kwenda Rongwe na Chanika kwenda Nzasa. Pia, kuna Barabara ya Bangulo kwenda Pepeteka na Pugu – Majohe – Mbondole, ili ziweze kupitika muda wote. Serikali inaendelea kuangalia uwezekano wa kuongeza fedha kupitia Mradi wa *DMDP II,* ili kukamilisha kazi nzuri ya uboreshaji wa miundombinu katika Mkoa wa Dar es Salaam, zikiwemo barababara za Jimbo la Ukonga.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bakari Bakari Shingo, swali la nyongeza.

**MHE. BAKARI B. SHINGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri nampongeza Mheshimiwa Waziri, lakini nataka nifahamu; amesema ametenga shilingi milioni mia tano na kidogo, kwa ajili ya barabara hizo alizozitaja. Ninaona ni kama barabara hii, maana ni kwa kiwango cha vumbi. Barabara ninazoulizia mimi ni za *DMDP* ambazo zina sifa ya kutengenezwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo nahitaji nifahamu hapo kwamba, ninazo barabara hizo? Kwa sababu, kimsingi sina hizo barabara. Nataka nijue jibu la moja kwa moja.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli anachokisema Mheshimiwa Shingo, kwamba, kwenye Mradi wa *DMDP II,* Jimbo la Ukonga halikupata barabara. Kwa sasahivi kwa sababu, fedha zote za *DMDP II* zimekwisha kwenye maeneo mengine sisi, kama Wizara pamoja na Wizara ya Fedha, tumeanza *engagement* na *World Bank,* ili tupate fedha, kwa ajili ya Mradi mwingine wa *DMDP III*. Kwa hiyo, kwenye mradi huo tukipata fedha tu tutaanza na Jimbo la Ukonga kwa sababu, tunajua hali ilivyo na tutahakikisha kwamba, barabara za Jimbo la Ukonga zinajengwa kwa kiwango cha lami.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Eric James Shigongo, swali la nyongeza.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kuniona. Mji wa Nyehunge ni makao makuu ya Jimbo la Buchosa. Barabara zake za mitaa zina hali mbaya sana pamoja na wema wote ambao Mheshimiwa Waziri na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania umetutendea. Je, barabara za mji huu zinaweza kuingizwa katika taratibu, ili na zenyewe ziweze kujengwa kwa kiwango cha lami?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Eric Shigongo, Mbunge wa Buchosa, kwa kazi kubwa anayoifanya, kwa ajili ya Wana-Bbuchosa. Ni kweli, tunafahamu kwamba, barabara hizi alizozitaja Mheshimiwa Mbunge zinahitaji fedha, kwa ajili ya ujenzi angalau kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, namhakikishia Mheshimiwa Shigongo kwamba, tunaendelea kutafuta fedha. Fedha zikipatikana tutazipeleka, kwa ajili ya ujenzi wa barabara hizi kwa kiwango cha lami.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Agnesta Kaiza, swali la nyongeza.

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kuniona. Kata tano kati ya 13 ndani ya Jimbo la Segerea, kwa maana ya Kata ya Vingunguti, Kata ya Liwiti, Kata ya Tabata, Kata ya Kimanga na Kata ya Bonyokwa, zinapitiwa na Mradi huu wa *DMDP II.* Barabara hizi ni mbovu sana na mradi umesimama kabisa; sababu kubwa ya mradi huu kusimama ni hakujalipwa fidia hata kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kufahamu, kwa umuhimu wa barabara hizi na kwa uchakavu wa barabara hizi. Je, Serikali ina kauli gani kuhusiana na kulipa fidia kwa wananchi, ili mradi huu uweze kuanza?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye miradi hii ya Benki ya Dunia, fedha za kulipa fidia huwa zinatoka kwenye Serikali. Sisi Wizara ya TAMISEMI pamoja na wenzetu wa Wizara ya Fedha tuko kwenye majadiliano kuona ni namna gani tutapata fedha kwa haraka, ili tulipe fidia kwenye barabara zile na kazi ya ujenzi ianze.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hizi, kama alivyosema Mheshimiwa Kaiza, ziko kwenye mradi wa *DMDP II.* Pindi tutakapolipa fidia, moja kwa moja barabara zile zitatengenezwa kwa hiyo, namhakikishia na asiwe na wasiwasi. Serikali hii itatafuta fedha zilipe fidia, ili kazi ya ujenzi wa barabara zile ianze.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa. Tunaendelea na swali linalofuata.

Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe, Mbunge wa Momba, sasa aulize swali lake.

Na. 21

**Ukarabati wa Barabara toka Nkala hadi Kamsamba**

**MHE. CONDESTER M. SICHWALE** aliuliza:-

Je, lini Barabara kutoka Nkala – Chilulumo – Mkulwe hadi Kamsamba itafanyiwa ukarabati kwa kuwa ni chakavu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe, Mbunge wa Momba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya Nkala – Chilulumo – Mkulwe – Kamsamba ni muunganiko wa Barabara mbili; yaani Barabara ya Chilulumo – Nkala, yenye urefu wa kilometa 30.45 na Barabara ya Ntungwa – Kamsamba yenye urefu wa kilometa 49.84 hivyo, kwa pamoja zinafanya jumla ya kilometa 80.29. Barabara hizi zinahudumiwa na Wakala wa Barabra za Mijini na vijijini *(TARURA)*, Wilaya ya Momba.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mpango wa bajeti ya mwaka wa fedha 2026/2027 barabara hizi zimetengewa shilingi milioni 298.3. Kati ya hizo, shilingi milioni 37.5 zitafanya kazi ya matengenezo ya kawaida yenye urefu wa kilometa 15 na shilingi milioni 260.8 zitatumika kufanya matenegenezo ya sehemu korofi zenye urefu wa kilometa 17 na hivyo, kufanya jumla ya urefu wa barabara utakaokarabatiwa kuwa kilometa 32. Kutokana na umuhimu wa barabara hii, Serikali inaendelea kutenga fedha, kwa ajili ya matengenezo na ukarabati mkubwa kulingana na upatikanaji wa fedha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe, swali la nyongeza.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru tena. Ninashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri, ni majibu yanayoridhisha na yanatia moyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina ombi. Tunaomba barabara hizi zianze kutengenezwa mapema iwezekanavyo kabla msimu wa mvua haujarejea kwa sababu, zinapotengenezwa kipindi cha mvua, fedha inakuwa haileti tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina maswali mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tunayo Barabara nyingine ya Ikana – Makamba, ambayo inaunganisha barabara hii kufika Nkala; nayo imeharibika sana, ni chakavu na ni barabara ya muhimu sana katika uchumi wa Jimbo la Momba. Tunaomba nayo atoe maelekezo ianze kufanyiwa marekebisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Barabara nyingine ya Ivuna – Mkomba katikati kuna kiteputepu kikubwa, kimewahi kuzua taharuki kubwa kwenye mitandao ya kijamii kwamba, kimejengwa kwa pesa nyingi. Sasahivi kiteputepu hicho kimeharibika na huwa kinasababisha watu wengi kufariki. Tunaomba, nalo atupatie pesa za dharura, ili kiweze kufanyiwa kazi. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshukuru tena Mheshimiwa Condester kwa maswali yake mawili ya nyongeza. Maswali haya yanazungumzia barabara ambazo zinahitaji kupewa kipaumbele kwa haraka kutokana na hali ilivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamuelekeza *CEO* wa *TARURA* ahakikishe anawasiliana na watumishi wenzake, *RM* wa Mkoa wa Songwe pamoja na *DM* wa Wilaya ya Momba kuhakikisha kwamba, barabara hizi zinachukuliwa na kufanyiwa matengenezo kwa uharaka kwa kadiri ya fedha za tahadhari

zinavyopatikana. Kwa hiyo, ninamhakikishia Mheshimiwa Condester kwamba, barabara hizi zitatengenezwa kwa kadiri ya upatikanaji wa fedha, hasa hizi za dharura. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Khalid Nsekela, swali la nyongeza.

**MHE. KHALID M. NSEKELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Barabara ya Nkwenda – Kakanja – Mabira, ni kiungo kwa wafanyabiashara na wananchi wa Jimbo la Kyerwa. Barabara hii imechakaa sana kiasi kwamba, ina-*slowdown movements*. Naomba kuuliza, Serikali ina makakati gani wa haraka na wa dharura kuikarabati? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kuwasemea wananchi wa jimbo lake, hasa kwa upande huu wa miundombinu ya barabara. Ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, barabara hii aliyoitaja, tutahakikisha tunatuma *team* yetu kuiangalia na kuona *estimates* zake ni kiasi gani. Kwa kadiri tunavyopata fedha, kama alivyosema Mheshimiwa Waziri Mkuu hapa, sasa fedha hiyo inapelekwa moja kwa moja *TARURA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutaona namna bora ya kurekebisha barabara ile, ili wananchi waweze ku-*access* huduma kwenye maeneo yale. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hawa Mwaifunga, swali la nyongeza.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa kuniona. Kwanza, napenda kuishukuru Serikali kwa kutuletea zaidi ya shilingi milioni 500, kwa ajili ya ujenzi wa Daraja la Igambilo kwenye Barabara ya Kata ya Misha.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara zinazounganisha daraja hili ni dhoofu kabisa kiasi kwamba, mvua itakaponyesha daraja lile litakwenda na maji kwa sababu, ni eneo ambalo lina maji mengi. Nini mpango wa Serikali kuhakikisha barabara zinazounganisha daraja lile zinajengwa, ili kunusuru ujenzi wa daraja hili ambalo limejengwa kwa gharama kubwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ina fedha ambazo zinaangalia maeneo korofi, zinaitwa *bottlenecks*. Kwa hiyo, kwenye hizi barabara zenye madaraja haya, tutaangalia kama barabara hii, ama daraja hili, liko kwenye mpango wa utekelezaji, ili tupeleke fedha huko mara moja. Kama haliko kwenye mpango wa utekelezaji, tutaangalia namna fedha ya dharura tunavyoipata tuipeleke kule, ili daraja lile liweze kujengwa. Ninakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Isack Copriano, swali la nyongeza.

**MHE. ISACK J. COPRIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Barabara ya kutoka Kijiji cha Mbasi kwenda Kijiji cha Nselela tumetenga fedha mwaka huu, kwa ajili ya kujenga Daraja la Loolo – Senkenge kwa mfuko ule wa fedha ya jimbo. Ni lini basi kazi hiyo itatangazwa, ili daraja hilo lijengwe kwa sababu, ni daraja ambalo mvua ikinyesha wananchi kupata huduma inakuwa ni tatizo. Ninaomba kauli ya Serikali, ni lini *TARURA* wataitangaza barabara hiyo, kwa ajili ya ujenzi wa Daraja hilo la Loolo – Sekenge lililoko Mbaash?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza sana Mheshimiwa Laizer kwa namna anavyowasemea Wananchi wa Jimbo la Monduli, tunampongeza sana. Amezungumzia daraja hili linalounganisha Mbaash na Selela.

Mheshimiwa Naibu Spika, daraja hili lipo kwenye mpango wa ujenzi na kama alivyosema, ninamuagiza na kumuelekeza *CE* awaelekeze wataalamu wake watangaze daraja lile, ili lianze kujengwa mara moja kabla mvua haijaanza. Ninakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na swali linalofuata.

Mheshimiwa Njalu Daudi Silanga, Mbunge wa Itilima, sasa aulize swali lake.

Na. 22

**Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia Shule ya Amali, Itilima**

**MHE. NJALU D. SILANGA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itapeleka vifaa vya karakana vya kufundishia na kujifunzia katika Shule ya Amali, Wilaya ya Itilima?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Njalu Daudi Silanga, Mbunge wa Itilima, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2023/2024 Serikali ilitoa shilingi bilioni 88.84, kwa ajili ya ujenzi wa shule 103 za amali za kihandisi, ambapo shule 28 zimekamilika na zinatumika, ikiwemo Shule ya Sekondari ya Ufundi ya Mwamapalala, iliyojengwa katika Wilaya ya Itilima. Mwaka 2025/2026 Serikali ilitenga shilingi bilioni 7.0, kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya karakana ambavyo vitasambazwa katika shule 38 za amali, ikiwemo Shule ya Sekondari Mwamapalala Ufundi. Ununuzi wa vifaa hivi upo hatua za mwisho na vitasambazwa kabla au ifikapo Oktoba mwaka huu wa 2026.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kutenga fedha za ununuzi wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia masomo ya amali kadiri ya mahitaji na upatikanaji wa fedha utakapokamilika. Ninakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Njalu Daudi Silanga, swali la nyongeza.

**MHE. NJALU D. SILANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza, ninaishukuru Serikali kwa jinsi wanavyopanga fedha, ili kupeleka katika maeneo yetu ndani ya hizo shule 28. Swali langu ni je, ni kiasi gani cha fedha kitakachotengwa, kwa ajili ya kupeleka vifaa hivyo vinavyohusika kwenye Shule ya Mwamapalala?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Ni kiasi gani cha fedha kitakachotengwa kwenda kukamilisha karakana ya umeme, uchomeaji na vitu vingine vinavyotajwa katika mnyororo mzima wa shule hiyo ya amali?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema kwenye jibu la msingi. Ni kwamba, Serikali imetenga shilingi bilioni 7.0, kwa ajili ya *bulk procurement* ya vifaa hivi kwa hiyo, hatujasema kila shule itapelekewa shilingi ngapi, lakini tumesema vifaa vitapelekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi vifaa vinavyonunuliwa kwa jumla ya shilingi bilioni saba vitagawanywa kwenye shule hizi 38 za amali, ili kuzifanya ziwe na vifaa ambavyo vijana hawa, ambao wanasoma mambo haya ya uhandisi, wapate vifaa hivyo. Shule hii ya Mwamapalala ina fani tatu muhimu ambazo ni fani ya mabomba, fani ya uashi na fani ya ufundi mbao kwa hiyo, vifaa vitakavyopelekwa pale ni vya kujifunzia shughuli ya *plumbing*, uashi na mbao *(carpentry);* hatujasema ni shilingi ngapi kwa kila

shule, bali tutapeleka vifaa hivyo kadiri vitakavyokuwa vimepatikana. Ninakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Oscar Kikoyo, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Jimbo la Muleba Kusini, tunashukuru, tumepewa shule ya amali, lakini miundombinu hasa karakana, zote hazijajengwa. Je, tukianza kununua vifaa kabla ya kukamilisha majengo ya msingi ya hizi shule za amali hatuoni kwamba, shule zingine zinakwenda kupiga hatua wakati nyingine zitabaki nyuma?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye jibu langu la msingi nimezungumzia shule 103 za amali ambazo zimeanza ujenzi wake na nyingine zimekamilika. Hizi shilingi bilioni saba nilizozizungumzia zinapelekwa kwenye shule 38 ambazo zimekamilika. Kwenye Jimbo la Muleba Kusini tutaendelea kukamilisha ujenzi wa shule ile na baada ya hapo tutapeleka vifaa, ili wanafunzi watakaoanza kusoma kwenye shule ile waanze na vifaa vya karakana vikiwepo. Nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, maswali mafupi. Mheshimiwa Clayton Chipando, swali la nyongeza.

**MHE. CLAYTON R. CHIPANDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza kwa Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI. Kwanza, tunaipongeza Serikali kwa kutujengea shule nzuri sana pale *Airport,* katika Kata ya Katubuka, lakini hatari iliyopo pale ni shule ile inaenda kumezwa na maji yanayotokana na mafuriko ya Bwawa la Katubuka. Serikali ina mpango gani wa kuondoa yale maji, ili kuiokoa shule yetu, ambayo tumeweka hela nyingi katika Manispaa ya Kigoma, Ujiji? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza sana Mheshimiwa Chipando kwa namna anavyowasemea wananchi wa jimbo lake. Leo naona hajanitia shoti.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu kwamba, kuna Bwawa lile la pale Katubuka ambalo haliungani na Ziwa Tanganyika. Linapojaa, maji yake huwa yanasambaa kwenye maeneo ya wananchi mpaka kwenye ile shule, ambayo Mheshimiwa Chipando ameitaja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jana tu wataalamu wa TAMISEMI pamoja na wa halmashauri wamekaa, ili kuona ni namna gani fedha ya *TACTIC* iliyoko kule itaweza kutumika kujenga mtaro, ambao utatoa na kuyapeleka kule kwenye Ziwa, ili bwawa lile lisiwe linajaa maji wakati wote. Kwa hiyo, tutakaa na Mheshimiwa Chipando baada ya kupata taarifa ya wataalamu ambao wamekaa jana, ili ku-*share* naye na yeye kuwapelekea wananchi namna tunavyotaka kuondoa adha ya maji yanayojaa kwenye Bwawa lile la Katubuka. Ninakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea! *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, lakini na mimi pia nachukua fursa hii, kama alivyosema Mheshimiwa Waziri Mkuu, kumpongeza sana Mheshimiwa Deogratius John Ndejembi kwa kuteuliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tunamuahidi kufanyanaye kazi kwa juhudi na maarifa. Ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora.

Ninamwita Mheshimiwa Juma Othman Hija, Mbunge wa Tumbatu, sasa aulize swali lake.

Na. 23

**Idadi ya Kaya Zilizonufaika na Mpango wa *TASAF* Mkoa wa Kaskazini Unguja**

**MHE. JUMA OTHMAN HIJA** aliuliza:-

Je, kaya ngapi za Mkoa wa Kaskazini Unguja zimenufaika na Mpango wa *TASAF* katika kipindi cha mwaka 2025? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Utumishi. Mheshimiwa Regina Ndege Qwaray, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Ninaomba uniruhusu na mimi nitumie sekunde chache kuungana na Mheshimiwa Waziri Mkuu kumpongeza Mheshimiwa Deogratius Ndejembi kwa kuaminiwa na Mheshimiwa Rais kuwa mteule katika nafasi ya Makamu wa Rais. Sisi, kama Naibu Mawaziri, Mawaziri na Waheshimiwa Wabunge, tunamuombea kila la heri. Tunamuomba Mwenyezi Mungu ampe ujasiri aweze kumsaidia Mheshimiwa Rais katika majukumu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa uniruhusu nijibu swali la Mheshimiwa Juma Othman Hija, Mbunge wa Tumbatu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Kaskazini Unguja una Kaya 10,504 zilizonufaika na Mpango wa *TASAF*. Kati ya kaya hizo, zilizonufaika na Mpango wa *TASAF* katika Mkoa wa Kaskazini Unguja, Kaya 7,233 zimeshiriki katika miradi ya ajira za muda na Kaya 2,680 zimeshiriki katika shughuli za kukuza uchumi wa kaya kutegemeana na sifa na uwezo wa kaya husika. Ninashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Juma Othman Hija, swali la nyongeza.

**MHE. JUMA OTHMAN HIJA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Ninaishukuru Serikali kwa majibu yake mazuri ya swali hili, lakini nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa *TASAF* ni miongoni mwa mipango mizuri ya Serikali, ambayo inawawezesha wananchi katika maisha yao ya kawaida, lakini kumekuwa na malalamiko madogo madogo kutoka kwa wanakaya juu ya namna ya kupata mpango huo. Je, ni vigezo na sifa gani zinahitajika kwa wanakaya, ili kupata mpango huu wa *TASAF*? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Juma Othman Hija, kama alivyouliza. Utaratibu wa kupata kaya za walengwa ni shirikishi. Kumekuwa na utaratibu wa kushirikisha jamii, wananchi pamoja na Serikali za Mitaa kwa sababu, ndiyo wanaowafahamu zaidi walengwa kwa hiyo, kwa kutumia vigezo vya kuangalia kiwango cha umaskini katika kaya ndipo wanateuliwa, ili kuingia kwenye ule mfumo wa *TASAF*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, Serikali imeendelea kuweka mfumo mzuri wa kuhakikisha unafuatilia Mpango wa *TASAF* kwa walengwa waliowekwa kwenye mpango, ili kuhakikisha ambao wamewekwa ni wale hasa wanaostahili kuwepo kwenye mpango wa *TASAF*. Pale inapogundulika kwamba, walengwa walioingizwa kwenye mfumo siyo wenye sifa au hawajakidhi vigezo, basi wanatolewa mara moja, ili kutoa nafasi kwa wale walengwa wenye sifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, Serikali kwa kupitia *TASAF,* imeendelea kuwafuatilia kwa ukaribu, ili kugundua kama kuna

sehemu ambayo watu ambao hawana sifa wameingizwa. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tamima Abass, swali la nyongeza.

**MHE. TAMIMA HAJI ABASS:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi. Lengo la Mfuko wa *TASAF* ni kusaidia au kuokoa kaya masikini ndani ya jamii zetu. Je, Serikali imejipangaje au imefanya tathmini kuhakikisha lengo hilo limefikiwa kwa wananchi wetu? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge. Ni kweli kwamba, *TASAF* ilianzishwa, kwa ajili ya kusaidia kaya masikini; kuwatoa katika hali ya umasikini na kwenda katika hali ya kujitegemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, Serikali katika utekelekezaji wa Mpango wa Pili wa *TASAF* imekwenda kwa walengwa milioni 1.4, ambao tayari wamenufaika na mpango wa *TASAF*. Katika hao, walengwa 4,000 wamehitimu; wameweza kujitegemea kiuchumi kwa maana wanaweza kupata yale mahitaji muhimu kama afya, elimu, chakula na malazi. Kwa hiyo, kama alivyouliza, Mheshimiwa Mbunge ni kwamba, *TASAF* lengo lake ni kumtoa mtu katika kaya masikini na kuanza kujitegemea, lakini kwa kuzingatia vigezo. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji. Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 24

**Mkakati wa Kuvutia Wawekezaji katika Kilimo cha Chai na Viwanda**

**MHE. SUMA I. FYANDOMO** aliuliza:-

Je, nini mkakati wa Serikali wa kuvutia wawekezaji katika kilimo cha chai na viwanda?

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji. Mheshimiwa Dkt. Chaya, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaendelea nachukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Deogratius John Ndejembi kwa kuaminiwa na Mheshimiwa Rais kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sisi, kama Naibu Mawaziri, tunaahidi kumpa ushirikiano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema haya, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mbeya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kutangaza fursa zilizoko kwenye sekta ya kilimo na uchakataji wa mazao, kama maeneo ya kipaumbele katika uwekezaji. Katika kilimo cha chai, mkakati ni kuvutia uwekezaji katika uzalishaji, uchakataji, ufungashaji, uhifadhi na uongezaji thamani kwa masoko ya ndani na nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali, kupitia Mamlaka ya Uwekezaji na Maeneo Maalum ya Kiuchumi Tanzania *(TISEZA)*, imeweka vivutio vya kikodi na visivyo vya kikodi kwa wawekezaji wanaowekeza katika mnyororo mzima wa chai, ili kupunguza gharama za uwekezaji, kuzalisha, kuongeza mapato ya wakulima,

kuongeza ajira na kupata fedha za kigeni kutokana na mauzo ya nje na kuleta teknolojia mpya katika uzalishaji wa chai. Ninaomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo, swali la nyongeza.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa majibu mazuri ya Serikali.

Ni nini mkakati wa Serikali wa kuwavutia wawekezaji ili waje kuwekeza kwenye viwanda vya chai vilivyopo Wilaya ya Rungwe, kiwanda cha Msekela, kiwanda cha Chivanje na kiwanda cha *WATCO*, kwa kuwa wakulima ni wengi sana wanaolima chai kwenye Wilaya ya Rungwe?

Swali la pili, kiwanda cha Msekela, mwekezaji alinunua pia mashamba ya kiwanda cha Msekela. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuongea naye ili aone namna ya kuyaachia hayo mashamba, atafutwe mwekezaji mwingine ili wananchi wa Wilaya ya Rungwe waweze kupona kwa namna ambavyo wanategemea sana kilimo cha chai kwenye Wilaya ya Rungwe?

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mbeya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Fyandomo, amekuwa akiuliza sana maswali hapa Bungeni, lakini kimsingi amekuwa akiwatetea sana wakulima wa chai wanaotoka katika Mkoa wa Mbeya. Sanjari na hivyo, Mbunge kutoka Jimbo la Rungwe, Mheshimiwa Mwantona, vilevile amekuwa akinisumbua sana kuhusu hawa wakulima wa chai na niwahakikishie kwamba Serikali ipo pamoja nao.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo sasa ninaomba nijibu maswali mawili, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la kwanza, kama Serikali kwa kushirikiana na wenzetu wa Wizara ya Kilimo, tunao mkakati wa kuhakikisha kwamba tunafufua kile kiwanda cha *WATCO* na vile viwanda vingine ambavyo Mheshimiwa Mbunge amevisema. Hivi sasa tunatafuta wawekezaji na tayari tumeshaanza mkakati wa kutafuta wawekezaji wa ndani na wa nje, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge ndani ya muda mfupi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, kwa kushirikiana na wenzetu wa Kilimo, tutahakikisha kile kiwanda kinaanza kufanya kazi ili kuwasaidia wakulima wa chai katika Mkoa wa Mbeya.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili, ni kweli katika eneo la Rungwe, hususan Mkoa wa Mbeya, kuna mwekezaji ambaye kimsingi alinunua eneo kubwa sana, zaidi ya ekari 2,000 na ni zaidi ya miaka mitano ama kumi huko imepita, Mheshimiwa Rais wakati wa kampeni alitoa maelekezo kwamba tufanye tathmini ili tuone kama yule mwekezaji ana-*capacity* ya kuendeleza yale mashamba. Serikali tayari tumeshaanza kufanya tathmini kwa kushirikiana na wenzetu wa Wizara ya Kilimo, lakini ninaomba nimwelekeze Mkurugenzi Mtendaji wa *TISEZA* wakamilishe hiyo tathmini haraka ili maamuzi sahihi ya Serikali yaweze kufanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Pindi Chana, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri sana ya Serikali kwamba kuna vivutio vya kikodi na visivyo vya kikodi kwa wawekezaji hawa wa chai, Mkoa wa Njombe ni miongoni mwa Mikoa ambayo inalima sana chai nchini, ukichukua katika maeneo ya Lupembe, Luponde, Madope, Wemba, Mlangali na maeneo mengine.

Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha wawekezaji hawa kwa jinsi ambavyo tunawapa vivutio vizuri, wanawalipa wakulima wetu wa chai kwa wakati, kiwango kinachostahili, pia wananunua ile chai kadri wanavyolima na kuvuna?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Pindi Chana, Mbunge kutoka Mkoa wa Njombe kwa kuwatetea wananchi wa Njombe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli ninatambua kwamba wananchi wa Njombe siyo tu wakulima wa chai, vilevile wanalima mazao mbalimbali yakiwemo parachichi na kadhalika. Serikali, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, tumekuwa tukishirikiana sana na wenzetu wa Wizara ya Kilimo kuhakikisha kwamba tunatafuta wawekezaji hususan kwenye zao la parachichi vilevile na mazao ya chai, ikiwa ni pamoja na kuhakikisha tunapata wawekezaji wenye tija ambao kimsingi watahakikisha ile *value chain* yote ya chai inakuwa na thamani na tunawasaidia wakulima wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba sisi kama Serikali, mawazo yake, maoni yake na ushauri wake tutaufanyia kazi kwa maslahi ya wananchi wetu. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ester Bulaya, swali la nyongeza.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami ninashukuru kwa kupata nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Mji wa Bunda ina eneo kubwa kwa ajili ya uwekezaji na limekaa takribani miaka kumi, wananchi walishalipwa fidia. Nini mkakati wa Serikali kuwekeza kwenye eneo lile ili kuchachusha uchumi wa Halmashauri ya Mji wa Bunda na vijana wa Bunda na akina mama waweze kupata ajira?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Ester Bulaya, hii ni mara yake ya tatu kuliuliza hili swali la eneo la uwekezaji la *Bunda SEZ*. Na leo ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na nimpe taarifa nzuri kwamba tayari Serikali imeshapata wawekezaji wawili ambao ni wawekezaji wakubwa na wameshaanza kusafisha eneo pale *Bunda SEZ*. Wawekezaji hao wapo kwenye maeneo mawili wa kwanza anawekeza kwenye viwanda vya kuchakata nyama, lakini machinjio, lakini masuala ya ufungashaji lakini wa pili anawekeza kwenye suala la *value chain* ya samaki. Ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba sisi kama Serikali, *Bunda SEZ* ni mojawapo ya maeneo ya kipaumbele. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Johannes Lukumay, swali la nyongeza.

**MHE. JOHANNES L. LUKUMAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza kwa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kwa ridhaa yako niruhusu nami nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kupendekeza jina la Mheshimiwa Ndejembi kuwa Makamu wa Rais, pia nimpongeze sana Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya, kwa kufanya ziara katika Jimbo la Arumeru Magharibi, kutembelea sekta binafsi, kiwanda cha kutengeneza bidhaa za afya. Nakushukuru sana.

Swali, Jimbo la Arumeru Magharibi ni lango kuu la utalii Kanda ya Kaskazini, nini mkakati wa Serikali wa kuvutia wawekezaji wa kujenga hoteli za nyota tatu au tano katika eneo la Engorika, Kata ya Kiutu ili kuvutia watalii? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Johannes Lukumay, Mbunge wa Arumeru Magharibi, kwanza kwa maswali yake lakini ni kweli nilitembelea Jimbo la Mheshimiwa Dkt. Lukumay na kwa kweli nikupongeze sana, una wawekezaji wengi sana kikiwemo kile kiwanda cha dawa ambacho kinakuja kuwekeza Tanzania, ninakupongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Arumeru Magharibi ni sehemu ya Mkoa wa Arusha, na kama tunavyotambua Arusha ni kati ya Mikoa ambayo tunaitegemea sana kwa utalii. Katika vipaumbele vyetu na mikakati yetu ya kuvutia wawekezaji kwenye suala la utalii, eneo la Arumeru ni mojawapo ya maeneo ambayo tumeanza kuyafanyia kazi kuhakikisha tunavutia wawekezaji wa kujenga hoteli za kisasa, hoteli za nyota tano, hoteli za kitalii ili kuweza kukuza uchumi wa nchi, uchumi wa Arumeru, vilevile tuongeze kipato kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali tutalifanyia kazi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Maliasili na Utalii, sasa namwita Mheshimiwa Nuru Issa Kashakari, Mbunge wa Kigoma Kusini, aulize swali lake.

Na. 25

**Kumaliza Mgogoro Kati ya Hifadhi ya Mahale na Wananchi**

**MHE. NURU I. KASHAKARI** aliuliza:-

Je, lini Serikali itamaliza mgogoro kati ya Hifadhi ya Mahale na wananchi katika Jimbo la Kigoma Kusini?

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Ernest Silinde, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO K.n.y. WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Mimi pia niungane na wote ambao tunampongeza Mheshimiwa Deogratius Ndejembi kwa kuteuliwa kushika nafasi ya Makamu wa Rais na kwa kweli sisi kama Naibu Mawaziri tunamuunga mkono kuhakikisha kwamba anafanya kazi ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Nuru Issa Kashakari, Mbunge wa Kigoma Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Hifadhi ya Taifa ya Milima Mahale ina mgogoro na Kijiji cha Kalilani hususan kwenye vitongoji viwili vya Mahasa na Kabukuyungu. Kufuatia tathmini ya kina iliyofanywa na Kamati ya Mawaziri Nane wa Kisekta, Serikali kupitia Uamuzi wa Baraza la Mawaziri (BLM) wa Tarehe 23 Septemba, 2019 iliamua kuwa wananchi wanaoishi katika vitongoji vya Mahasa na Kabukuyungu, wahamishwe kwa ajili ya kupisha shughuli za uhifadhi kwa kufanya uthamini wa mali zao na kuwalipa fidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha mgogoro baina ya wananchi na Hifadhi ya Taifa Milima Mahale unamalizika, Serikali imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ikiwemo kulipa fidia kwa wananchi wanaotakiwa kupisha shughuli za uhifadhi ambapo hadi sasa jumla ya kaya 205 kati ya kaya 376 zimefanyiwa uthamini na kulipwa jumla ya shilingi bilioni 1.6, kutoa elimu na kufanya uhamasishaji kwa kaya 171 ambazo hazijafanyiwa uthamini ili ziweze kulipwa fidia na hatimaye kukamilisha zoezi la kupisha shughuli za uhifadhi na kuandaa Mpango wa Matumizi ya Ardhi kwa maeneo yaliyobaki ya Kijiji cha Kalilani (Vitongoji vya Katumba, Storo na Kalolwa) ili kuondoa mwingiliano wa matumizi ya ardhi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nuru Issa Kashakari, swali la nyongeza.

**MHE. NURU I. KASHAKARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninaipongeza Serikali kwa majibu mazuri aliyoyajibu Naibu Waziri, lakini pia nikupongeze na wewe binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kijiji cha Kalilani katika Wilaya ya Uvinza, mgogoro huu ni wa takribani miaka 30 mpaka sasa hivi, lakini wale wananchi wa pale wamekuwa wakipitia madhila mengi sana na mitihani mingi sana.

Je, ni lini Serikali itamaliza mgogoro huu kama alivyozungumza kwamba tayari wameshaanza kulipa fidia. Je, ni lini Serikali itamaliza mgogoro huu ili sasa wananchi nao waanze kupata manufaa kwenye nchi yao?

Swali la pili, nimekuwa nikiona sehemu mbalimbali hapa nchini watu wakiondolewa katika maeneo yao wakipewa fidia, lakini baada ya kupewa fidia huwa wanaonyeshwa na mahala pengine pa kwenda kujenga. Kwa sababu wananchi wa pale kama nilivyosema kwenye swali la msingi kwamba wana miaka takribani 30 wanakimbizwa, wanapigwa, wananyanyaswa, wanapelekwa huku na kule, hawalimi wala hawajengi, hawana kipato chochote, hata kama mkiwalipa hizo fedha, hizo fidia hazitawakidhi.

Je, kuna mpango upi wa Serikali kuhakikisha kwamba wale wananchi wa pale wanatengewa maeneo mengine ili mkiwalipa hizo fidia waende wakajenge huko wanakokwenda? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO K.n.y. WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshukuru sana Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Kigoma Kusini, kaka yangu Nuru Issa Kashakari kwa maswali yake madogo mawili ya msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamthibitishia tu kwamba moja ya jitihada za Serikali ni kuhakikisha mgogoro huu unaisha kwa wakati, na ndiyo maana katika kaya 376 tayari kaya 205 zimelipwa fidia na zimeondoka katika eneo lile. Jukumu lililobaki ni kuhakikisha hizi kaya 171 zinaondoka na ndiyo maana imeundwa Kamati maalum ambayo inaenda kuendelea kuwapa elimu, ambayo ilitokana na upotoshwaji ambayo imefanya hizi kaya walikuwa wanataka kama kugomea lile zoezi. Kwa hiyo Kamati inafanya kazi na ikishamaliza maana yake sasa tutawalipa fidia ambayo inaendana na kiwango cha sasa ili wanapokwenda kule waweze kupata makazi na waanzishe maisha mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile jukumu la Serikali ambalo ililifanya wakati wa mchakato huu kupitia ofisi ya Mkuu wa Mkoa na Halmashauri ya Uvinza walitenga eneo lenye ukubwa wa hekta 2,000 katika vitongoji vya Kalolwa na Katumba Storo ambapo maeneo yale yametengwa kwa ajili ya hawa wananchi ambao wanataka kuhamia ambayo ni makubwa zaidi kuliko eneo la hekta 20 ambalo walikuwa wanakaa pale awali. Kwa hiyo, eneo lipo limetengwa kwa ajili yao na wale wote watakaohamia wataenda kukatiwa maeneo pamoja na kulipwa fidia ya kuhamia maeneo hayo. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kiza Mayeye, swali la nyongeza.

**MHE. KIZA H. MAYEYE:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo la Kigoma Kaskazini, Kata ya Mkongoro, Bitale, Kalinzi na Nyarubanda, kuna Bonde la Shunga na Mshunuzi. Wananchi wa maeneo hayo wamekuwa wakinyanyaswa, wakifukuzwa wakiambiwa kwamba wamevamia hifadhi ya Gombe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka kujua, ni lini mgogoro wa Gombe na wananchi wa Kata hizi utaisha? Je, Waziri upo tayari kufika Jimbo la Kigoma Kaskazini mara baada ya Bunge

kuahirishwa ili uone changamoto wanayoipitia wananchi wa Kigoma Kaskazini katika Kata hizi? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kuna maswali mawili, kuna kuelezea mgogoro na kuna ziara, sasa jibu moja.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO K.n.y. WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ninakubali kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii kufika eneo hilo na kujadili na wale wananchi kuhusu mgogoro wa eneo la Gombe ili kuweza kupata ufumbuzi wa kudumu. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Edibily Kinyoma, swali la nyongeza.

**MHE. EDIBILY K. KINYOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Waziri, Jimbo la Kasulu Vijijini lina changamoto ya migogoro ya ardhi ambayo inahusisha hifadhi, inafanana kabisa na ile ya Kigoma Kusini. Je, uko tayari kuungana na Waziri wa Ardhi ili mje kwenye Jimbo la Kasulu Vijijini kumaliza migogoro hii?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO K.n.y. WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimthibitishie tu Mheshimiwa Mbunge, Ofisi ya Waziri wa Maliasili na Utalii iko tayari kuongozana na Ofisi ya Waziri wa Ardhi kufika katika eneo hilo kwa ajili ya kupata ufumbuzi wa kudumu. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, swali la Mheshimiwa Katani Ahmadi Katani, Mbunge wa Tandahimba, litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Esther Matiko.

Na. 26

**Ucheleweshaji wa Ujenzi wa Barabara ya Mnivata – Nanyamba – Tandahimba – Masasi**

**MHE. ESTHER N. MATIKO K.n.y. MHE. KATANI A. KATANI** aliuliza:-

Je, nini kauli ya Serikali juu ya kukamilika kwa wakati ujenzi wa Barabara ya Mnivata – Nanyamba – Tandahimba – Masasi?

**NAIBU SPIKA:** Naibu Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa Godfrey Kasekenya, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninaomba niungane na Mheshimiwa Waziri Mkuu kumpongeza Mheshimiwa Deogratius Ndejembi, kwa kuaminiwa kwake na Mheshimiwa Rais kuwa Makamu wa Rais, nami niahidi kwamba tutatoa ushirikiano wa hali ya juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo ninaomba sasa nijibu swali la Mheshimiwa Katani Ahmadi Katani, Mbunge wa Tandahimba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)* inaendelea na kazi ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Mnivata – Tandahimba – Newala – Masasi yenye urefu wa kilometa 160. Utekelezaji wa mradi huu umegawanywa katika sehemu mbili, sehemu ya kwanza ni Mnivata – Mitesa (kilometa 100) ambayo utekelezaji wake umefikia 60% na unatarajiwa kukamilika mwezi Desemba, 2027.

Sehemu ya pili ya Mitesa – Masasi (kilometa 60), utekelezaji wake umefika 75% na unaratajiwa kukamilika mwezi Machi, 2027. Serikali itaendelea kusimamia kwa ukaribu ujenzi wa barabara hii ili ukamilike kwa wakati kulingana na mkataba. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Esther Matiko, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana na nitaenda kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, hii barabara ya Mnivata – Nanyamba – Tandahimba – Masasi ambayo ilitarajiwa kukamilika mwezi wa 10 kwa jinsi nilivyoambiwa na Mheshimiwa Katani, yenye kilometa 160 mpaka sasa imekamilika kilometa 29 tu. Sasa Mheshimiwa Katani pamoja na wananchi wa maeneo haya wangependa kujua Serikali inatumia mkakati gani kuhakikisha kwamba barabara hii inakamilika kama ambavyo imeelekezwa, *deadline* itakavyokuwa, ili hii barabara iweze kutumika kwa sababu ni barabara ya kiuchumi na inaunganisha Wilaya kama ilivyoainishwa?

Swali la pili, barabara ya lami ya kutoka *keep left* – Mogabiri iliyopo Tarime Mjini ni barabara ya kiuchumi, kijamii kwa sababu inaunganisha wananchi kutoka Tarime Mjini kwenda mpaka Serengeti kwenye ile mbuga yetu lakini pia ipo mpakani, kwa sababu mwezi Machi, 2026 alikuja Waziri wa Ujenzi akaongea na wananchi wa Tarime Mjini na akawaahidi kwamba barabara ile inaenda kutekelezwa mapema sana iwezekanavyo, lakini mpaka sasa hivi ninavyoongea mkandarasi bado hajarudi *site*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka kujua ni lini Serikali itahakikisha inapeleka fedha ili ianze utekelezaji wa barabara ile muhimu sana ambayo ni kilometa 9.3 tu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Mheshimiwa Esther Matiko kwa maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli barabara hii ya Mnivata - Tandahimba, Mitesa hadi Masasi ilitakiwa iwe imekamilika, lakini barabara hii ilichelewa kuanza kwa sababu mbalimbali. Barabara hii inafadhiliwa na wenzetu wa *ADB* ambao tunasaidiana nao kujenga hiyo barabara. Kwa hiyo, wakati wa kuanza kimsingi tulichelewa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wote wa Tandahimba, Mtwara, Masasi na Newala na watakuwa mashahidi kwamba, katika vipande hivyo vyote viwili, Mnivata – Mitesa na Mitesa – Masasi, wakandarasi wote wawili sasa hivi kwa kweli kasi yao ni kubwa sana, ndiyo maana tumekwenda 60% kwa 75%, na tuna uhakika kwamba tutakamilisha baada ya kuongeza muda, kwa muda ambao tumewapangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi utakubaliana na mimi kwamba, tayari sehemu kubwa ya barabara nchi hii tumeshakamilisha, sasa hivi tunaweka lami katika vipande vyote hivyo viwili kuhakikisha kwamba hii barabara ya uchumi inakamilika kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu barabara ya Tarime – Mogabiri, ni kweli Waziri alitembelea kule, tutaikamilisha na tutapeleka fedha. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Esther Matiko kwamba, ahadi ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi iko pale pale, kama alivyosema Mheshimiwa Waziri Mkuu wakati anajibu moja ya maswali hapa, Wizara ya Fedha kwa kweli imeshatekeleza ile ahadi ya kutuletea fedha moja kwa moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kuna fedha za matengenezo kwa maana ya *Road Fund,* pia kuna fedha ya yale madai ya wakandarasi wa nyuma, ikiwemo na yale madai ya watu wa *advance payment*. Ninavyoongea sasa hivi tumeshapokea fedha ambazo tayari tumeshaanza kugawa kwenye barabara zilizokuwa ama zimesimama, ama hazijapewa *advance,* kwa hiyo, tumeshaanza. Nina hakika Mheshimiwa Esther Matiko, hiyo barabara yako itakuwa ni barabara mojawapo ya

kipaumbele na hasa kwa sababu Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi alikuja na akaahidi mbele yako na mbele ya wananchi.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Waheshimiwa Wabunge ninaomba maswali yawe mafupi. Mheshimiwa John Luhende, swali la nyongeza.

**MHE. JOHN S. LUHENDE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na tatizo kubwa la barabara zetu hizi ambazo ziko chini ya *TANROADS*. Mfano, Barabara ya Nzega - Tabora, Tabora - Manyoni mpaka Dodoma, uwepo wa mashimo yanayosababisha ajali mbalimbali, mfano mzuri, mimi mwenyewe usiku wa kuamkia jana tumelala usiku porini kwa sababu ya ubovu wa barabara, tairi yetu ilipata pancha baada ya kuingia shimoni.

Swali la msingi ni kwamba, Serikali au Wizara ni lini mtawasimamia ipasavyo watendaji wa *TANROADS* ili wafanye kazi yao ya *maintenance* kwenye barabara hizi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba tunazo barabara nyingi sana ambazo zimechakaa, naamini Mheshimiwa Mbunge nadhani ni Mjumbe pia wa Kamati ya Miundombinu, ndiyo maana hata katika Bunge letu la Bajeti tuliomba fedha kwa wenzetu wa Hazina na tuna utaratibu ambao tunaendelea nao kupata fedha ili tuweze kukarabati barabara nyingi ambazo kwa kweli sisi sote tunapita zimechoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, mipango inakwenda vizuri kati ya Wizara ya Ujenzi na Wizara ya Fedha kuona namna gani tunaweza tukapata fedha kwa wingi ili maeneo yote korofi ambayo yamechoka tuweze kuyakarabati kwa kiwango cha hali ya juu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara tumeshatoa maelekezo kwa wenzetu wa *TANROADS* kwamba, tutakapopata hizo fedha hakika tuhakikishe kwamba zinasimamiwa na zinatengenezwa katika kiwango ambacho kimesanifiwa. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mabula Magangila, swali la nyongeza.

**MHE. MABULA J. MAGANGILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Nyambula – Nyang'holongo ni barabara ambayo ni kiunganishi kikubwa kati ya Jimbo la Msalala kwa maana ya Wilaya ya Kahama na Wilaya ya Nyang'hwale. Barabara hii inatumika kwa shughuli za uzalishaji, shughuli za madini, pia shughuli za usafirishaji wa abiria kuunganisha hizi Wilaya mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, msimu uliopita wa mvua barabara hii ilikuwa imekatika, ilitusumbua sana, Bunge lililopita niliuliza swali hapa na Mheshimiwa Waziri akasema barabara ianze kutengenezwa mara moja, mpaka leo barabara hii haijaanza kutengenezwa na msimu wa mvua unakaribia kuanza tena kwenye hiyo barabara.

Je, ni nini kauli ya Serikali kwa barabara hii ambayo ni muhimu sana kwa uchumi wa wananchi wa Msalala? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge na mimi nilishapata taarifa kuhusu hii barabara ya Nyambula – Nyang'holongo – Nyang'hwale kwenda Busisi. Moja, hii barabara ipo kwenye mipango ya kusanifiwa yote pia kwa sababu imeharibika, fedha ambazo Waheshimiwa Wabunge watakumbuka walikuwa wanaziomba ni fedha za matengenezo ziende moja kwa moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tunavyoongea sasa hivi, Serikali imetimiza ile ahadi, *Road Fund* kwa maana ya kupata fedha za matengenezo tumeshazipokea kama zinavyotakiwa. Kwa hiyo, naomba

nimwelekeze Meneja wa *TANROADS* kuhakikisha kwamba, katika mgao wa kwanza ama wa pili kabla ya mvua kuanza, ahakikishe kwamba hii barabara ya Nyambula – Nyangh'olongo kwenda Nyang'hwale inawekwa kwenye mpango wa kutengenezwa haraka iwezekanavyo. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Festo Sanga, swali la nyongeza.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri, unafahamu kwamba ajenda ya kudumu ya Makete ni barabara ya Makete – Mbeya, *speed* ya mkandarasi iko chini sana. Wananchi wa Makete wanauliza ni lini *speed* ya mkandarasi itaongezeka ili barabara hii iweze kupitika na iweze kujengwa kwa kiwango cha lami kama ambavyo Serikali imekusudia? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mkandarasi ameshapewa, nimwelekeze tu Meneja wa *TANROADS* Mkoa wa Njombe na sasa kwa kuwa bado tumeshatoa maelekezo Mtendaji Mkuu aweze kuwasiliana na Meneja wa *TANROADS* Mkoa wa Njombe, kama mkandarasi ana fedha, hana sababu ya kuwa na *speed* ndogo na hasa tukielewa kwamba kipindi hiki kwa Mikoa ya Njombe ndiyo kipindi cha kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nitumie nafasi hii kumwelekeza Mtendaji Mkuu wa *TANROADS* kuhakikisha kwamba, anakwenda kuona changamoto ni nini kwa huyu mkandarasi kwenda taratibu wakati hiki hasa ndiyo kipindi cha kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakuomba Mheshimiwa Mbunge, pengine baada ya hapa tukutane tuone kama kuna changamoto, ikiwezekana niweze kufanya ziara kuangalia nini hasa ni changamoto. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, nimekuona Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa Ulega.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuongezea majibu mazuri sana anayoyatoa Mheshimiwa Naibu Waziri wangu Injinia Kasekenya Msongwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba uniruhusu pia kuungana na Mheshimiwa Waziri Mkuu kumpa pongezi nyingi sana na kumtakia heri nyingi *Comrade* Deo Ndejembi, kwa kuteuliwa kwake na kuaminiwa na Chama chetu Cha Mapinduzi kuwa Makamu wa Rais Mteule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nilitaarifu Bunge ya kwamba, sisi Wizara ya Ujenzi tunalishukuru sana Bunge hili Tukufu, katika miezi michache iliyopita mlipitisha Sheria ya Fedha za Mfuko wa Barabara na Bunge lilitoa maelekezo ya kwamba, fedha hizo ziende moja kwa moja katika Mfuko wa Barabara. Ninayo heshima na kwa taadhima kubwa nakushukuru wewe, Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge wote, bila ya kusahau Kamati yetu ya Bunge ya kwamba Serikali inatekeleza jambo lile sasa kwa vitendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwezi wa Julai na sasa Agosti, jumla ya fedha shilingi bilioni 106 zimeingia moja kwa moja kutoka *TRA* na kuja katika Mfuko wa Barabara. Maana yake ni nini? Maana yake ni kwamba, kuanzia sasa wataalam wetu *TANROADS* wamejipanga vizuri kuhakikisha kuwa barabara zote ikiwemo barabara ya Babati, Dareda *Mission* mpaka Singida zinafanyiwa marekebisho ili kuondoa yale mashimo yaliyosemwa na Mbunge kutoka Tabora vilevile, kwamba barabara zetu nyingi zimeharibika sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kupitia fedha hizo *TANROADS* imejipanga kukabiliana pia mvua za *El-Nino* zinazokuja hapa mbele ili kuhakikisha barabara zetu zinaendelea kupitika wakati wote. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri, ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, mliowasha *microphone* halafu mnazungumza, mnasikika huko nje. Kwa hiyo, washa *mic* wakati unataka kuuliza swali la nyongeza, mnawasha *mic* mnazungumza mnasikika huko nje.

Tunaendelea Wizara ya Uchukuzi, Mheshimiwa Mariam Abdallah Ibrahim, Mbunge Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 27

**Ujenzi wa Bandari ya Kisiju – Mkuranga**

**MHE. MARIAM A. IBRAHIM** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga Bandari ya Kisiju iliyopo Wilaya ya Mkuranga, Mkoa wa Pwani?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uchukuzi, Mheshimiwa David Kihenzile, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niungane na Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Waheshimiwa Mawaziri kumpongeza sana Mheshimiwa Deogratius John Ndejembi kwa kuaminiwa na Chama chetu na Mheshimiwa Rais kuwa Makamu wetu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya utangulizi huo, kwa niaba ya Waziri wa Uchukuzi Mheshimiwa Profesa Makame Mbarawa Mnyaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Maryam Abdallah Ibrahim, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania *(TPA)* imetenga bajeti ya shilingi bilioni mbili katika mwaka huu wa fedha 2026/2027 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa bandari hiyo kwa kuanza na gati dogo na

miundombinu wezeshi ili kuruhusu vyombo vidogo kupata sehemu ya kuegesha.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, mpango wa muda mrefu unaandaliwa ili kufanya upembuzi yakinifu, utakaobainisha namna bora ya kujenga bandari mahsusi katika eneo hilo ambalo lipo Kaskazini mwa Delta kubwa ya Mto Rufiji na lina sifa ya kuwa na mito midogo midogo ya asili na mikondo ya maji inayopita katika vijiji vya jirani ukiwemo Mto Mbezi, ambayo inasababisha changamoto ya kujaa kwa mchanga *(siltation)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mariam Abdallah Ibrahim, swali la nyongeza.

**MHE. MARIAM A. IBRAHIM:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali, ninalo swali moja la nyongeza.

Je, Serikali mara baada ya kukamilisha ujenzi wa gati ya Kisiju Pwani, Bagamoyo, Kibiti na maeneo yote ya Pwani, haioni umuhimu sasa wa kuanzisha usafirishaji wa majini moja kwa moja ambao utatokea Mafia - Kisiju mpaka Dar es Salaam na kutokea Bagamoyo, Mbweni na Dar es Salaam, hii ni kutokana na msongamano mkubwa na ukuaji wa Jiji la Dar es Salaam na Pwani? ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mariam Abdallah Ibrahim kwa jinsi ambavyo anafuatilia kwa ukaribu sana usafiri na usafirishaji katika ukanda wa bahari ambao wananufaika watoto kwa wazee, lakini pamoja na vijana, lakini hususan wanawake ambao yeye anawawakilisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimkumbushe Mheshimiwa Mbunge pamoja na Waheshimiwa Wabunge kwamba, Serikali inatambua uelekeo wa nchi yetu hasa katika Dira ya 2050, ambapo moja ya vichocheo muhimu vya uchumi na maendeleo

ambayo Tanzania inaota kuyafikia ni kuhakikisha kwamba, tunakuwa na usafirishaji fungamanishi ili kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kufanya hivi, yapo mambo yamekwishaanza kufanyika. Moja, maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuhakikisha kwamba sekta ianze kujipanga kutekeleza hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbili, Ilani ya CCM ya Mwaka 2025/2030 kifungu cha 2 (44) imeainisha maeneo ya msisitizo ikiwa ni sambamba na ujenzi wa vivuko pamoja na meli. Tatu, Waziri wetu, Mheshimiwa Prof. Mbarawa, amenituma leo niliarifu Bunge kwamba, katika bajeti yetu hii ya mwaka 2026/2027 tumetenga fedha bilioni kumi ikiwa ni kwa ajili ya kuanza ujenzi wa meli kwenye ukanda wa Bahari ya Hindi, hii ni baada ya kukamilika usanifu wa kina ambao umeonesha kwamba biashara hiyo inalipa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge makini kabisa, Mheshimiwa Mariam kwamba awe na Subira. Tunapoanza utekelezaji wa ujenzi wa meli hii ambayo itakuwa ni ya mizigo, ni mwanzo mwema wa kuchukua pia ushauri wake na Waheshimiwa Wabunge wengine kuhakikisha kwamba, tunaanza pia kufikiria kwa ajili ya kwenda kutengeneza usafirishaji kwa ajili ya raia pamoja na mambo mengine katika eneo hilo. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbwilo Kapunda, swali la nyongeza.

**MHE. BAZILIO K. MBWILO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaamini kwamba Mheshimiwa Waziri anafahamu fika umuhimu wa bandari mbili za Kipili na Kabwe kwamba, ndizo bandari kuu zinazohusika katika kusafirisha mizigo kutoka Tanzania kwenda nchi Jirani. Bandari hizo zote mbili zimemezwa na maji ya ziwa, kiasi kwamba sasa meli kutoka nchi

jirani haziwezi tena kuja, badala yake mizigo inasafirishwa kwa kutumia maboti, kiasi kwamba tunashindwa kusafirisha mizigo yote inayostahili kwa wakati.

Je, Mheshimiwa Waziri unatuahidi ni lini hizo bandari mbili nilizozitaja zinaweza kurekebishwa ili zirudie *full capacity* yake? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kama alivyoainisha juu ya changamoto ya kujaa kwa maji kwenye bandari zetu, hii nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, siyo tu upande wa Kabwe na Kipili pia Kasanga, ukienda kule Kigoma hata ukienda Ziwa Nyasa mwaka huu tulikuwa na changamoto hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ni jambo ambalo linajitokeza baada ya miaka kama 50, ambapo bandari zetu zimejikuta kwamba zinakumbwa na changamoto ya kujaa kwa maji. Kwa hiyo, hii inatokana na mabadiliko ya hali ya hewa au tabianchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpe pole Mheshimiwa Mbunge kwa changamoto hiyo ambayo kimsingi imesababishwa na mabadiliko ya tabianchi kama nilivyoeleza. Pili, nimweleze kwamba Serikali imelitambua jambo hilo na tayari timu ya wataalamu imeendelea kufanya tathmini ya kina kufahamu namna bora ya kuweza kumaliza changamoto hii ya muda mfupi na muda mrefu, naomba avumilie, tutakapokamilisha tutakuja na mwarobaini na namna bora ya kuweza kumaliza tatizo hili ili wananchi wa Kipili, wananchi wa Kabwe pamoja na maziwa yetu makuu waendelee kunufaika vyema na usafiri katika Ziwa ya Tanganyika na maeneo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, ikizingatiwa kwamba meli yetu ya *MV* Liemba ambayo ilisimama kwa miaka zaidi ya 10, Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan amekamilisha ukarabati wake na kwa sasa inafanyiwa majaribio na muda wowote inaweza kuanza safari zake katika Ziwa Tanganyika.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu ya maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi cha maswali kutoka kwetu na majibu kwa upande wa Serikali, ninaomba niwaletee matangazo yaliyopo mezani.

Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na wageni waliopo Bungeni asubuhi hii. Tunao wageni wa Mheshimiwa Spika ambao ni wageni wanne wa Mheshimiwa Spika kutoka Mkokwa *General Supplies Limited* ya Ilala Mchikichini, Jijini Dar es Salaam ambaye ni Ndugu Rashid Mkokwa, Mkurugenzi Mkuu na Mlezi wa Kampuni, Ndugu Daud Mkawa, Mkurugenzi Mwendeshaji, Ndugu Mussa Katema, Meneja Mahusiano na Ndugu Fatma Mkokwa, Msimamizi Mwendeshaji, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Wageni waliokaa Jukwaa la Spika ni wageni watatu wa Mheshimiwa Profesa Riziki Silas Shemdoe ambae ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, haw ani Wafanyabiashara wa Kampuni ya Tecno kutoka Jijini Dodoma ambao ni hawa wafuatao. Ndugu Rui Pu - Meneja Masoko, Ndugu Leila Msosa - Meneja Uhusiano, na Ndugu Abdul Salum – Meneja. Karibuni sana. *(Makofi)*

Pia wapo wageni Saba wa Mheshimiwa Daniel Godfrey Chongolo Waziri wa Kilimo, Wakurugenzi na Maafisa kutoka Wizara ya Kilimo, ambao ni Ndugu Gerald Mweli - Katibu Mkuu, Profesa Kenneth Bengesi - Mkurugenzi Mkuu Bodi ya Sukari, Ndugu Beatrice Banzi - Mkurugenzi Mkuu Bodi ya Chai, Ndugu Saddy Kambona - Mkurugenzi Mkuu Bodi ya Mkonge, na Ndugu Erick Maxmilian - Mwakilishi wa Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Uthibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wageni wengine 17 wa Mheshimiwa Chongolo Waziri wa Kilimo ni Wakurugenzi na Maafisa Waandamizi kutoka Wizara na Taasisi zake, karibuni sana mliopo Bungeni. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Steven Lemomo Kiruswa ambaye ni Naibu Waziri wa Madini ni Viongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Longido. Yupo Mheshimiwa Michael Laizer - Mbunge Mstaafu wa Jimbo la Longido na Mwenyekiti Mstaafu wa CCM Mkoa wa Arusha, karibu sana. Wageni wengine watano wa Mheshimiwa Dkt. Kiruswa ni Viongozi kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Longido Mkoani Arusha, wapo watano, karibuni sana. Ahsanteni sana karibuni hapa Bungeni. *(Makofi)*

Pia wapo wageni sita wa Mheshimiwa Switbert Zacharia Mkama ambaye ni Naibu Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, ambao ni familia yake kutoka Ukerewe Mkoani Mwanza. Tunaanza na Ndugu Matilda Masasi ambaye ni Mke wa Mheshimiwa Naibu Waziri, Ndugu Benjamin Mkama - mtoto wa Mheshimiwa Naibu Waziri, karibuni sana. *(Makofi)*

Vilevile, yupo Ndugu Tilumanywa Mazula - Kaka wa Mheshimiwa Naibu Waziri, Ndugu Edwini Jacob - mdogo wa Mheshimiwa Naibu Waziri, Ndugu Dorah Hillary - mdogo wa Mheshimiwa Naibu Waziri. *Father* Charles Ng'wanzalima - Padre wa Parokia ya Ihago, Jimbo Kuu la Katoliki Mwanza, karibu sana Kiongozi wetu wa dini. *(Makofi)*

Wageni wengine wa Mheshimiwa Mkama Naibu Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari ni Babu na Bibi wa Mheshimiwa. Karibuni sana Babu na Bibi, bado mnaonekana vijana. *(Makofi/Kicheko)*

Wageni wengine wa Waheshimiwa Wabunge ni Mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Ritta Enespher Kabati, rafiki yake kutoka Jijini Dar es Salaam Dkt. Manase Frank, karibu sana. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Tunao Ndugu Alexanda Chuwa, Afisa kutoka Ofisi za Umoja wa Mataifa *UNSACCO* ya Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wanafunzi 86 na Walimu nane wa Shule ya Sekondari Nghong'ona ya Jijini Dodoma, karibuni sana walimu pamoja na wanafunzi. *(Makofi)*

Wapo wanachama nane wa Umoja wa Wamiliki wa Mameneja wa Shule na Vyuo visivyo vya Serikali nchini, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo pia wanakwaya 44 wa Kwaya ya *Heavenly Echoes* kutoka Jijini Nairobi nchini Kenya, karibuni sana wageni wetu hapa Bungeni. *(Makofi)*

Tangazo kutoka Ofisi ya Katibu wa Bunge, Katibu wa Bunge anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kuwa, kikao cha *briefing* kitafanyika leo siku ya Alhamisi Tarehe 27 Agosti, 2026 Saa Saba Mchana mara baada ya kusitisha Shughuli za Bunge. Kikao hiki kitafanyika katika Ukumbi wa Msekwa, hivyo Waheshimiwa Wabunge wote mnaombwa kuhudhuria kikao hiki muhimu bila kukosa.

Tangazo lingine ni kutoka kwa Mwenyekiti wa Jumuiya ya Waadventista Wasabato hapa Bungeni ni kuhusu tangazo la ibada kwa Waheshimiwa Wabunge na Watumishi. Jumuiya ya Waadventista Wasabato Bungeni inayo heshima kuwaalika Waheshimiwa Wabunge na Watumishi wa Bunge kushiriki ibada itakayofanyika katika Ukumbi wa Ibada Bungeni *(Chapel)* uliopo katika Jengo la Pius Msekwa kuanzia Saa Nane Mchana.

Katika ibada hiyo Mchungaji Zawadi Yesaya na Mchungaji Thomas Bihene watahudumu kwa kutoa Neno la Mungu. Aidha, Kwaya ya *Heavenly Echoes* kutoka Jijini Nairobi nchini Kenya itatoa huduma ya uimbaji. Mwenyezi Mungu awabariki Waheshimiwa Wabunge na Watumishi wa Bunge wanaopanga kushiriki katika ibada hiyo. Ahsanteni sana.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea.

Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Kilimo wa Mwaka 2026 *[The Agricultural (Amendments) Bill, 2026]***

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**NAIBU SPIKA:** Sasa ninamwita Mheshimiwa Waziri wetu wa Kilimo, Mheshimiwa Daniel Chongolo kwa ajili ya kuwasilisha taarifa ya Wizara yake.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote ninaomba kabla ya kutoa hotuba kuhusu Muswada, nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Kilimo kwa Mwaka 2026 *(The Agricultural Laws (Amendments) Act, 2026)* unaopendekeza kufanya marekebisho katika sheria nne zilizoainishwa katika sehemu ya pili hadi sehemu ya tano ya Muswada.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya kipekee, nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuendelea kuongoza nchi yetu kwa uzalendo wa hali ya juu. Ninaomba niungane na Waheshimiwa Wabunge na wananchi wenzangu kuendelea kumwombea Mheshimiwa Rais wetu, kwa Mwenyezi Mungu amjalie kila la heri katika kuliongoza Taifa letu la Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naungana na Mheshimiwa Waziri Mkuu kumpongeza Mheshimiwa Deogratius John Ndejembi kwa kuaminiwa na kupendekezwa na CCM kushika dhamana ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, sisi wasaidizi wao tunamwahidi ushirikiano wetu wa dhati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, ninapenda kuwashukuru na kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kuwaletea maendeleo wananchi wote wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa mchoyo wa shukrani kama sitakushukuru na kukupongeza wewe binafsi pamoja na Mheshimiwa Spika kwa kuongoza na kusimamia vikao na mijadala ndani ya Bunge letu kwa umahiri na kwa kuzingatia sheria na kanuni zinazoliongoza Bunge hili. Ninawapongeza pia Waheshimiwa Wabunge kwa kuendelea kutekeleza ipasavyo wajibu wao wa Kikatiba wa kutunga sheria pamoja na kuisimamia Serikali, hakika mnaifanya kazi hii vema sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, ninaishukuru Ofisi ya Bunge ikiongozwa na Katibu wa Bunge, Ndugu Baraka Ildephonce Leonard na watumishi wote wa Bunge kwa ushirikiano mnaoipatia Wizara ya Kilimo katika kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawapongeza watumishi wote wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuendelea kutekeleza vyema majukumu na kazi za Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, wakiongozwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali mwenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, ninampongeza Mwandishi Mkuu wa Sheria pamoja na watumishi wote wa Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria kwa kufanikisha maandalizi ya Muswada huu kwa wakati na kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie shukrani zangu kwa kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo, inayoongozwa na Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika, Mbunge wa Njombe Mjini na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Mariam Ditopile Mzuzuri, Mbunge wa Jimbo la Kondoa Mjini kwa ushirikiano na ushauri waliotupatia wakati wa kupitia Muswada huu kwa Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati hii imefanya kazi kubwa na nzuri ya kuchambua Muswada huu kwa umakini, sambamba na maoni yaliyowasilishwa na wadau mbalimbali waliyoitwa mbele ya Kamati na kuishauri Serikali kuboresha Muswada huu. Ushauri uliotolewa na Kamati umezingatiwa na pia umeisaidia Serikali kuandaa jedwali la marekebisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Kilimo wa Mwaka 2026 *(The Agricultural Laws (Amendments) Act, 2026)* ambao unapendekeza marekebisho katika sheria nne ambazo ni:

(i) Sheria ya Usalama wa Chakula, Sura ya 249;

(ii) Sheria ya Tasnia ya Mkonge, Sura ya 30;

(iii) Sheria ya Tasnia ya Sukari, Sura ya 251; na

(iv) Sheria ya Tasnia ya Chai, Sura ya 275.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la marekebisho yanayopendekezwa katika sheria hizi ni kuondoa upungufu uliobainika katika utekelezaji wa baadhi ya masharti yaliyomo katika sheria hizo ili kuongeza ufanisi, usimamizi na utekelezaji wa sheria hizo kwa taasisi husika. Aidha, mapendekezo haya yanalenga kuwezesha sheria husika kuendana na mabadiliko mbalimbali ya kijamii, kisiasa na kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu umegawanyika katika sehemu tano ambapo sehemu ya kwanza inahusu masharti ya utangulizi ambayo yanajumuisha jina la Muswada na namna ambavyo masharti mbalimbali ya sheria yanayopendekezwa kurekebishwa katika sehemu zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Pili ya Muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Usalama wa Chakula, Sura ya 249, Sheria hii ilitungwa mwaka 1991 ili kusimamia uzalishaji,

uchakataji na uuzaji wa nafaka na mazao mchanganyiko, kuweka utaratibu wa Kitaifa wa uhakika wa usalama wa chakula na masuala mengine yanayohusiana na hayo. Tangu kutungwa kwake Sheria hii imefanywa marekebisho mara mbili, mwaka 2009 na mwaka 2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, marekebisho yanayopendekezwa yanalenga kuipa Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko, uwezo wa kutekeleza majukumu yaliyokuwa yakitekelezwa na Bodi ya Pareto Tanzania na kushughulikia majukumu hayo katika tasnia hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 2 kinapendekezwa kurekebisha na kuboresha fasili ya misamiati *other produce* na *food commodities* ili kuongeza fasili ya misamiati ambayo imetumika katika sheria lakini haikuwa imetafsiriwa. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuongeza ufafanuzi wa misamiati hiyo kama inavyotumika katika sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 4 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuwezesha Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko kutekeleza majukumu yaliyokuwa yanatekelezwa na Bodi ya Pareto Tanzania na kuipa Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko nguvu ya kisheria ya udhibiti wa bidhaa zinazotokana na nafaka na mazao mchanganyiko kuingia kutoka nchini bila kuathiri sheria za ubora na viwango vya bidhaa nchini. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuongeza ufanisi katika usimamizi wa tasnia ya Pareto.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 6 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuipa Bodi ya Wakurugenzi mamlaka ya kutwaa miongozo kwa ajili ya utekelezaji wa masharti ya sheria. Kifungu hiki kinapendekezwa kurekebishwa zaidi kwa kuipa bodi mamlaka ya kushughulikia na kutatua migogoro kati ya wakulima na wafanyabiashara wengine wa mazao ya nafaka kwa madhumuni ya kukuza na kuhimiza utatuzi wa migogoro kwa njia ya maridhiano. Mapendekezo hayo ya marekebisho yanakusudia

kurahisisha uzingatiwaji wa masharti ya sheria na kuongeza ufanisi wa sekta hii na hivyo kuchangia katika ukuaji wa uchumi nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, vifungu vya 11 na 12 vinapendekezwa kurekebishwa kwa madhumuni ya kuboresha mamlaka ya Mkurugenzi Mkuu, kama Afisa Mtendaji Mkuu wa Mamlaka, pamoja na hadhi na wajibu kwa watu waliowajiriwa kama watumishi wa mamlaka. Masharti ya vifungu kwa sasa yanabainisha kwamba watumishi wa mamlaka watatekeleza majukumu ya bodi na siyo ya mamlaka. Hivyo mapendekezo ya marekebisho yanaweka usahihi wa utekelezaji wa majukumu ya mamlaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 19 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuainisha haki ya kukata rufaa dhidi ya uamuzi wa mamlaka wa kukataa kutoa leseni. Kwa sasa hakuna utaratibu wa rufaa dhidi ya uamuzi wa mamlaka wa kukataa kutoa leseni. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuimarisha utaratibu wa utoaji wa haki kwa watu ambao hawajaridhika na uamuzi wa mamlaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 31 kinapendekezwa kurekebishwa ili kutambua taasisi stahiki ya uamuzi wa viwango vya malipo ya wajumbe wa bodi. Kwa sasa Waziri mwenye dhamana na masuala ya kilimo ndiye mwenye mamlaka ya kuamua viwango vya malipo ya posho za wajumbe wa bodi. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kumwezesha Msajili wa Hazina, ambaye ni mamlaka stahiki kubainisha viwango vya malipo ya posho za wajumbe wa bodi. Vilevile, marekebisho yanalenga kuimarisha uhuru wa bodi katika kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu Kipya cha 32(a), kinapendekezwa kuongezwa ili kumpa Waziri mwenye dhamana na masuala ya kilimo mamlaka ya kuongeza mazao mchanganyiko. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuweka mazingira wezeshi ya kisheria kwa ajili ya kuongeza wigo wa mazao yanayodhibitiwa chini ya sheria pale panapokuwa na uhitaji wa kufanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 33(a) kinapendekezwa kuongezwa ili kuwezesha kufanyika kwa vikao vya wadau na kuwezesha usimamizi wa majukumu ya pamoja na upatikanaji wa fedha za kugharamia majukumu ya pamoja. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuwezesha maendeleo ya nafaka na mazao mchanganyiko.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 39(a) kinapendekezwa kuongezwa ili kuweka masharti ya ufifilishaji wa makosa yaliyoainishwa katika sheria. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kurahisisha na kuharakisha mchakato wa uchukuaji wa hatua za kisheria kwa makosa mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Tatu ya Muswada inapendekezwa Marekebisho ya Sheria ya Tasnia ya Mkonge Sura ya 30. Sheria hii ilitungwa mwaka 1997, tangu kutungwa kwake sheria hii imerekebishwa mara mbili mwaka 2004 na mwaka 2009. Kifungu cha Pili cha sheria kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza fasili ya msamiati '*shared function*', lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuongeza ufafanuzi wa neno hilo kama linavyotumika katika sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vifungu vya 5 na 22 vinapendekezwa kurekebishwa kwa lengo la kumpa Waziri mamlaka ya kutengeneza kanuni zinazohusu uchakataji, usafirishaji nje ya nchi na uhifadhi wa mkonge badala ya bodi. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuimarisha utekelezaji bora wa masharti ya sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu Kipya cha 24(a) kinapendekezwa kuongezwa ili kutoa masharti ya ufifilishaji wa makosa yaliyoainishwa kwenye sheria. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kurahisisha na kuharakisha mchakato wa uchukuaji wa hatua za kisheria kwa makosa mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Nne ya Muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Tasnia ya Sukari Sura ya 251. Sheria hii ilitungwa mwaka 2001 kwa madhumuni ya kuanzisha

Bodi ya Sukari Tanzania na Chuo cha Taifa cha Sukari, kuweka masharti ya kuboresha, kuendeleza na kudhibiti sekta ya sukari pamoja na mambo yanayohusiana na hayo. Tangu kutungwa kwa sheria hii, imefanyiwa marekebisho mara nne mwaka 2009, 2017, 2020 na 2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 2 kinachopendekezwa kinalenga kurekebishwa kwa kuboresha fasili ya msamiati *sugar by-product, raw sugar, refined sugar* na *special sugar* ili kuongeza fasili mpya za misamiati inayotumika katika sheria. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kufafanua maana ya misamiati hiyo kama ilivyotumika katika sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 15 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuweka sharti la usajili wa viwanda au mitambo ya sukari kwa kuzingatia matumizi au madhumuni ya bidhaa ya sukari inayozalishwa. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuongeza wigo wa bidhaa za sukari zinazodhibitiwa ili kuboresha ubora wa bidhaa hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 18 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kujumuisha sukari ilyosafishwa na sukari ghafi zinazoweza kuingizwa nchini na mtu ambaye tayari ana kiwanda cha kuchakata sukari ghafi, kinachofanya kazi kwa lengo la kuzalisha sukari ya matumizi ya viwandani. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuongeza udhibiti na kukuza uwekezaji katika tasnia ya sukari.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 21 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kutenganisha mkataba wa utekelezaji wa leseni ya uingizaji wa sukari nchini. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuendeleza sharti la mkataba wa utekelezaji kama nyenzo muhimu katika udhibiti wa wazalishaji wa sukari na masharti ya uagizaji wa sukari ghafi kwa maana *ya raw sugar* kwa ajili ya uzalishaji wa sukari ya matumizi ya viwandani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 42 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza wigo wa watu wanaokusudia kufungasha upya sukari inayozalishwa ndani ya nchi katika

kiwango kisichozidi ujazo wa gramu 100. Marekebisho haya yataruhusu watu ambao sio wazalishaji wa sukari waliosajiliwa na bodi kufanya ufungashaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuimarisha udhibiti wa shughuli za ufungashaji upya wa sukari ili kulinda ubora wa viwango vya sukari. Jedwali la kwanza linapendekezwa kurekebishwa kwa kumtambua Mkurugenzi Mkuu kama Katibu wa Bodi. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuboresha uratibu wa shughuli za bodi ili kuongeza ufanisi wa utendaji wa bodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jedwali la pili linapendekeza kurekebishwa kwa kuboresha muundo wa Baraza la Uongozi la Chuo cha Taifa cha Sukari. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuhakikisha kunakuwepo na uwakilishi wa Wizara na wadau muhimu katika baraza hilo. Aidha, jedwali hilo linapendekezwa kurekebishwa kwa kumtambua Mkuu wa Chuo kama Katibu wa Baraza.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kubainisha jina sahihi la Mkuu wa Chuo kulingana na matakwa ya *NACTVET* pamoja na kuboresha uratibu wa shughuli za baraza ili kuongeza ufanisi wa utendaji wa baraza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Tano ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Tasnia ya Chai Sura ya 275. Sheria hii ilitungwa mwaka 1997 kwa lengo la kuanzisha Bodi ya Chai Tanzania na Wakala wa Maendeleo ya Wakulima Wadogo wa Chai Tanzania pamoja na kukuza na kudhibiti kilimo na uuzaji wa chai nje ya nchi. Tangu kutungwa kwake sheria hii imefanyiwa marekebisho mara nne; mwaka 1998, 2001, 2004 na 2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada unapendekeza kurekebisha jina refu, vifungu vya pili, tatu, nne, tano na 31 pamoja na jedwali la kwanza na la pili kwa kuifuta Wakala wa Maendeleo ya Wakulima Wadogo wa Chai Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha Tano kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuipa bodi majukumu ambayo awali yalikuwa yakitekelezwa na Wakala wa Maendeleo ya Wakulima Wadogo wa Chai Tanzania ambayo yatasimamiwa na idara mahususi. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuongeza ufanisi wa bodi na kupunguza gharama za uendeshaji wa shughuli za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 32(a) kinapendekezwa kuongezwa ili kuweka masharti ya mwendelezo na mpito kuhusiana na wafanyakazi, mali, masilahi, haki, stahiki, madeni au wajibu wa Wakala wa Maendeleo ya Wakulima Wadogo wa Chai Tanzania kufuatia kufutwa kwake. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kulinda masilahi ya wafanyakazi na kuhakikisha usimamizi bora na uendelevu wa tasnia ya chai ikiwemo wakulima wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jedwali la kwanza linapendekezwa kurekebishwa kwa kujumuisha uwakilishi wa wadau muhimu katika bodi. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuongeza ufanisi wa bodi katika kutekeleza majukumu yake. Jedwali la pili linapendekezwa kufutwa ili kuendana na pendekezo la kuifuta Wakala wa Maendeleo ya Wakulima Wadogo wa Chai nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya kwa mujibu wa Kanuni ya 102 ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la mwaka 2025 ninaomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Kilimo ya Mwaka 2026 (*The Agricultural Law Amendments Act 2026*) ujadiliwe na kupitishwa katika hatua ya Kusomwa kwa Mara ya Pili na ya Tatu na hatimaye marekebisho yanayopendekezwa yawe sehemu ya sheria za nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

## HOTUBA YA MHE. DANIEL GODFREY CHONGOLO (MB), WAZIRI WA KILIMO AKIWASILISHA MUSWADA WA SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA ZA KILIMO WA MWAKA 2026 (THE AGRICULTURAL LAWS (AMENDMENTS) ACT, 2026) KATIKA BUNGE LA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA ALHAMIS 27 AGOSTI, 2026 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

**Mheshimiwa Spika,** awali ya yote, naomba kabla ya kutoa hotuba kuhusu Muswada nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako tukufu kuwasilisha Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Kilimo wa mwaka 2026 (The Agricultural Laws (Amendments) Act, 2026) unaopendekeza kufanya marekebisho katika Sheria Nne (4) zilizoainishwa katika Sehemu ya Pili hadi Sehemu ya Tano ya Muswada.

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee nitumie nafasi hii kumpongeza Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuiongoza Nchi yetu kwa uzalendo wa hali ya juu. Naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge na wananchi wenzangu kuendelea kumuombea Rais wetu kwa Mwenyezi Mungu amjaalie kila la kheri katika kuliongoza Taifa letu la Tanzania.

**Mheshimiwa Spika,** aidha, napenda kuwashukuru na kuwapongeza Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Mhe.Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kuwaletea maendeleo wananchi wote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**Mheshimiwa Spika,** nitakuwa mchoyo wa shukrani kama nisipokushukuru na kukupongeza wewe binafsi pamoja na

Mheshimiwa Naibu Spika kwa kuongoza na kusimamia vikao na mijadala ndani ya Bunge letu kwa umahiri na kwa kuzingatia Sheria na Kanuni zinazoliongoza Bunge hili. Ninawapongeza pia Waheshimiwa Wabunge kwa kuendelea kutekeleza ipasavyo wajibu wao wa kikatiba wa kutunga sheria pamoja na kuisimamia Serikali.
Aidha, Ninaishukuru Ofisi ya Bunge ikiongozwa na Katibu wa Bunge Bw. Baraka Ildiphonce Leonard na watumishi wote wa Bunge kwa ushirikiano mnaoipatia Wizara ya Kilimo katika kutekeleza majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika,** ninawapongeza watumishi wote wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuendelea kutekeleza vyema majukumu na kazi za Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Vilevile, ninampongeza Mwandishi Mkuu wa Sheria pamoja na watumishi wote wa Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria kwa kufanikisha maandalizi ya Muswada huu kwa wakati na kwa ufanisi.

**Mheshimiwa Spika,** nimalizie shukrani zangu kwa kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo inayoongozwa na Mhe. Deodatus Philip Mwanyika (Mbunge wa Njombe Mjini) na Makamu Mwenyekiti Mhe. Mariamu Ditopile Mzuzuri (Mbunge wa Kondoa Mjini) kwa ushirikiano na ushauri waliotupatia wakati wa kupitia Muswada huu katika Kamati. Kamati hii ilifanya kazi kubwa na nzuri ya kuchambua Muswada huu kwa umakini sambamba na maoni yaliyowasilishwa na wadau mbalimbali walioitwa mbele ya Kamati na kuishauri Serikali kuboresha Muswada huu. Ushauri uliotolewa na kamati umezingatiwa na pia umesaidia Serikali katika kuandaa Jedwali la Marekebisho.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako tukufu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Kilimo wa mwaka 2026 (The Agricultural Laws (Amendments) Act, 2026) ambao unapendekeza marekebisho katika Sheria Nne ambazo ni, Sheria ya Usalama wa Chakula, Sura ya 249, Sheria ya Tasnia ya Mkonge, Sura ya 30, Sheria ya Tasnia ya Sukari, Sura ya 251 na Sheria ya Tasnia ya Chai, Sura ya 275.

**Mheshimiwa Spika,** lengo la marekebisho yanayopendekezwa katika Sheria hizi ni kuondoa upungufu uliobainika katika utekelezaji wa baadhi ya masharti yaliyomo katika Sheria hizo ili kuongeza ufanisi, usimamizi na utekelezaji wa Sheria hizo kwa taasisi husika. Aidha, mapendekezo haya yanalenga kuwezesha Sheria husika kuendana na mabadiliko mbalimbali ya kijamii, kisiasa na kiuchumi.

**Mheshimiwa Spika,** Muswada huu umegawanyika katika Sehemu Tano ambapo Sehemu ya Kwanza inahusu Masharti ya Utangulizi ambayo yanajumuisha jina la Muswada na namna ambavyo masharti mbalimbali ya Sheria yanapendekezwa kurekebishwa katika Sehemu zake.

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya Pili ya Muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Usalama wa Chakula, Sura ya 249. Sheria hii ilitungwa mwaka 1991 ili kusimamia uzalishaji, uchakataji na uuzaji wa nafaka na mazao mchanganyiko, kuweka utaratibu wa kitaifa wa uhakika wa usalama wa chakula na masuala mengine yanayohusiana na hayo. Tangu kutungwa kwake, Sheria hii imefanyiwa marekebisho mara mbili mwaka 2009 na mwaka 2023.

**Mheshimiwa Spika,** marekebisho yanayopendekezwa yanalenga kuipa Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko uwezo wa kutekeleza majukumu yaliyokuwa yanatekelezwa na Bodi ya Pareto Tanzania na kushughulikia masuala yanayohusiana na hayo katika tasnia hiyo.

Kifungu cha 2 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuboresha fasili ya misamiati "other produce" na "food commodities" ili kuongeza fasili ya misamiati ambayo imetumika katika Sheria lakini haikuwa imetafsiriwa. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuongeza ufafanuzi wa misamiati hiyo kama inavyotumika katika Sheria.

Kifungu cha 4 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuwezesha Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko kutekeleza majukumu yaliyokuwa yanatekelezwa na Bodi ya

Pareto Tanzania na kuipa Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko nguvu ya kisheria ya udhibiti wa bidhaa zinazotokana na nafaka na mazao mchanganyiko kuingia na kutoka nchini bila kuathiri sheria za ubora na viwango wa bidhaa nchini. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuongeza ufanisi katika usimamizi wa tasnia ya pareto.

Kifungu cha 6 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuipa Bodi ya Wakurugenzi mamlaka ya kutoa miongozo kwa ajili ya utekelezaji wa masharti ya Sheria. Kifungu hiki kinapendekezwa kurekebishwa zaidi kwa kuipa Bodi mamlaka ya kushughulikia na kutatua migogoro kati ya wakulima na wafanyabiashara wengine wa nafaka na mazao mchanganyiko kwa madhumuni ya kukuza na kuhimiza utatuzi wa migogoro kwa njia ya maridhiano. Mapendekezo haya ya marekebisho yanakusudia kurahisisha uzingatiaji wa masharti ya Sheria na kuongeza ufanisi wa sekta na hivyo kuchangia katika ukuaji wa uchumi wa nchi.

**Mheshimiwa Spika,** vifungu vya 11 na 12 vinapendekezwa kurekebishwa kwa madhumuni ya kuboresha mamlaka ya Mkurugenzi Mkuu kama Afisa Mtendaji Mkuu wa Mamlaka, pamoja na hadhi na wajibu wa watu walioajiriwa kama watumishi wa Mamlaka. Masharti ya vifungu kwa sasa yanabainisha kwamba watumishi wa mamlaka watatekeleza majukumu ya Bodi na siyo ya Mamlaka. Hivyo, mapendekezo ya marekebisho yanaweka usahihi wa utekelezaji wa majukumu ya Mamlaka.

Kifungu cha 19 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuainisha haki ya kukata rufaa dhidi ya uamuzi wa Mamlaka wa kukataa kutoa leseni. Kwa sasa, hakuna utaratibu wa rufaa dhidi ya uamuzi wa mamlaka wa kukataa kutoa leseni. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuimarisha utaratibu wa utoaji haki kwa watu ambao hawajaridhika na uamuzi wa Mamlaka.

Kifungu cha 31 kinapendekezwa kurekebishwa ili kutambua taasisi stahiki ya uamuzi wa viwango vya malipo ya wajumbe wa Bodi. Kwa sasa Waziri mwenye dhamana na masuala ya kilimo ndiye mwenye mamlaka ya kuamua viwango vya malipo ya posho za wajumbe wa Bodi. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni

kumwezesha Msajili wa Hazina ambaye ni mamlaka stahiki kubainisha viwango vya malipo ya posho za wajumbe wa Bodi. Vilevile, marekebisho yanalenga kuimarisha uhuru wa Bodi katika utekelezaji wa majukumu yake.
Kifungu kipya cha 32A kinapendekezwa kuongezwa ili kumpa Waziri mwenye dhamana na masuala ya kilimo mamlaka ya kuongeza mazao mchangayiko. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuweka mazingira wezeshi ya kisheria kwa ajili ya kuongeza wigo wa mazao yanayodhibitiwa chini ya Sheria pale kunapokuwa na uhitaji wa kufanya hivyo.

Kifungu cha 33A kinapendekezwa kuongezwa ili kuwezesha kufanyika kwa vikao vya wadau na kuwezesha usimamizi wa majukumu ya pamoja na upatikanaji wa fedha za kugharamia majukumu ya pamoja. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuwezesha maendeleo ya nafaka na mazao mchanganyiko.

Kifungu cha 39A kinapendekezwa kuongezwa ili kuweka masharti ya ufifilishaji wa makosa yaliyoainishwa katika Sheria. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kurahisisha na kuharakisha mchakato wa uchukuaji wa hatua za kisheria kwa makosa mbalimbali.

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya Tatu ya Muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Tasnia ya Mkonge, Sura ya 30. Sheria hii ilitungwa mwaka 1997. Tangu kutungwa kwake Sheria hii imerekebishwa mara mbili, mwaka 2004 na mwaka 2009.

Kifungu cha 2 cha Sheria kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza fasili ya msamiati “shared function”. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuongeza ufafanuzi wa neno hilo kama linavyotumika katika Sheria.

Vifungu vya 5 na 22 vinapendekezwa kurekebishwa kwa lengo la kumpa Waziri mamlaka ya kutengeneza kanuni zinazohusu uchakataji, usafirishaji nje ya nchi na uhifadhi wa mkonge badala ya Bodi. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuimarisha utekelezaji bora wa masharti ya Sheria.

Kifungu kipya cha 24A kinapendekezwa kuongezwa ili kutoa masharti ya ufifilishaji wa makosa yaliyoainishwa chini ya Sheria. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kurahisisha na kuharakisha mchakato wa uchukuaji wa hatua za kisheria kwa makosa mbalimbali.

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya Nne ya Muswada inapendekeza kurekebisha Sheria ya Tasnia ya Sukari, Sura ya 251. Sheria hii ilitungwa mwaka 2001 kwa madhumuni ya kuanzisha Bodi ya Sukari Tanzania na Chuo cha Taifa cha Sukari, kuweka masharti ya kuboresha, kuendeleza na kudhibiti sekta ya sukari pamoja na mambo yanayohusiana na hayo. Tangu kutungwa kwake Sheria hii imefanyiwa marekebisho mara nne, mwaka 2009, 2017, 2020 na 2024.

Kifungu cha 2 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuboresha fasili ya msamiati "sugar by-product", "raw sugar", "refined sugar" na "special sugar" ili kuongeza fasili mpya za misamiati inayotumika katika Sheria. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kufafanua maana ya misamiati hiyo kama ilivyotumika katika Sheria.

Kifungu cha 15 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuweka sharti la usajili wa viwanda au mitambo ya sukari kwa kuzingatia matumizi au madhumuni ya bidhaa ya sukari inayozalishwa. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuongeza wigo wa bidhaa za sukari zinazodhibitiwa ili kuboresha ubora wa bidhaa hizo.

Kifungu cha 18 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kujumuisha sukari iliyosafishwa na sukari ghafi zinazoweza kuingizwa nchini na mtu ambaye tayari ana kiwanda cha kuchakata sukari ghafi kinachofanya kazi kwa lengo la kuzalisha sukari ya matumizi ya viwandani. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuongeza udhibiti na kukuza uwekezaji katika tasnia ya sukari.

Kifungu cha 21 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kutenganisha mkataba wa utekelezaji na leseni ya uingizaji wa sukari nchini.

Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuendeleza sharti la mkataba wa utekelezaji kama nyenzo muhimu katika udhibiti wa wazalishaji wa sukari na masharti ya uagizaji wa sukari ghafi (raw sugar) kwa ajili ya uzalishaji wa sukari ya matumizi ya viwandani. Kifungu cha 42 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuongeza wigo wa watu wanaokusudia kufungasha upya sukari inayozalishwa ndani ya nchi katika kiwango kisichozidi ujazo wa gramu 100. Marekebisho haya yataruhusu watu ambao si wazalishaji wa sukari walio sajiliwa na Bodi kufanya ufungashaji. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuimarisha udhibiti wa shughuli za ufungashaji upya wa sukari ili kulinda ubora na viwango vya sukari.

Jedwali la Kwanza linapendekezwa kurekebishwa kwa kumtambua Mkurugenzi Mkuu kama Katibu wa Bodi. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuboresha uratibu wa shughuli za Bodi ili kuongeza ufanisi wa utendaji wa Bodi.

Jedwali la Pili linapendekezwa kurekebishwa kwa kuboresha muundo wa Baraza la Uongozi la Chuo cha Taifa cha Sukari. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuhakikisha kunakuwepo na uwakilishi wa Wizara na wadau muhimu katika Baraza hilo. Aidha, Jedwali hilo linapendekezwa kurekebishwa kwa kumtambua Mkuu wa Chuo kama Katibu wa Baraza. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kubainisha na jina sahihi la Mkuu wa Chuo kulingana na matakwa ya NACTVET pamoja na kuboresha uratibu wa shughuli za Baraza ili kuongeza ufanisi wa utendaji wa Baraza.

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya Tano ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Tasnia ya Chai, Sura ya 275. Sheria hii ilitungwa mwaka 1997 kwa lengo la kuanzisha Bodi ya Chai Tanzania na Wakala wa Maendeleo ya Wakulima Wadogo wa Chai Tanzania, pamoja na kukuza na kudhibiti kilimo na uuzaji wa chai nje ya nchi. Tangu kutungwa kwake, Sheria hii imefanyiwa marekebisho mara nne mwaka 1998, 2001, 2004 na 2009.

**Mheshimiwa Spika,** Muswada unapendekeza kurekebisha jina refu, vifungu vya 2, 3 4 5 na 31 pamoja na Jedwali la Kwanza na la Pili kwa kuifuta Wakala wa Maendeleo ya Wakulima Wadogo wa Chai Tanzania.

**Mheshimiwa Spika,** Kifungu cha 5 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuipa Bodi majukumu ambayo awali yalikuwa yakitekelezwa na Wakala wa Maendeleo ya Wakulima Wadogo wa Chai Tanzania ambayo yatasimamiwa na Idara mahsusi. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuongeza ufanisi wa Bodi na kupunguza gharama za uendeshaji wa shughuli za Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Kifungu cha 32A kinapendekezwa kuongezwa ili kuweka masharti ya mwendelezo na mpito kuhusiana na wafanyakazi, mali, maslahi, haki, stahili, madeni au wajibu wa Wakala wa Maendeleo ya Wakulima Wadogo wa Chai Tanzania kufuatia kufutwa kwake. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kulinda maslahi ya wafanyakazi na kuhakikisha usimamizi bora na endelevu wa tasnia ya chai.

**Mheshimiwa Spika,** Jedwali la Kwanza linapendekezwa kurekebishwa kwa kujumuisha uwakilishi wa wadau muhimu katika Bodi. Lengo la marekebisho yanayopendekezwa ni kuongeza ufanisi wa Bodi katika kutekeleza majukumu yake. Jedwali la Pili linapendekezwa kufutwa ili kuendana na pendekezo la kuifuta Wakala wa Maendeleo ya Wakulima wa Wadogo wa Chai Tanzania.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo haya, kwa mujibu wa Kanuni ya 102 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2025, ninaomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Kilimo wa mwaka 2026 (The Agricultural Laws (Amendments) Act, 2026) ujadiliwe na kupitishwa katika hatua ya kusomwa kwa mara ya Pili na ya Tatu na hatimaye marekebisho yanayopendekezwa yawe sehemu ya Sheria za Nchi.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo NAOMBA KUTOA HOJA.

Daniel G. Chongolo *(Mb.)*
**WAZIRI WA KILIMO**
27 Agosti, 2026

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Hoja imeungwa mkono. Ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo, Mheshimiwa Deodatus Mwanyika. *(Makofi)*

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA, KILIMO NA MIFUGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Kilimo wa Mwaka 2026 *(The Agricultural Amendments Bill 2026)*. Kwa mujibu wa Kanuni ya 102(v) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada wa Sheria ya Kilimo kuhusu Marekebisho ya Sheria za Kilimo wa Mwaka 2026 ulisomwa Bungeni kwa mara ya kwanza katika Mkutano wa Tatu, Kikao cha Hamsini na Nane kwenye Bunge la Kumi na Tatu, tarehe 26 Juni, 2026 kwa mujibu wa Kanuni ya 99(i) ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya100(i) ikisomwa pamoja na Kanuni ya 139(xiv) na Kifungu cha 7(1)(b) cha nyongeza ya nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge ulielekeza Muswada huu kwenye Kamati ya kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo ili ufanyiwe uchambuzi na kujadiliwa

kwa kina. Ninaomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba Kamati imeuchambua na kuujadili Muswada huu kwa kuzingatia Katiba, Sheria mbalimbali pamoja na Kanuni za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu namna uchambuzi wa Muswada ulivyofanyika. Hatua za kufanya Muswada huu zilianza kwa maandalizi mbalimbali ya kiutendaji yaliyofanywa na sekretarieti kwa ajili ya kuwezesha utekelezaji bora wa shughuli za Kamati. Maelezo ya uchambuzi wa Muswada ulifanywa na kuwasilishwa kwenye Kamati ya Sekretarieti ya Bunge kwa mujibu wa Kanuni ya 25(2)(b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Hatua hii ilijenga msingi wa utekelezaji wa kazi za Kamati kuhusiana na Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilikutana na Serikali tarehe 11 Agosti, 2026 ili kupokea maelezo ya Mheshimiwa Daniel Godfrey Chongolo, Mbunge, na Waziri wa Kilimo, kuhusu madhumuni na sababu za Muswada huu. Baada ya Kamati kupatiwa maelezo ya Serikali, Wajumbe walipata fursa ya kuuliza maswali na kupata maelezo ya ufafanuzi katika ibara mbalimbali za Muswada.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia kanuni ya 100(ii) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilifanya mkutano wa kusikiliza maoni ya wadau (*public hearing*) tarehe tarehe 12 na 13 Agosti, 2026 ili kupokea maoni yao kuhusu Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kushukuru wadau wote waliotoa maoni yao mbele ya Kamati hii kuuboresha Muswada huu. Ninaomba kuwatambua kwa majina kama ifuatavyo: Chama cha Wazalishaji wa Sukari Tanzania *(TSPA)*; Chama cha Kilele cha Ushirika wa Wakulima Wadogo wa Chai Tanzania; Chama cha Wakulima Wadogo wa Chai Njombe (NJOTIKOJE); na vilevile tulikuwa na mtaalamu mwelekezi wa masuala ya chai Ndugu Philbert Kavia.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hatua hiyo, Wajumbe wa Kamati walipata fursa tena ya kujadili maudhui ya Muswada kwa kuzingatia hoja zilizotokana na maelezo ya uchambuzi,

maoni pamoja na nyaraka mbalimbali kuhusiana na Muswada huu. Mnamo tarehe 18 Agosti, 2026 Kamati ilikutana tena na Waziri wa Kilimo ili kujadili kuhusu hoja zilizobainika kwa kila ibara ya Muswada na kumshauri Waziri kufanya marekebisho katika ibara zilizoonekana kuhitaji marekebisho kwa mujibu wa Kanuni ya 100(iii) ya kanuni za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hatua hiyo, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 100(i) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilitaarifu Ofisi ya Spika kwamba imekamilisha uchambuzi wa Muswada ili ujadiliwe Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa Muswada. Kamati ilichambua Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Kilimo wa Mwaka 2026 ukiwa umegawanyika katika sehemu tano na unapendekeza kufanya marekebisho katika sheria nne kwa madhumuni ya kuondoa upungufu au dosari au kutatua changamoto ambazo zimejitokeza katika utekelezaji wa sheria hizo kama zilivyoelekezwa na Mtoa Hoja mbele ya Kamati. Sheria zilizopendekezwa kufanyiwa marekebisho ni zifuatazo:-

i. Sheria ya Usalama wa Chakula Sura ya 249;
ii. Sheria ya Tasnia ya Mkonge Sura ya 30;
iii. Sheria ya Tasnia ya Sukari Sura ya 251; na
iv. Sheria ya Tasnia ya Chai Sura 275.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya kwanza ya Muswada inayohusu masharti ya utangulizi inajumuisha ibara ya kwanza inayohusu jina la sheria na inayokusudiwa kutungwa na ibara ya pili. Ibara ya pili inaweka masharti ya namna ambavyo Sheria mbalimbali zinapendekezwa kurekebishwa katika sehemu zake. Sheria zinafanyiwa marekebisho na maudhui yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imefanya uchambuzi wa maudhui ya marekebisho ya Muswada kwa kuzingatia changamoto ambazo Mtoa Hoja alieleza Kamati kuwa Muswada huu umelenga kuzitatua pamoja na masuala mengine ambayo Kamati iliona yanafaa kuzingatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya pili ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Usalama wa Chakula, Sura 249. Sehemu hii inahusu ibara ya tatu hadi ya 13 ya Muswada. Marekebisho haya yanagusa mambo mbalimbali. Miongoni mwa mambo hayo ni matumizi ya misamiati mahususi katika sheria hii kuipa bodi mamlaka ya kushughulikia na kutatua migogoro kati ya wakulima na wafanyabiashara wa nafaka na mazao mchanganyiko kwa njia ya maridhiano badala ya kuamua kwa usuluhishi; kuondoa mamlaka ya Waziri katika kuamua viwango vya malipo ya Wajumbe wa Bodi na kuhamishia kwenye mamlaka husika; pia, kuboresha mamlaka ya Mkurugenzi Mkuu kama Afisa Mtendaji Mkuu wa Mamlaka pamoja na hadhi na wajibu wa watu walioajiriwa na mamlaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo mengine yaliyojitokeza katika mapendekezo ni marekebisho yanayolenga kujumuisha zao la pareto miongoni mwa mazao mchanganyiko yatakayosimamiwa na *COPRA* na kuiwezesha mamlaka hiyo kutekeleza majukumu yaliyokuwa yanatekelezwa na Bodi ya Pareto.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, mapendekezo hayo yanaainisha haki ya kukata rufaa dhidi ya uamuzi wa mamlaka kwa kukataa kutoa leseni. Rufaa hiyo itakatwa kwa maandishi kwenda kwa Waziri. Lengo la marekebisho haya ni kuimarisha utoaji haki kwa mtu ambaye hajaridhika na uamuzi wa mamlaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni kumpa mamlaka Waziri mwenye dhamana ya masuala ya kilimo kutangaza kwa notisi kwenye Gazeti la Serikali zao lolote la kilimo kuwa kati ya mazao mchanganyiko. Halikadhalika, marekebisho hayo yanaweka utaratibu wa ufifilishaji wa makosa (*compounding of offenses*) ambapo inampa Mkurugenzi Mkuu au aliyeidhinishwa wakati wowote kabla ya kesi kuanza mahakamani kufifilisha kosa na kuamuru mkosaji kulipa kiasi cha fedha kisichozidi nusu ya faini ambayo angelazimika kulipa iwapo angepatikana na hatia na ikiwa atashindwa kulipa fedha iliyoamuliwa kulipwa atatozwa riba kwa kiwango kilichobainishwa kwenye kanuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, inaweka masharti kuwa mtu aliyeshtakiwa kulipa kiwango kilichofifilishwa hatashitakiwa mahakamani kwa kosa ambalo limefifilishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Tatu ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho ya Sheria ya Tasnia ya Mkonge, Sura 30. Sehemu hii inahusu Ibara ya 14 hadi 18 ya Muswada.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika sheria hii yapo mambo mbalimbali yanayolengwa kubadilika kwa marekebisho ya Sheria inayopendekezwa. Mambo hayo ni pamoja na kuhamisha mamlaka kutoka bodi ya mkonge kwenda kwa Waziri. Mapendekezo haya yanampa Waziri mamlaka ya kutunga kanuni zinazohusu uchakataji, usafirishaji nje na uhifadhi wa mkonge.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo mengine ni kuweka utaratibu wa ufifilishaji wa makosa yaliyoainishwa chini ya sheria hii. Lengo la marekebisho haya ni kuanzisha utaratibu wa makosa madogo ya kisheria kwa njia ya kiutawala badala ya kuyapeleka yote mahakamani ili kuongeza ufanisi wa sheria, kuboresha utekelezaji wa sheria katika tasnia ya mkonge.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya nne ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho ya Sheria ya Tasnia ya Sukari, Sura 251. Sehemu hii inahusu Ibara ya 19 hadi 26 ya Muswada. Marekebisho yaliyopendekezwa yanaleta masharti mapya ya usajili wa viwanda au mitambo ya kutengeneza sukari ambapo inaeleza kuwa bodi itatoa usajili kwa watu wanaokusudia kuanzisha viwanda au mitambo ya kuzalisha sukari za nyumbani, sukari ya viwandani, sukari maalum pamoja na bidhaa zinazotokana na miwa au bidhaa zinazotokana na uzalishaji wa sukari.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni kuipa bodi mamlaka ya kutoa leseni za uagizaji wa sukari kwa matumizi ya nyumbani, viwandani na sukari ghafi. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza uthibiti na kukuza uwekezaji katika tasnia ya sukari.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, mapendekezo ya marekebisho yanalenga kuipa Bodi ya Sukari mamlaka ya kuingia mkataba wa utekelezaji na mzalishaji wa sukari kwa lengo la kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa mipango ya maendeleo au upanuzi wa uwezo wa uzalishaji wa sukari.

Mheshimiwa Naibu Spika, marekebisho yanalenga kuongeza wigo wa watu wanaokusudia kufungasha upya sukari inayozalishwa ndani ya nchi kwa ukubwa usiozidi gramu 100 ili kuwajumuisha watu ambao sio wazalishaji waliosajiliwa na bodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya tano ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho ya Sheria ya tasnia ya chai sura 275. Sehemu hii inahusu Ibara ya 27 hadi 35 ya Muswada. Mapendekezo ya marekebisho ya sheria hii yanalenga kuifuta Wakala wa Maendeleo ya Wakulima wa Chai Tanzania na kuipa Bodi ya Chai Tanzania majukumu ya awali yaliyokuwa yakitekelezwa na Wakala wa Maendeleo ya Wakulima wa Chai Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, mapendekezo yanaweka masharti ya mwendelezo wa mpito kuhusiana na wafanyakazi, mali, masilahi, haki, stahiki, madeni na wajibu wa Wakala wa Chai Tanzania kufuatia kufutwa kwake ambapo inaeleza kuwa wafanyakazi, mali na madeni vitahamishiwa kwenye bodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni na ushauri wa Kamati. Kwa sehemu kubwa Kamati imekubaliana na mapendekezo ya Muswada yaliyowasilishwa na Mtoa Hoja isipokuwa baadhi ya maeneo Wajumbe wa Kamati walitoa maoni, mapendekezo na kufanya marekebisho ya msingi ili kuboresha Muswada kama inavyofafanuliwa katika aya zinazofuata.

Mheshimiwa Naibu Spika, marekebisho ya Sheria ya usalama wa chakula sura ya 249. Ibara ya tano inapendekeza kufanya marekebisho katika kifungu cha 4(2)(h) kwa kuongeza maneno *and their food commodities* kwa lengo la kuongeza wigo wa mamlaka katika kutoa leseni kwa mtu anayeingiza na kusafirisha bidhaa za chakula. Majadiliano ya Kamati na Serikali yalifikia

mwafaka kuwa maneno *food commodities* yatafsiriwe ili kuondoa mkanganyiko wa maana iliyokusudiwa wakati matumizi ya Sheria ya kuchanganya maana ya maneno *commodity* na *food* yanayotumika katika Sheria ya Viwango, Sura ya 130.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilibaini kuwa marekebisho haya yanasababisha mwingiliano wa jukumu la kutoa leseni ya kuingiza na kusafirisha bidhaa za chakula kati ya *COPRA* na *TBS* ambapo kifungu 30 na 31 cha Sheria ya Viwango, Sura ya 130 kinaipa *TBS* jukumu hilo. Kwa msingi huo, Kamati ilishauri kuwa kuwepo na mashirikiano ya taasisi hizi mbili katika kutoa vibali hivyo ili kuhakikisha ufanisi na kuepuka urudufu wa majukumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, marekebisho ya Sheria ya Tasnia ya Mkonge, Sura ya 30. Ibara ya 18 inapendekeza kufanya marekebisho kwa kuongeza kifungu kipya cha 24(A) cha Sheria kinachohusu ufifilishaji wa makosa. Kamati ilishauri kuwa kifungu hiki kiboreshwe kwa kuweka kinga ya kutoshitakiwa mahakamani kwa kosa ambalo limefifilishwa kwa mtu aliyekiri kosa na kulipa kiwango kilichofifilishwa kama ilivyo katika Ibara ya 13, kifungu kipya cha 39(A)(4) cha Sheria. Serikali ilikubali pendekezo la Kamati na kufanya marekebisho kama ilivyopendekezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu marekebisho ya Sheria ya Tasnia ya Sukari, Sura 251. Ibara ya 22 inapendekeza kufanya marekebisho ya kifungu cha 18(i) cha sheria. Marekebisho haya yanalenga kuipa bodi mamlaka ya kutoa leseni za uingizaji wa sukari kutoka nje ya nchi kwa matumizi ya nyumbani *(domestic use)*, viwandani *(refined sugar for industry use)* na sukari ghafi *(raw sugar)*. Katika majadiliano na Serikali Kamati ilishauri kuwa kifungu hiki kiboreshwe kwa kuweka katazo la kuingiza sukari ghafi *(raw sugar)* kwa mtu yeyote ambaye sio mzalishaji isipokuwa kwa ambaye ni mzalishaji au msafishaji wa sukari mwenye kitu tunaita *operating refinery* na nisisitize *operating refinery*.

Mheshimiwa Naibu Spika, msingi wa ushauri huu ni kwamba itasaidia kuweka udhibiti na kuhakikisha kwa kiasi sahihi cha sukari kinaingizwa, uingizaji unafanywa na viwanda vya kusafisha sukari vinavyofanya kazi, na matumizi ya sukari hiyo yanathibitiwa na

mamlaka husika, jambo litakalosaidia kulinda afya za watumiaji, viwanda vyetu vya ndani, na soko. Serikali ilikubali mapendekezo ya Kamati na kufanya marekebisho kulingana na mapendekezo ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 23 inapendekeza kufuta na kuandika upya Ibara ya 21(1) inayohusu kusaini mkataba wa utekelezaji *(performance contract)* kati ya Bodi ya Sukari na wazalishaji kwa ajili ya utekelezaji na upanuzi wa shughuli za uzalishaji wa sukari, linaendelea kutekelezwa. Hata hivyo, mapendekezo hayo yanaondoa masharti ya awali yanayoweka muda wa kuingia mikataba hiyo ambayo ilikuwa siku 60 kwa wenye leseni mpya na siku 30 kwa ambao wana leseni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashauri kuwa muda wa utekelezaji wa mkataba huo uwe siku 60 ili kuwezesha ufuatiliaji wa maendeleo na upanuzi wa uzalishaji wa sukari kama ilivyokuwa awali. Kwa kuondoa masharti ya muda kwa wanaopata leseni ya kuingiza sukari inaweza kupelekea ugumu wa kutekeleza masharti ya Kifungu cha 21(2) cha sheria kinachoweka muda wa miaka mitano wa utekelezaji wa mkataba. Serikali ilikubali maoni ya Kamati na kuweka marekebisho hayo kwenye jedwali la marekebisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 24 inapendekeza kufanya marekebisho katika Kifungu cha 42 kwa kufuta na kuandika upya Kifungu Kidogo cha kwanza na cha pili kwa kuipa mamlaka Bodi ya Kusajili mtu yeyote anayekusudia kufanya shughuli za kufungasha upya sukari *(repackaging)* kwa matumizi ya kubadili ukubwa, aina ya kifungashio au chapa ya bidhaa *(rebranding)*, ili kujumuisha watu ambao sio wasambazaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilishauriana na Serikali kwa kuzingatia hali halisi ya mazingira ya biashara ya sukari nchini. Kamati ilikuwa na maoni kuwa kifungu hiki kiboreshwe kwa kuweka sharti kuwa suala la kufungasha upya sukari lifanywe na mzalishaji wa ndani *(local manufacturer)* na wafanyabiashara wengine wafungashe sukari ya ndani, *local produced* kwa ajili ya huduma tu *(hospitality and service)* kwa uzito usiozidi gramu 100.

Hii ni kutokana na ukweli kwamba sekta ya sukari imekuwa kwenye mpango kabambe wa kuhakikisha kuwa nchi inazalisha sukari inayotosheleza mahitaji ya ndani, na hivyo ni lazima uwekezaji uendelee; na Serikali ihakikishe mazingira ya biashara yanakuwa himilivu na kulinda viwanda vya ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, ni muhimu kuendelea kulinda viwanda vya ndani na mwanya wowote ambao unaweza kutumika kurudisha nyuma jitihada hizi kupitia wafanyabiashara wasio waaminifu na kupelekea kuathiri wazalishaji wa ndani kinyume na matarajio na mipango ya nchi. Serikali ilikubali pendekezo la Kamati na kufanya marekebisho kama ilivyopendekezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Sheria ya Tasnia ya Chai, Sura 275, mapendekezo ya marekebisho ya sheria hii yanalenga kuifuta Wakala wa Maendeleo ya Wakulima wa Chai Tanzania na kuipa Bodi ya Chai Tanzania majukumu ambayo awali yalikuwa yakitekelezwa na Wakala wa Maendeleo ya Wakulima wa Chai Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, majukumu hayo ni pamoja na kujenga na kukuza uwezo wa wakulima wadogo wa chai, kuwezesha utoaji wa huduma za ugani kwa wakulima wadogo wa chai, kujenga na kuimarisha umoja wa wakulima wadogo wa chai kupitia vikundi vya vyama vyao. Vilevile kuwezesha uendelezaji wa kilimo cha chai katika maeneo mapya na kuhamasisha wakulima wadogo wa chai, kujenga na kuendesha viwanda vyao vya kusindika majani mabichi ya chai.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaona kuwa mabadiliko haya ya sheria yatapunguza ari, msukumo, huduma na hatimaye uzalishaji wa chai na kuleta athari katika ufanisi na kipato cha wakulima na kuendelea kupunguza mchango wa sekta ya chai kwenye pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakulima wadogo wa chai ndio nguzo ya sekta ya chai nchini. Katika miaka 10 wamezalisha 50% ya chai yote nchini. Wakala wamekuwa wakiwaunganisha wakulima na kuwasaidia wakulima wadogo kwenye uzalishaji,

huduma za ugani, masoko, ushirikiano na taasisi au wadau wengine, wakiwemo wale wa Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa msingi huo Kamati ina maoni kuwa, kutokana na muundo wa Bodi ya Chai ambao ni wa udhibiti na usimamizi wa jumla, itakuwa ni ngumu kwa Bodi kufanya majukumu ya kila siku ya kiutendaji yaliyokuwa yanafanywa na wakala kama ilivyoainishwa hapo juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, ni vema ikaanzishwa kurugenzi ndani ya bodi itakayoongozwa na mkurugenzi mwenye sifa stahiki, ambaye ni mtaalamu wa chai, na mwenye uzoefu wa siyo chini ya miaka mitano katika masuala ya maendeleo ya wakulima wadogo wa chai, atakayetekeleza majukumu yaliyokuwa yanatekelezwa na wakala ili wakulima wadogo ambao ni wananchi wa kawaida waendelee kuwa na chombo mahususi chenye jukumu la kuendelea kuwasaidia wakulima kuongeza uzalishaji wenye tija na kunufaika na mnyororo wa thamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na uwepo wa kurugenzi, zitungwe kanuni mahususi zitakazoweka utaratibu wa namna ya wakulima wadogo wa chai watakavyosimiwa na kusaidiwa. Serikali ilikubali pendekezo la Kamati na kufanya marekebisho kama ilivyopendekezwa. Vilevile iliahidi kutengeneza kanuni mahususi kwa ajili ya uendeshaji kwa ajili ya kuonyesha sifa kwa ajili ya kuainisha majukumu ya Kurugenzi ya Wakulima Wadogo wa Chai.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni na ushauri wa jumla. Pamoja na mapendekezo ambayo Kamati imeyatoa katika kila Ibara ya Muswada, Kamati ina maoni na ushauri wa jumla ambao ni vema Serikali ikauzingatia na kuufanyia kazi kwa kuwa ni masuala yanayohusiana na kilimo nchini, kama ifuatavyo:-

(i) Serikali ihakikishe inalinda maslahi mapana ya walengwa, pindi itakapotunga kanuni kwenye vifungu ambavyo Waziri au Bodi imepewa dhamana kwa ajili ya uendeshaji, kwa mujibu wa marekebisho yaliyofanywa, kwa kuhakikisha kuwa

kanuni hizo zinaweka mazingira bora ya utekelezaji wa sheria, zinalinda haki na maslahi ya walengwa.

(ii) Serikali ihakikishe inatoa elimu na uelewa wa kutosha kwa wadau na walengwa wa mabadiliko haya ya sheria, hususan kuhusu kuvunjwa kwa Wakala wa Maendeleo ya Wakulima Wadogo wa Chai na majukumu yake kuhamishiwa kwenye Bodi ya Chai. Elimu hiyo itasaidia kuhamasishwa kwa Bodi ya Chai. vilevile, elimu hiyo itasaidia kuwawezesha wadau kuelewa mabadiliko hayo, majukumu ya taasisi zitakazoathirika na majukumu hayo, pamoja na taratibu na huduma watakazopaswa kuzifuata baada ya mabadiliko hayo ili kuhakikisha kwamba utekelezaji wa sheria mpya unakuwa na ufanisi na haileti mkanganyiko kwa wadau.

(iii) Kamati ilibaini kuwepo kwa mwingiliano wa majukumu kati ya *COPRA* na *TBS*. Kamati inashauri hatua zaidi zianze ili kuondoa mwingiliano huo na kuhakikisha kuwa kila taasisi inabaki kwenye jukumu lake la msingi.

(iv) Mabadiliko ya mara kwa mara ya sheria na ya kiutendaji yanaweza kuathiri kwa kiasi kikubwa utekelezaji endelevu na wenye ufanisi wa mipango na mikakati ya Serikali.

(v) Serikali ihakikishe kwamba inalinda na kuhifadhi maslahi ya watumishi waliokuwa Wakala wa Maendeleo ya Wakulima Wadogo wa Chai, ambao wataendelea na ajira zao chini ya Bodi. Haki hizo zizingatie haki na stahiki zao za msingi za kiutumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho. Ninapenda kuchukua nafasi hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Wajumbe wa Kamati kwa kuujadili na kuuchambua Muswada huu ili kuboresha maudhui yaliyomo katika marekebisho yaliyopendekezwa. Kwa umuhimu wa mchango wao katika kushughulikia Muswada huu, ni kama majina yao yalivyoorodheshwa kwenye taarifa ya Kamati ambayo sitayataja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati, ninapenda kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Daniel Godfrey

Chongolo, Mbunge na Waziri wa Kilimo, na Mheshimiwa David Ernest Silinde Mbunge na Naibu Waziri wa Kilimo kwa ushirikiano mkubwa wanaoupa Kamati ambao kwa sehemu kubwa umechangia kuiwezesha Kamati kutekeleza shughuli zake kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawashukuru pia watendaji wote wa Wizara ya Kilimo na taasisi zilizo chini ya Wizara wakiongozwa na Katibu Mkuu, Bwana Gerald Godfrey Mweli, akisaidiwa na Manaibu Katibu Mkuu, Prof. Peter Msoffe na *Eng.* Athmani Kilundumya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee kabisa, ninamshukuru Katibu wa Bunge, Ndugu Baraka Leonard kwa kuwaongoza vema watumishi wa Ofisi ya Bunge katika uratibu na usimamizi wa shughuli za Kamati kwa ujumla hadi kukamilika kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu msimamo wa Kamati kuhusu hoja. Baada ya kusema hayo, Kamati inalishauri Bunge lako Tukufu kuujadili, kuukubali, na kuupitisha Muswada huu pamoja na jedwali la marekebisho kama lilivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MAONI NA USHAURI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA, KILIMO NA MIFUGO KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA ZA KILIMO WA MWAKA 2026 [ THE AGRICULTURAL LAWS (AMENDMENTS) BILL,2026 – KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI**

---

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1. Maelezo ya Awali

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo, kuhusu

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Kilimo wa Mwaka 2026, [The Agricultural (Amendments)Bill 2026, kwa mujibu wa Kanuni ya 102 (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2025,

**Mheshimiwa Spika**, Muswada wa Sheria ya Kilimo, kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Kilimo wa Mwaka 2026, [ The Agricultural (Amendments)Bill 2026 ulisomwa Bungeni kwa mara ya kwanza katika Mkutano wa Tatu, Kikao cha 58 kwenye Bunge la Kumi na Tatu, tarehe 26 Junii, 2026 kwa mujibu wa Kanuni ya 99(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 100 (1) ikisomwa pamoja na Kanuni ya 139 (14) na Kifungu cha 7(1) (b) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, uliuelekeza Muswada huu kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo ili ufanyiwe uchambuzi na kujadiliwa kwa kina. Naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kwamba, Kamati imeuchambua na kuujadili Muswada huu kwa kuzingatia, Katiba, Sheria mbalimbali pamoja na Kanuni za Kudumu za Bunge.

### 1.2. Namna Uchambuzi wa Muswada ulivyofanyika

**Mheshimiwa Spika**, hatua za kuufanya muswada huu zilianza kwa maandalizi mbalimbali ya kiutendaji yaliyofanywa na Sekretarieti kwaajili ya kuwezesha utekelezaji bora wa shughuli za Kamati. Maelezo ya uchambuzi wa muswada ulifanywa na kuwasilishwa kwenye Kamati na Sekretarieti ya Bunge kwa mujibu wa Kanuni ya 25(2)(b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Hatua hii ilijenga msingi wa utekelezaji wa kazi za Kamati kuhusiana na Muswada huu.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilikutana na Serikali tareheAgosti, 2026 ili kupokea maelezo ya **Mhe. Daniel Godfrey Chongolo, (Mb) Waziri wa Kilimo** kuhusu madhumuni na sababu za Muswada huu. Baada ya Kamati kupatiwa maelezo ya Serikali, Wajumbe walipata fursa ya kuuliza maswali, na kupata maelezo ya ufafanuzi katika ibara mbalimbali za Muswada.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia Kanuni ya 100(2) ya Kanuni za

Kudumu za Bunge Kamati ilifanya Mkutano wa kusikiliza maoni ya wadau *(Public Hearing*) tarehe na 13 Agosti, 2026 ili kupokea maoni yao kuhusu Muswada huu.

**Mheshimiwa Spika**, Napenda kuwashukuru wadau wote waliotoa maoni yao mbele ya Kamati ili kuuboresha Muswada huu. Naomba kuwatambua kwa majina kama ifuatavyo;-

(i) Chama cha Wazalishaji wa Sukari Tanzania (TSPA)
(ii) Chama Kilele cha Ushirika wa Wakulima Wadogo wa Chai Tanzania (TASTGCU)
(iii) Chama cha Wakulima Wadogo wa Chai Njombe (NJOTIKOJE)
(iv) Filbert Kavia-Mshauri Mwelekezi Masuala ya Chai

**Mheshimiwa Spika**, baada ya hatua hiyo, Wajumbe wa Kamati walipata fursa tena ya kujadili maudhui ya Muswada kwa kuzingatia hoja zilizotokana na maelezo, uchambuzi, maoni pamoja na nyaraka mbalimbali kuhusiana na muswada huu. Mnamo tarehe 18 Agosti, 2026 Kamati ilikutana tena na Waziri wa Kilimo ili kujadiliana kuhusu hoja zilizobainika kwa kila ibara ya Muswada na kumshauri Waziri kufanya marekebisho katika Ibara zilioonekana kuhitaji marekebisho kwa mujibu wa Kanuni ya 100(3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya hatua hiyo, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 100 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge na Kamati ilitaarifu Ofisi ya Spika kwamba imekamilisha uchambuzi wa Muswada ili ujadiliwe Bungeni.

## 2.0 UCHAMBUZI WA MUSWADA

**Mheshimiwa Spika**, kamati ilichambua Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Kilimo wa Mwaka 2026, [ The Agricultural (Amendments)Bill 2026, ukiwa umegawanyika katika sehemu Tano (5) na unapendekeza kufanya marekebisho katika sheria Nne (4) kwa madhumuni ya kuondoa mapungufu au dosari au kutatua changamoto ambazo zimejitokeza katika utekelezaji wa Sheria hizo

kama zilivyoelezwa na mtoa hoja mbele ya Kamati. Sheria zinazopendekezwa kufanyiwa marekebisho ni zifuatazo: -

(a) Sheria ya Usalama wa Chakula, Sura ya 249;
(b) Sheria ya Tasnia ya Mkonge, Sura ya 30;
(c) Sheria ya Tasnia ya Sukari, Sura ya 251; na
(d) Sheria ya Tasnia ya Chai, Sura ya 275.

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Kwanza ya Muswada inayohusu masharti ya utangulizi, inajumuisha **Ibara ya 1** inyohusu jina la Sheria inayokusudiwa kutungwa na **Ibara ya 2** inaweka masharti ya namna ambavyo Sheria mbalimbali zinazopendekezwa kurekebishwa katika sehemu zake.

**2.1 Sheria zinazofanyiwa Marekebisho na Maudhui yake.**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imefanya uchambuzi wa maudhui ya marekebisho ya Muswada kwa kuzingatia changamoto ambazo mtoa hoja alieleza Kamati kuwa Muswada huu umelenga kuzitatua pamoja na masuala mengine ambayo Kamati iliona yanafaa kuzingatiwa.

**2.2.1 Sehemu ya Pili ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Usalama wa Chakula, Sura ya 249. Sehemu hii inahusu Ibara ya 3 hadi 13 ya Muswada.**

**Mheshimiwa Spika,** Marekebisho haya yanagusa mambo mbalimbali. Miongoni mwa mambo hayo ni matumizi ya misamiati mahususi katika Sheria hii, kuipa Bodi mamlaka ya kushughulikia na kutatua migogoro kati ya Wakulima na Wafanyabiashara wa nafaka na mazao mchanganyiko kwa njia ya maridhiano badala ya kuamua kwa usuluhishi, kuondoa mamlaka ya Waziri katika kuamua viwango vya malipo ya Wajumbe wa Bodi na kuhamishia kwenye Mamlaka husika, kuboresha mamlaka ya Mkurugenzi Mkuu kama Afisa Mtendaji Mkuu wa Mamlaka pamoja na hadhi na wajibu wa watu walioajriwa na mamlaka.

**Mheshimiwa Spika,** mambo mengine yaliyojitokeza katika

mapendekezo ni marekebisho yanayolenga kujumuisha zao la Pareto miongoni mwa mazao mchanganyiko yatakayosimamiwa na COPRA na kuiwezesha Mamlaka hiyo kutekeleza majukumu yaliyokuwa yanatekelezwa na Bodi ya Pareto Tanzania.

Aidha, Mapendekezo haya yanaanisha haki ya kukata rufaa dhidi ya Uamuzi wa Mamlaka ya kukataa kutoa leseni, rufaa hiyo itakatwa kwa maandishi kwenda kwa Waziri. Lengo la marekebisho haya ni kuimarisha utoaji haki kwa mtu ambae hajaridhika na uamuzi wa Mamlaka.

**Mheshimiwa Spika,** Jambo lingine ni kumpa mamlaka Waziri mwenye dhamana ya masuala ya Kilimo kutangaza kwa Notisi kwenye Gazeti la Serikali zao lolote la kilimo kuwa kati ya mazao mchanganyiko.

Halikadhalika marekebisho haya yanaweka utaratibu wa ufifilishaji wa makosa (Compounding of offences) ambapo inampa Mkurugenzi Mkuu au Mtu aliyeidhinishwa wakati wowote kabla ya kesi kuanza mahakamai, kufifilisha kosa na kuamuru mkosaji kulipa kiasi cha fedha kisichozidi nusu ya faini ambayo angelazimika kulipa ikiwa angepatikana na hatia na ikiwa atashindwa kulipa fedha iliyoamuriwa kulipa atatozwa riba kwa kiwango kitakachobainishwa kwenye Kanuni. Vilevile inaweka masharti kuwa mtu aliyeshtakiwa kulipa kiwango kilichofifilishwa hatashtakiwa mahakamani kwa kosa ambalo limefifilishwa.

**2.2.2 Sehemu ya tatu ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho ya Sheria ya Tasnia ya Mkonge, Sura ya 30. Sehemu hii inahusu ibara ya 14 hadi 18 ya Muswada.**

**Mheshimiwa Spika,** Katika sheria hii yapo mambo mbalimbali yanayolengwa kubadilika kwa marekebisho ya sheria inayopendekezwa, mambo hayo ni pamoja na kuhamisha mamlaka kutoka Bodi ya Mkonge kwenda kwa Waziri. Mapendekezo haya yanampa Waziri mamlaka ya kutunga Kanuni zinazohusu uchakataji, usafirirshaji nje ya nchi na uhifadhi wa Mkonge.

**Mheshimiwa Spika,** mambo mengine ni kuweka utaratibu wa ufifilishaji wa makosa yaliyoanishwa chini ya sheria hii. Lengo la marekebisho haya ni kuanzisha utaratibu wa makosa madogo ya kisheria kwa njia ya kiutawala badala ya kuyapeleka yote mahakamani ili kuongeza ufanisi wa sheria na kuboresha utekelezaji wa sheria katika tasnia ya Mkonge.

**2.2.3 Sehemu ya Nne ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho ya Sheria ya Tasnia ya Sukari, Sura 251 Sehemu hii inahusu ibara ya 19 hadi 26 ya Muswada.**

**Mheshimiwa Spika,** Marekebisho yanayope-ndekezwa yanaleta masharti mapya ya usajili wa Viwanda au Mitambo ya kutengeneza sukari ambapo inaeleza kuwa Bodi itatoa usajili kwa watu wanaokusudia kuanzisha viwanda au mitambo ya kuzalisha sukari za nyumbani, sukari ya viwandani, sukari maalumu pamoja na bidhaa zinazotokana na miwa au bidhaa zitokanazo na uzalishaji wa sukari.

**Mheshimiwa Spika,** jambo jingine ni kuipa mamlaka Bodi kutoa leseni za uingizaji wa sukari kwa matumizi ya nyumbani, viwandani na sukari ghafi. Lengo la marekebisho haya ni kuongeza udhibiti na kukuza uwekezaji katika tasnia ya sukari. Vilevile mapendekezo ya marekebisho, yanalenga kuipa Bodi ya Sukari mamlaka ya kuingia Mkataba wa utekelezaji na mzalishaji wa sukari kwa lengo la kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa mipango ya maendeleo au upanuzi wa uwezo wa uzalishali wa sukari.

**Mheshimiwa Spika,** marekebisho yanalenga kuongeza wigo wa watu wanaokusudia kufungasha upya sukari inayozalishwa ndani ya nchi kwa ukubwa usiozidi gramu 100, ili kuwajumuisha watu ambao si wazalishaji waliosajiliwa na Bodi.

**2.2.4 Sehemu ya tano ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho ya Sheria ya Tasnia ya Chai, Sura ya 275. Sehemu hii inahusu ibara ya 27 hadi 35 ya Muswada.**

**Mheshimiwa Spika,** mapendekezo ya marekebisho ya sheria hii yanalenga kuifuta Wakala wa Maendeleo ya Wakulima wa Chai Tanzania na kuipa Bodi ya Chai Tanzania majukumu ambayo awali yalikuwa yakitekelezwa na Wakala wa Maendeleo ya Wakulima wa Chai Tanzania. Aidha, mapendekezo yanaweka masharti ya mwendelezo wa mpito kuhusiana na wafanyakazi, mali, maslahi, haki, stahili, madeni na wajibu wa Wakala wa Chai Tanzania kufuatia kufutwa kwake, ambapo kinaeleza kuwa Wafanyakazi, mali na madeni vitahamishiwa kwenye Bodi.

## 3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, kwa sehemu kubwa Kamati imekubaliana na mapendekezo ya Muswada yaliyowasilishwa na mtoa hoja. Isipokuwa baadhi ya maeneo Wajumbe wa Kamati walitoa maoni, mapendekezo na kufanya marekebisho ya msingi ili kuboresha muswada huu kama inavyofafanuliwa katika aya zinazofuata.

### 3.1 Marekebisho ya Sheria ya Usalama wa Chakula, Sura ya 249.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 5 iinapendekeza kufanya marekebisho katika Kifungu cha 4 (2)(h) kwa kuongeza maneno "*and their food commodities*" kwa lengo la kuongeza wigo wa Mamlaka katika kutoa leseni kwa mtu anayeingiza na kusafirisha bidhaa za chakula. Majadiliano ya Kamati na Serikali yalifikia mwafaka kuwa maneno "*food commodities*" yatafsiriwe ili kuondoa mkanganyiko wa maana iliyokusudiwa wakati wa matumizi ya Sheria na kuchanganya maana ya maneno "*commodity*" na "*food*" yanayotumika katika Sheria ya Viwango Sura 130.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilibaini kuwa marekebisho haya

yanasababisha mwingiliano wa jukumu la kutoa leseni ya kuingiza na kusafirisha bidhaa za chakula kati ya COPRA na TBS ambapo Kifungu cha 30 na 31 cha Sheria ya Viwango Sura ya 130 kinaipa TBS jukumu hilo. Kwa msingi huo Kamati ilishauri kuwa kuwepo na mashirikiano ya Taasisi hizi mbili katika kutoa vibali hivyo ili kuhakikisha ufanisi na kuepuka urudufu wa majukumu.

### 3.2 Marekebisho ya Sheria ya Tasnia ya Mkonge, Sura ya 30

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 18 inapendekeza kufanya marekebisho kwa kuongeza Kifungu kipya cha 24A cha Sheria kinachohusu ufifilishaji wa makosa. Kamati ilishauri kuwa Kifungu hiki kiboreshwe kwa kuweka kinga ya kutoshtakiwa Mahakamani kwa kosa ambalo limefifilishwa kwa mtu aliyekiri kosa na kulipa kiwango kilichofifilishwa kama ilivyo katika Ibara ya 13 Kifungu kipya cha 39A (4) cha Sheria. Serikali ilikubali pendekezo la Kamati na kufanya marekebisho kama ilivyopendekezwa.

### 3.3 Marekebisho ya Sheria ya Tasnia ya Sukari, Sura 251

**Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 22 inapendekeza kufanya marekebisho katika Kifungu cha 18(1) cha Sheria. Marekebisho haya yanalenga kuipa Bodi mamlaka ya kutoa leseni za uingizaji wa sukari kutoka nje ya nchi kwa matumizi ya Nyumbani (*domestic use*), Viwandani (*refined sugar for industrial use*) na sukari ghafi (*raw sugar*). Katika majadiliano na Serikali, Kamati ilishauri kuwa Kifungu hiki kiboreshwe kwa kuweka katazo la kuingiza sukari ghafi (raw sugar) kwa mtu yeyote ambaye si mzalishaji (refinery) au ambaye ni mzalishaji/msafishaji wa sukari (Operating refinery).

**Mheshimiwa Spika,** msingi wa ushauri huu ni kwamba itasaidia kuweka uthibiti na kuhakikisha kuwa kiasi sahihi cha sukari kinaagizwa, uingizaji unafanywa na viwanda vya kusafisha sukari vilivyopo na vinavyofanya kazi na matumizi ya sukari hiyo yanathibitihswa na mamlaka husika jambo litakalosaidia kulinda afya za watumiaji, viwanda na soko. Serikali ilikubali mapendekezo ya Kamati na kufanya marekebisho kulingana na mapendekezo ya Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 23 inapendekeza kufuta na kuandika upya Ibara ya 21(1) kinachohusu kusaini mkataba wa utekelezaji (*performance contract*) kati ya Bodi ya Sukari na Wazalishaji kwaajil ya uendelezaji na upanuzi wa shughuli za uzalishaji wa sukari linaendelea kutekelezwa. Hata hivyo mapendekezo haya yanaondoa masharti ya awali yanayoweka muda wa kuingia mikataba hiyo ambapo ilikuwa siku 60 kwa wenye leseni mpya na siku 30 kwa ambao wanaleseni.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inashauri kuwa muda wa utekelezaji wa Mkataba huo uwe siku 60 ili kuwezesha ufuatiliaji wa maendeleo na upanuzi wa uzalishaji wa sukari kama ilivyokuwa awali. Kwa kuondoa masharti ya muda kwa wanaopata leseni kuingiza sukari inaweza kupelekea ugumu wa kutekeleza masharti ya Kifungu cha 21(2) cha Sheria kinachoweka muda wa miaka mitano wa utekelezaji wa Mkataba. Serikali ilikubaliana na maoni ya Kamati na kuweka marekebisho hayo kwenye jedwali la marekebisho.

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 24 inapendekeza kufanya marekebisho katika Kifungu cha 42 kwa kufuta na kuandika upya kifungu kidogo cha (1) na cha (2) kwa kuipa mamlaka Bodi ya kusajili mtu yeyote anayekusudia kufanya shughuli za kufungasha upya sukari (re- packing) kwa madhumni ya kubadili ukubwa, aina ya kifungashio au chapa ya bidhaa (re-branding) ili kuwajumuisha watu ambao si wazalishaji.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilishauriana na Serikali kwa kuzingatia hali halisi ya mazingira ya biashara ya sukari nchini. Kamati ilikuwa na maoni kuwa Kifungu hiki kiboreshwe kwa kuweka sharti kuwa suala la kufungasha upya sukari lifanywe na mzalishaji wa ndani (local manufacturer) na wafanyabiashara wengine wafungashe sukari ya ndani (local produced) kwa ajili ya huduma tu (Hospitality and Services) kwa uzito usiozidi gramu 100. Hii ni kutokana na ukweli kwamba Sekta ya sukari imekuwa kwenye mpango kabambe wa kuhakikisha nchi inazalisha sukari itakayotosheleza mahitaji ya ndani, na hivyo ni lazima uwekezaji uendelee na Serikali ihakikishe mazingira ya biashara yanakuwa

himilivu na kulinda viwanda vya ndani. Hivyo ni muhimu kuendelea kulinda viwanda vya ndani na mwanya wowote ambao unaweza kutumika kurudisha nyuma jitihada hizo kupitia wafanyabiashara wasio waaminifu na kupelekea kuathiri wazalishaji wa ndani kinyume na matarajio na mipango ya nchi. Serikali ilikubali pendekezo la Kamati na kufanya marekebisho kama iliyopendekezwa.

**3.4 Sheria ya Tasnia ya Chai, Sura ya 275.**

**Mheshimiwa Spika,** mapendekezo ya marekebisho ya sheria hii yanalenga kuifuta Wakala wa Maendeleo ya Wakulima wa Chai Tanzania na kuipa Bodi ya Chai Tanzania majukumu ambayo awali yalikuwa yakitekelezwa na Wakala wa Maendeleo ya Wakulima wa Chai Tanzania. Majukumu hayo ni pamoja na kujenga na kukuza uwezo wa wakulima wadogo wa chai, kuwezesha utoaji wa huduma za ugani kwa wakulima wadogo wa chai, kujenga na kuimarisha umoja wa Wakulima Wadogo wa Chai kupitia vikundi na vyama vyao, kuwezesha uendelezaji wa kilimo cha chai katika maeneo mapya na kuwahamasisha wakulima wadogo wa chai kujenga na kuendesha viwanda vyao vya kusindika majani mabichi ya chai.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaona kuwa mabadiliko haya ya sheria yatapunguza ari, msukumo, huduma na hatimaye uzalishaji wa chai na kuleta athari katika ufanisi na kipato cha wakulima na kuendelea kupunguza mchango wa sekta ya chai kwenye pato la taifa. Wakulima wadogo wa chai ndiyo nguzo ya sekta ya chai nchini katika miaka 10 wamezalisha 50% ya chai yote nchini. Wakala umekuwa ukiwaunganisha wakulima na kuwasaidia wakulima wadogo kwenye uzalishaji, huduma za ugani, masoko na ushirikiano na taasisi au wadau wengine wakiwemo wale wa Kimataifa.

**Mhehimiwa Spika,** kwa msingi huo Kamati ina maoni kuwa kutokana na muundo wa Bodi ya Chai ambao ni wa uthibiti na usimamizi wa jumla itakuwa ni ngumu kwa Bodi kufanya majukumu ya kila siku ya kiutendaji yaliyokuwa yanafanywa na Wakala kama yalivyoanishwa hapo juu. Hivyo ni vema ikaanzishwa

kurugenzi ndani ya Bodi itakayoongozwa na Mkurugenzi mwenye sifa stahiki ambaye ni mtaalamu wa chai na mwenye uzoefu wa si chini ya miaka mitano katika masuala ya maendeleo ya wakulima wadogo wa chai, atayetekeleza majukumu yaliyokuwa yanatekelezwa na Wakala ili wakulima wadogo ambao ni wananchi wa kawaida waendelee kuwa na chombo mahsusi chenye jukumu la kuendelea kuwasaidia wakulima kuongeza uzalishaji wenye tija na kunufaika na mnyororo wa thamani. Pamoja na hiyo kurugenzi zitungwe Kanuni mahususi zitakazoweka utaratibu wa namna ya Wakulima Wadogo wa Chai watakavyosimamiwa na kusaidiwa. Serikali ilikubali pendekezo la Kamati na kufanya marekebisho kama iliyopendekezwa na vilevile iliahidi kutengeneza Kanuni Mahsusi kwa ajili ya uendeshaji, kuanisha majukumu ya Kurugenzi ya Wakulima Wadogo wa Chai.

## 4.0 MAONI NA USHAURI WA JUMLA

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mapendekezo ambayo Kamati imeyatoa katika kila Ibara ya Muswada, Kamati ina maoni na ushauri wa jumla ambao ni vema Serikali ikauzingatia na kuufanyia kazi kwa kuwa ni masuala yanayohusiana na kilimo nchini kama ifuatavyo;

(a) Serikali ihakikishe inalinda maslahi mapana ya walengwa pindi itakapotunga Kanuni kwenye vifungu ambavyo Waziri au Bodi imepewa dhamana kwa ajili ya uendeshaji kwa mujibu wa Marekebisho yaliyofanywa kwa kuhakikisha kuwa Kanuni hizo zinaweka mazingira bora ya utekelezaji wa sheria, zinalinda haki na maslahi ya walengwa.

(b) Serikali ihakikishe inatoa elimu na uelewa wa kutosha kwa wadau na walengwa wa mabadiliko haya ya sheria, hususan kuhusu kuvunjwa kwa Wakala wa Maendeleo ya Wakulima Wadogo wa Chai na majukumu yake kuhamishiwa kwenye Bodi ya Chai. Elimu hiyo itasaidia kuwawezesha wadau kuelewa mabadiliko hayo, majukumu ya taasisi zitakazoathiri majukumu hayo, pamoja na taratibu na huduma watakazopaswa kuzifuata baada ya mabadiliko hayo ili kuhakikisha utekelezaji wa sheria mpya unakuwa na ufanisi na

haileti mkanganyiko wa wadau.

(c) Kamati ilibaini kuwepo na mwingiliano wa Majukumu katika ya COPRA na TBS. Kamati inashauri hatua zaidi zianze ili kuondoa mwingiliano huo na kuhakikisha kila taasisi inabaki kwenye jukumu lake la msingi.

(d) Mabadiliko ya mara kwa mara ya sheria na ya kiutendaji yanaweza kuathiri kwa kiasi kikubwa utekelezaji endelevu na wenye ufanisi wa mipango na mikakakati ya Serikali.

(e) Serikali ihakikshe inalinda na kuhifadhi maslahi ya watumishi waliokuwa wa Wakala wa Maendeleo ya Wakulima Wadogo wa Chai ambao wataendelea na ajira zao chini ya Bodi ya Pareto. Haki hiyo izingatie haki na stahili zao za msingi za kiutumishi.

## 5.0 HITIMISHO

### 5.1 Shukrani

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuchukua fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Wajumbe wa Kamati kwa kuujadili na kuuchambua Muswada huu ili kuboresha maudhui yaliyomo katika marekebisho yanayopendekezwa. Kwa umuhimu wa mchango wao katika kushughulikia muswada huu, naomba niwatambue kama ifuatavyo: -

1. Mhe. Deodatus Philip Mwanyika, Mb **Mwenyekiti**
2. Mhe. Mariam Ditopile Mzuzuri, Mb **M/Mwenyekiti**
3. Mhe. Salma Rashid Kikwete, Mb Mjumbe
4. Mhe. Prof. Sospeter Mwijarubi Muhongo, Mjumbe
5. Mhe. Yustina Arcadius Rahhi, Mb Mjumbe
6. Mhe. Khadija Hassan Aboud, Mb Mjumbe
7. Mhe. Tauhida Galos Cassian, Mb Mjumbe
8. Mhe. Emmanuel Peter Cherehani, Mb Mjumbe
9. Mhe. Omar Marcus Msigwa, Mb Mjumbe
10. Mhe. Suma Ikenda Fyandomo, Mb Mjumbe
11. Mhe. Kabula Enock Shitobelo, Mb Mjumbe
12. Mhe. Dkt.Rita Enerpher Kabati, Mb Mjumbe

13. Mhe. Livingstone Joseph Lusinde Mb Mjumbe
14. Mhe. Magreth Baraka Ezekiel, Mb Mjumbe
15. Mhe. Abubakar Alli Omari, Mb Mjumbe
16. Mhe. Kenneth Ernest Nollo, Mb Mjumbe
17. Mhe. Mojamed Issa Khalifan, Mb Mjumbe
18. Mhe. Mohamed Issa Khalifan, Mb Mjumbe
19. Mhe. Jacqueline Kandidus Ngonyani, Mb Mjumbe
20. Mhe. Khamis Hamad Yussuf, Mb Mjumbe
21. Mhe. Amour Seif Abdalla, Mb Mjumbe
22. Mhe. Khalid Mussa Nsekela, Mb Mjumbe
23. Mhe. Ghati Zephania Chomete, Mb Mjumbe
24. Mhe. Salum Khamis Salum, Mb Mjumbe
25. Mhe. Dickson Nathan Lutevele Villa Mjumbe

**Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati napenda kumshukuru Mhe. Daniel Godfrey Chongolo (Mb) - Waziri wa Kilimo na Mhe. David Ernest Silinde (Mb) – Naibu Waziri wa Kilimo, kwa ushirikiano mkubwa wanaoipatia Kamati ambao kwa sehemu kubwa umechangia kuiwezesha Kamati kutekeleza shughuli zake kikamilifu. Nawashukuru pia watendaji wote wa Wizara ya Kilimo na Taasisi zilizo chini ya Wizara wakiongozwa na Katibu Mkuu Bwana Gerald Geofrey Mweli, akisaidiwa na Naibu Makatibu Prof. Peter Msoffe na Ndg. Athumani Kilundumya

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee namshukuru Katibu wa Bunge - Ndg. Baraka I. Leonard kwa kuwangoza vyema watumishi wa Ofisi ya Bunge katika uratibu na usimamizi wa shughuli za Kamati kwa ujumla hadi kukamilika kwa taarifa hii.

**5.2 Msimamo wa Kamati Kuhusu Hoja**

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo, Kamati inalishauri Bunge lako tukufu kuujadili, kuukubali na kuupitisha Muswada huu pamoja na Jedwali la Marekebisho kama lilivyowasilishwa na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

Deodatus Philip Mwanyika (Mb)

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA, KILIMO NA MIFUGO**

27 Agosti, 2026

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kwa kutoa maoni na mapendekezo na ushauri wa Kamati kwa Serikali.

Waheshimiwa Wabunge, kama ilivyo desturi, baada ya kupokea taarifa ya mtoa hoja, na baada ya kupokea maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge, tunaingia hatua ya mjadala na tutaanza na Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo, atafuatiwa na Mheshimiwa Yustina Arcadius Rahhi, Mheshimiwa Dkt. Ritta Enespher Kabati, ajiandae.

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia Muswada huu ulioletwa na Serikali. Nitajikita zaidi kwenye sheria ya Sheria ya Tasnia ya Sukari Sura Na. 251.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya yote nichukue nafasi hii kwa dhati kabisa, nimshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kufanya uteuzi kupitia Halmashauri Kuu na Kamati Kuu, kumteua Mheshimiwa Deogratius John Louis Pancras Mtemi Ndejembi kuwa Makamu wa Rais. Ni imani kubwa sana, na mimi ninamfahamu vizuri Ndugu Deogratius Ndejembi kwamba atatoa msaada mkubwa katika kumshauri Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na maoni ambayo Kamati imeyatoa kwa Serikali, nilitaka nisisitize kwenye kipengele cha Bodi kutoa kibali cha wafungashaji wa sukari, *(packaging and rebranding)* ili kuweka uzito zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa ninashauri kwamba, kwanza, kama ambavyo tumekubaliana na Serikali, kwamba *packaging and rebranding* itafanyika kwa sukari ya

ndani *(local produced sugar)*, vilevile mimi nilitaka niende mbali, niseme kwamba Bodi itatoa usajili huo au ithibati hiyo baada ya huyu mfungashaji na anayefanya *repackaging*, kwanza apate idhini ya mzalishaji. Maana tukiachia hapo, mtu anaweza akafanya *forgery*, akasema mimi ninafungasha sukari, *traceability* yangu ni sukari ya Mtibwa. Kumbe Mtibwa hana habari kwamba kuna mtu anatumia *brand* ya sukari yake kufungasha sukari.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufanya hivyo maana yake tutaondoa mianya ya sukari kutoka nje, kuja kufungashiwa hapa ndani, na ikatumia viwanda vya ndani. Kwa hiyo, iwe inafanya kazi katika utatu mtakatifu, kwa maana ya Bodi ya Sukari, *manufacturer*, halafu na yule anaye-*rebrand*. Pia bodi itatoa, baada ya kuona mkataba wa kuridhia kutoka kwa *manufacturer* ambaye huyu ataweza kufanya *branding*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi nilikuwa ninaona jambo hili, twende zaidi kwamba, huyu anayefanya *branding* hatafanya, hadi awe ameingia mkataba/makubaliano na *local manufacturer*. Kwa kufanya hivyo, tutakuwa tumeweka mizani sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni kuhusu kuanzisha viwanda vya sukari ya viwandani na *refinery sugar*. Hapa napo, kwanza nchi yetu imepiga hatua sana katika kusimamia uzalishaji wa sukari, kiasi kwamba tuna utoshelevu. Sasa, ni mazingira gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, bodi ni lazima itoe usajili, kwamba tunahitaji hapa *refinery* ya sukari. Ina maana Serikali itatangaza kama tenda, isiwe mimi mwekezaji ninataka kutengeneza *refinery*. Hii nayo itasaidia kulinda uzalishaji wa ndani, kusiwe na mianya ya kuzalisha sukari hapa, wakati wengine wanalima halafu ndipo wanaingia kwenye kiwanda, huyu anaanza sasa *outright* kwenye uzalishaji. Kwa hiyo, kuwe kuna tangazo la tenda kwa ajili ya mtu anayetaka kujenga *refinery* tukiwa tuna lengo kwamba uzalishaji wake utakuwa kiasi hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni kama nilivyosema, kwamba suala la bodi kutoa usajili ni *demand driven,* lakini kwenye sukari ya viwandani, hapa napo bodi inahitaji umakini,

kwamba je, ile *crude* au *raw sugar* ambayo tunataka iende ikazalishe kwa ajili ya sukari ya viwandani, mtu hawezi ku-*temper* akazalisha kwa ajili ya *consumption* ya kawaida, badala ya kutumika sukari hiyo kwenye viwanda. Kwa hiyo, Bodi vilevile inahitaji hapa kujiridhisha katika kutoa kibali.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mwisho ambalo na mimi tulikubaliana na Serikali kupitia kwenye Kamati, ni kuhusu vifungashio, kwamba isizidi gramu 100. Jambo hili ni nzuri, lakini vilevile ni lazima tuwe na *category*. Kwamba, anayetaka ku-*rebrand* ni mtu anayefanya *service,* kwa mfano kwenye mahoteli au anataka ku-*rebrand* auze mtaani. Hiyo nayo ni lazima kuifanyia *scrutiny,* la sivyo mtu anaweza akavifyatua vya gramu mia mia, inakuwa kama *marketing segmentation*, ili aweze kuiuza baadaye katika *big scale*. Kwa hiyo, hili jambo nalo ni lazima tuweke *category,* kwamba ni watoa huduma wa aina gani wanaotakiwa ku-*rebrand*.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninakushukuru kwa kunipa nafasi, ninaunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Ernest Nollo. Nilimtaja Mheshimiwa Yustina Arcadius Rahhi, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Ritta Enespher Kabati, Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud, ajiandae.

**MHE. YUSTINA A. RAHHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia hoja hii ya marekebisho ya sheria mbalimbali za kilimo. jambo la kwanza, ninampongeza Waziri mwenye dhamana, Mheshimiwa Dkt. Daniel Chongolo pamoja na Naibu kwa kuweza kuleta Miswada hii kwa kipindi hiki, ambapo kiukweli kwenye kilimo kutokana na mabadiliko mbalimbali ya kiteknolojia na matumizi ya mazao ya kilimo ni *inevitable*. Kwa hiyo, ninawapongeza kwamba wameweza kuleta hizi sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kidogo kuhusu Sheria ya Tasnia ya Mkonge, Sura Na. 30. Mabadiliko yamefanyika katika Ibara ya 14 hadi 18, na nikisemee kifungu kipya cha 24, ambapo

sheria inaweka kinga kwa mtu yeyote ambaye amefanya makosa madogo madogo, lakini amefilisiwa au amepigwa faini, na amekiri kosa, amelipa faini, asipelekwe mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba makosa haya, maana kuna wafanyabiashara wengine kama faini inakuwa ndogo, pengine shilingi 30,000, au shilingi 50,000 amepigwa faini, atarudia kosa, kwani anajua faini yake ni 50,000 tu atalipa. Makosa haya yanaporudiarudia, bado ninapendekeza kwamba hatua za kumpeleka mahakamani au hatua nyingine zifuatwe tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu mwingine niuelekeze kwenye Tasnia ya Sukari, Sura 251, ambako kumekuwa na marekebisho katika Ibara ya 19 hadi 26. Nichangie kidogo katika Ibara ya 22, Kifungu cha 18, ambapo Bodi imepewa mamlaka ya kutoa leseni ya kuingiza sukari nchini, sukari kwa *domestic*, sukari ya viwandani na *raw sugar*. Nisemee tu kwamba sheria hii inahusu zaidi hii sukari ya viwandani, maana hii sukari yetu ya *domestic* tulishawapa *NRFA* kuleta sukari panapokuwa na *gap* au *buffer stock*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hii sukari ambayo inahitajika viwandani, wapewe watu ambao tayari wana viwanda vya *refinery* ambavyo vinafanya kazi, siyo kuonyesha tu kwamba tuna kiwanda na hakifanyi kazi. Hao ndio wanapaswa kupewa vibali vya kuleta sukari. Hii kusema kweli ni kwa ajili ya kulinda viwanda vyetu vya ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tuna kiwanda cha Mkulazi, ambapo nao wanazalisha sukari ya viwandani. Mahitaji ya sukari *raw*, ni tani 300,000; na hiki kiwanda chetu kina uwezo wa kuzalisha; na lengo lake ni kuzalisha kwenye tani 50,000. Tutakapokuwa na uwezo wa kuzalisha, basi kibali kitolewe kwa lile *gap*, na kwa kiwanda ambacho *already* kina *refinery*.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme pia kuhusu sheria hii ya vifungashio Ibara ya 24, Kifungu cha 42, inahusu kufungasha upya, *repacking*. Mtu yeyote anayetaka kufanya *repacking*, sheria imeelekeza, kwanza kupata kibali kutoka Bodi, lakini hii ni

kwa ajili ya matumizi ya huduma hizi *hospitality* pamoja na *service*. Sukari ambayo tunaona iko kwenye hospitali, kwenye mahoteli, *SGR*, na ndege, hizi zinaanza gramu tano lakini isizidi gramu 100.

Mheshimiwa Naibu Spika, sukari hii, lazima iwe sukari iliyozalishwa ndani ya nchi yetu, siyo sukari inayotoka nje. Hii ni kwa sababu kusema ukweli tunapaswa kulinda viwanda vyetu vya ndani. Wako wafanyabiashara ambao siyo waaminifu wanaleta sukari nyingi kutoka nje na wata-*repack* na kui-*brand* wanavyotaka; hii itadhoofisha nguvu ya viwanda vyetu vya ndani kuzalisha sukari. Kwa hiyo, Bodi hapa iwe macho tu kwamba itatoa vibali kwa sukari ambayo inazalishwa ndani ya nchi, lakini ni kwa ajili ya kulinda afya
ya walaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii sukari kuna utaratibu ambao Serikali *already* inafanya. Sukari inayokuja kama *raw sugar* inayopaswa kwenda viwandani, kwanza tunajua itakaa kwenye Ghala la Forodha pale *(bonded warehouse)*, itapata vipimo na itaelekezwa kiwandani, siyo kuja kutumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna wafanyabiashara ambao si waaminifu. Hii sukari ambayo ni *raw*, ambayo haifai kabisa kwa matumizi ya binadamu inakuwa *repacked*, na watu watauziwa na watakula kitu ambacho ni hatari kabisa kwa afya ya Watanzania. Kwa hiyo, tuombe Bodi na Serikali hapo iwe macho.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kudhibiti kiwango. Tunahitaji sukari kiasi gani? Tukii-*flood* nchi yetu na sukari kutoka nje tena kwa bei ndogo, ina maana, basi wazalishaji wote wa ndani na viwanda vya ndani vita-*cease*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu mwingine wa mwisho niuelekeze kwenye Tasnia ya Chai Sura 271. Sheria ya Marekebisho hapa inalenga kuondoa au kufuta Wakala wa Chai. Hao Wakala wa Chai walikuwa karibu zaidi na wakulima wadogo, na wakulima wadogo kwenye Tasnia ya Chai ndiyo wenye

mchango mkubwa. Karibu 50% ya chai ya Tanzania inazalishwa na wakulima wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hao walikuwa na kazi mbalimbali; kuwaunganisha wakulima pamoja, kuhakikisha kwamba wanapata huduma ya ugani kwa sababu kupitia kwa mawakala, kuna Maafisa Ugani pia walikuwa wameajiriwa ili kuwasogelea wakulima, na vilevile kuwapa mitaji na kuwaunganisha kupitia vyama vyao vya asili. Lengo lilikuwa ni kuwasaidia wakulima wadogo wadogo kuweza kuanzisha viwanda vidogo vidogo. Kama tunavyoona wakulima wa Kenya, pamoja na Sri Lanka, wana viwanda vidogo vidogo vingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa tumekubaliana kwamba haya majukumu yaende kwenye bodi, na bodi tunajua ni kitu kikubwa, sisi tuiombe Serikali au bodi, jicho kubwa liende kwa wakulima wadogo ambao tunaona wanakua kuliko wakulima wakubwa na kuliko mashamba makubwa. Pia, ifanye hivi kwa kuanzisha kurugenzi na hii kurugenzi wateuliwe wale ambao wamebobea kwenye Tasnia ya Chai.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tuwasogezee zaidi huduma ya ugani. Huduma ya ugani isiwe *pool* tu kwamba kwenye *NAESA*, Afisa Kilimo yeyote apelekwe kwenye eneo la chai. Tuhakikishe tu kwamba Maafisa Ugani watakaoenda kufanya kazi na hao wakulima wadogo wadogo, wawe wamebobea kwenye zao la chai.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga hoja mkono, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Yustina Rahhi. Nilimtaja Mheshimiwa Dkt. Ritta Enespher Kabati, atafuatiwa na Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud, na Mheshimiwa Ramadhani Hamza Singano ajiandae.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia hoja iliyoko

Mezani. Ninamshukuru sana Mwenyezi Mungu, lakini pia nikushukuru kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, kabla sijachangia mchango wangu, na mimi ninaungana na wenzangu wote kwa kumpongeza na kumshukuru Mheshimiwa Rais wetu na Kamati Kuu ya Chama cha Mapinduzi kwa kumteua Mheshimiwa Deogratius Ndejembi kuwa Makamu wa Rais. Sisi Waheshimiwa Wabunge kwa kweli tunaahidi ushirikiano mkubwa sana hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wetu wa Kilimo kwa kazi nzuri sana ambazo ameendelea kufanya katika Wizara yetu. Nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri pamoja na Katibu Mkuu, na watendaji wote wa Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nimpongeze sana Mwenyekiti wetu wa Kamati, amefanya kazi kubwa sana mpaka kuona kwamba hii sheria imeletwa humu ndani. Niwapongeze na Wajumbe wa Kamati hii, maana yake mpaka kupitishwa hii sheria, tumekaa, mpaka kuelimishwa, ilikuwa siyo kazi ndogo. Kwa hiyo, ninampongeza sana Mwenyekiti wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba mchango wangu nijikite kwenye Sheria ya Tasnia ya Chai, Sheria Na. 275. Marekebisho ya sheria hii, kama ambavyo mchangiaji wa nyuma alivyosema, inaenda kufuta kabisa Wakala wa Maendeleo ya Wakulima wa Chai Tanzania, na inaenda kuipa mamlaka Bodi ya Chai ya Tanzania kusimamia.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaona kwamba kazi ya wakala kwanza ilikuwa ni kuwaunganisha wakulima wote wale wadogo wadogo, na ilikuwa, ikiwasaidia kuzalisha na kutoa huduma kama ile ya ugani ambapo siku zote ule wakala ulikuwa unafanya kazi moja kwa moja na wale wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile ilikuwa inawatafutia wadau mbalimbali, wa ndani na wa nje na taasisi mbalimbali kwa

kuwapatia mitaji. Ndiyo maana tulikuwa tunaona kama kutakuwa na ugumu. Je, hawa wanaotusaidia kutoka nje, wataisaidia Serikali au watasaidiwa tena hawa wakulima wetu wadogo?

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kama Kamati tulipata bahati nzuri sana ya kuwasikiliza mawakala na wadau mbalimbali katika Kamati yetu na tukajiridhisha. Ndiyo maana leo hii tumekubaliana na Serikali, lakini yako mambo ambayo tuliona ni muhimu. Ninaomba nitoe mfano mmoja tu ambao wakala ulifanya vizuri sana *(NOSC)*. Huyu *NOSC* ni wakala ambaye anatoka kule Njombe katika kata ya Igominyi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaona kwamba huyu wakala alikuwa anasimamia; kwanza walikuwa wanamiliki 45% ya chai, lakini eneo la kilimo wakati wanalisimamia, walikuwa wamepokea hekta 500, baadaye wakapata hekta 3,000. Pia katika uzalishaji, kabla *NOSC* haijaweza kuwa wakala, walikuwa wanazalisha *kilograms* kama 1,200, lakini *NOSC* walivyochukua, wakaanza kupata *kilograms* 7,200. Kwa hiyo, ilikuwa wakulima wadogo wadogo wameanza kusimamiwa vizuri sana na kuleta maendeleo makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kutokana na muundo wa bodi ambao kazi yake hasa ni udhibiti na usimamizi, tunaona ingekuwa ngumu sana bodi kuweza kufanya kazi hiyo, ambayo ni majukumu ya kila siku. Kwa hiyo, tulikuwa tumependekeza kama Kamati kwamba, iundwe kurugenzi ambayo itasimamia kazi za kila siku za wakulima wadogo wadogo ambapo ile kurugenzi sasa itahakikisha wakulima wanakuwa na Maafisa Ugani wale wenye uelewa wa kilimo cha chai.

Mheshimiwa Naibu Spika, maana yake tumekuwa na Maafisa Ugani ambao hawana hata *knowledge* ya chai. Kwa hiyo, tunataka sasa Maafisa Ugani wawe kabisa wana uelewa mkubwa wa zao hili la chai.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tunaomba Mkurugenzi atakayeteuliwa kusimamia hii kurugenzi, awe kwanza na elimu ya kutosha, awe mbobevu, awe na uzoefu mkubwa wa zao hili la

chai, kwa sababu sasa hivi wakulima wanapata shida, hawana soko katika zao la chai. Nikichukulia tu mfano, hata pale Kilolo, wakulima wengi ni wazee. Vijana sasa hivi hawataki kulima chai kwa sababu kwanza hawaoni faida ya kulima chai, kwani hakuna soko lolote.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, Kilolo waliamua kutoa chai na kuweka tu parachichi ambayo ina faida, au kutoa chai na kuamua tuweke hata hii gobo tu ambayo kila siku tutapata faida.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaiomba Serikali sasa iwe na mkakati mahususi kuhakikisha zao la chai linasimamiwa kwa kiasi cha kutosha. Pia, ihakikishe kwamba hii kurugenzi sasa mitaji inapatikana au kama ni mikopo kwa hao wakulima wadogo wadogo, kwa sababu unaona karibu 50% wakulima wadogo ndio wanachangia katika kilimo cha chai. Pamoja na kuwa tuna kampuni kubwa zinalima, lakini bado wakulima wadogo ambao ndio wenye ardhi yao, na ambao ndio wako katika hilo eneo, wanafanya hiyo kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunapofanya marekebisho haya ya sheria, tunaomba Serikali ihakikishe sasa wakulima wadogo wa chai waweze kujengewa uwezo wa kuwa na *AMCOS,* kuwa na *SACCOS* ili hao wakulima wadogo waweze kuwa ndio wamiliki wa viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona zinakuja kampuni, za wawekezaji kutoka nje wanamiliki viwanda, na vinakufa, lakini wakulima wetu hawana pa kupeleka wala hawana soko la kupeleka chai. Tukiangalia tu mfano Sri Lanka, wakulima wadogo wana viwanda karibu 700, hapo Kenya wana viwanda karibu 90, na tukiangalia Rwanda wameanza juzi tu, sasa hivi wakulima wadogo wadogo ndiyo wanamiliki viwanda vinne.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamwomba kabisa Mheshimiwa Waziri wetu wa Kilimo, tunamwamini, ajenge uwezo wa wakulima wetu wamiliki hivi viwanda, ndiyo tutaweza kuendeleza zao la chai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuwepo na mkakati kuhakikisha viwanda vilivyofungwa, hasa vya wakulima, vinafufuliwa. Kwa mfano, Mufindi, kiwanda kimeshasimama. Ukienda Njombe kiwanda kimesimama, na Rungwe kiwanda kimesimama. Sasa wakulima wanapeleka wapi chai yao? Wakati tunaendelea na haya marekebisho, uwekwe mkakati halisi ambao utasababisha hivi viwanda viweze kufunguliwa na wakulima wa chai waweze kutendewa haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, ninaomba elimu itolewe. Sisi wenyewe Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Waziri amefanya kazi kubwa sana. Tulikuwa hatuelewi kwamba unapotoa wakala uweke bodi, inakuwaje? Je, wakulima itakuwaje? Ninaomba sasa Serikali iwe na mkakati, elimu itolewe kwa marekebisho ya Sheria hii ya Chai, wananchi waelewe kila kitu ili hii sheria iweze kufanya kazi vizuri na wahakikishe kwamba sasa chai inamsaidia mkulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bila kusahau Kiwanda cha Kilolo, jamani jengeni. Tumesubiria kwa muda mrefu. Hakuna hata faida waliyopata wananchi wa Kilolo kwenye chai wanayoilima.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuunga mkono Marekebisho ya Sheria yaliyotolewa na Serikali. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati. Nilimtaja Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud, atafuatiwa na Mheshimiwa Ramadhani Hamza Singano, na Mheshimiwa Balozi Dkt. Pindi Hazara Chana ajiandae.

**MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa nafasi. Kwanza nichukue nafasi hii kuipongeza Wizara yetu ya Kilimo, Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Naibu Katibu Mkuu, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii kwa ushirikiano wao wa karibu waliotupatia wakati wa kujadili Muswada huu. Ninawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakubaliana na mawazo na mapendekezo yote ya Kamati kwa sababu ni mawazo ambayo yamechambuliwa na kujadiliwa kwa kina karibu siku nane mfululizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninataka nijielekeze kwenye Sheria ya Tasnia ya Chai Sura 275. Tulikuwa na wakala wetu huu wa wakulima wadogo wadogo wa chai ambao sasa unavunjwa, na shughuli zao zinapelekwa moja kwa moja kwenye Bodi ya Chai. Wakulima wadogo wadogo ni watu ambao uwezo wao unakuwa mdogo pia ukilinganisha na wazalishaji wakubwa wa chai na wawekezaji wakubwa wa viwanda vya chai.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuwapeleka huko kwenye Bodi ya Chai, ninaendelea kuishauri Wizara na Serikali, ndani ya Bodi ya Chai, kuweko na kurugenzi ndogo ambayo kurugenzi hiyo itakuwa inafika moja kwa moja kwa wakulima wale wadogo wa chai, ambayo itasimamia kwa karibu sana shughuli zao za ukulima wa chai. Hiyo kurugenzi, huyo atakayepewa hiyo dhamana, awe na weledi na uelewa na ujuzi na utaalamu wa masuala ya chai na kuwasimamia wakulima wadogo wa chai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kurugenzi hiyo ambayo tunaitaka iwe karibu sana na kuwasaidia wakulima wadogo wa chai, tunaomba isaidie kuongeza uzalishaji wa chai, kuongeza kuzalisha kwa tija, kuongeza wigo wa kupanua masoko, kuwasaidia wakulima wadogo wa chai kupata utaalamu na huduma za ugani, kupata mitaji ya ndani na nje ya nchi katika kuendeleza sekta hii ya chai nchini Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, kuongeza msukumo wa kuanzisha viwanda vidogo vidogo vya wakulima wa chai hawa wadogo wadogo. Tukiongeza viwanda vidogo vidogo, tutaongeza wigo wa kutanua ajira ndani ya nchi yetu, na pia tutaongeza pato la Taifa katika Sekta hii ya Chai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninatoa mfano, nchi ya Sri Lanka ina zaidi ya viwanda 700 vidogo vidogo vya wakulima wa chai, kwa maana chai ina soko, lakini ni kulitafuta hilo soko na kulifanyia

kazi. Baada ya kuundwa hiyo kurugenzi, ninapendekeza mali, rasilimali ambazo zilikuwemo kwenye ule wakala, wapewe hiyo kurugenzi wazisimamie, zisichukuliwe na Bodi ya Chai kwa sababu zitakwenda kuongeza ufanisi katika shughuli zao. Wasiachwe yatima, wana mali zao, wapelekwe na mali zao na wazisimamie wao wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapendekeza, ninashauri, ninakubaliana na maoni ya Kamati kwamba Wajumbe wa Bodi watakaowawakilisha wakulima wadogo wa chai, wawe na ujuzi na wanaitambua hiyo sekta yenyewe ya chai ili akawasaidie kuwasemea hoja zao na shida zao ndani ya Bodi. Tunategemea kwamba, tukiiendeleza sekta hii, itaongeza pato la Taifa na wakulima wadogo nao wataendelea kupata tija kwa wanachokilima. Nia ni kuifufua Sekta hii ya Chai iweze kuongeza pato la Taifa katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nijielekeze kwenye Sura 251 kwenye Tasnia ya Sukari, hasa kwenye sehemu hii ya kufungasha upya sukari kwa gramu 100, zisizidi. Lengo hapa ni kuvilinda viwanda vya ndani. Kwa maana hiyo basi, tusiruhusu sukari nyingine ya namna yoyote itakayoingizwa kwenda kufanya vifungashio upya. Tuwaombe hawa wazalishaji wa ndani waongeze uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, katika hivyo vifungashio, *label* zao waweke imezalishwa wapi hiyo sukari; kampuni gani imefungasha; au ni mwekezaji gani wa ndani ameifungasha hiyo sukari yetu? Hili litasaidia sana kulinda soko letu dhidi ya sukari zinazoingizwa ambazo hazina viwango, ambazo zinakwenda kwa wananchi kuharibu afya zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwekezaji aeleze kwenye *label* yake, sukari imezalishwa wapi; na mfungashaji ni nani; au jina la kampuni iliyofungasha hiyo sukari. Lengo na madhumuni yetu kama nchi, au kama Taifa, ni kuhakikisha tunajitosheleza kwa sukari ndani ya nchi yetu. Kwa hiyo juhudi na msukumo wa uwekezaji katika Tasnia ya Sukari uko pale pale, na uendelee kutekelezwa vizuri tuweze kujitosheleza kwa sukari.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo makubwa ya kulima tunayo, uwezo wa mtaji na maji tunayo, *Alhamdulillah* na umwagiliaji huo Mheshimiwa Rais kawekeza sana kwenye sekta ya umwagiliaji. Tunamshukuru sana na tunaweza tukalima kwa kutumia umwagiliaji. Tunampongeza sana, kaleta mitambo ya kuchimba visima na mabwawa inayokwenda kilometa mbili kwenda chini. Kwa nini tusipate maji? Maji tutayapata tu na tutalima kwa umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninajielekeza kwenye kipengele hiki cha sukari ghafi. Sukari ghafi itakayoingizwa, watakaopewa kibali au ruhusa ya kuingiza hiyo sukari ghafi, ninasisitiza na mimi kama wenzangu, wawe na viwanda ndani ya nchi. Pia, siyo kuwa na viwanda tu, na ufuatiliaji wa karibu kuona hivyo viwanda kweli vinafanya kazi? Pia, isizalishwe sukari hiyo kwa matumizi mengine ambayo siyo ya kawaida, iende kwa matumizi hayo hayo ya viwandani yaliyokusudiwa, na siyo matumizi mengine, na siyo vinginevyo. Vilevile, ukaguzi wa mara kwa mara kuwafuatilia hao, ufanyike.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna taasisi zetu muhimu sana *TBS, COPRA* na stakabadhi za ghala. Kumekuwa na uingiliano wa majukumu katika kufuatilia au kutoa na kuingiza mazao ya chakula. Taasisi zetu ni muhimu na tunazihitaji sana na ninasisitiza kwamba ziangaliwe zile sheria ili kila mtu afanye majukumu yake na kila mtu awe na mipaka yake bila kuingiliana na kuleta sintofahamu. Lengo ni kuwasaidia Watanzania. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Khadija, ahsante sana.

**MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninamalizia kwa kuunga mkono hoja na ninakushukuru sana kwa nafasi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud, ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Ramadhani Hamza Singano,

atafuatiwa na Mheshimiwa Balozi Dkt. Pindi Hazara Chana, Mheshimiwa Dickson Lutevele Villa, ajiandae.

Mheshimiwa Singano hayupo, Mheshimiwa Balozi, Pindi Chana.

**MHE. DKT. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kumpongeza sana Mheshimiwa Deogratius Ndejembi kwa uteuzi huu muhimu ambao ameupata. Kwa kweli ni Mbunge mwenzetu tunachapa naye kazi na tutahakikisha tunampa ushirikiano wa kutosha, pongezi nyingi sana kwa Mheshimiwa Ndejembi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya utangulizi huu, ninaomba kusema kwamba, ninaunga mkono hoja hii muhimu ambayo imeletwa hapa na Mheshimiwa Waziri, kaka yangu Waziri wa Kilimo hongera sana kwa kutuletea marekebisho ya Sheria takribani nne: Sheria ya Usalama wa Chakula, Sheria ya Tasnia ya Mkonge, Sheria ya Tasnia ya Sukari na Sheria ya Chai.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitachangia upande wa kisheria kama *learned sister,* kwanza kwenye tafsiri wameongeza tafsiri ya neno *other produce* na kujumuisha zao la pareto. Hili ni jambo la msingi sana kuliweka zao la pareto. Ninakumbuka miaka ya nyuma nimelima pareto, nimechuma pareto katika Kijiji cha Manga huko Ludewa na tulikuwa tunakausha pareto miaka hiyo pale kwenye mafiga, unaweka juu inakauka, ikishakauka ndiyo mnapeleka kiwandani. Kwa hiyo, leo hii kurudisha nguvu na heshima ya zao la pareto kwa kweli ninafurahi sana na kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kifungu cha 4 cha Muswada, ukurasa wa nne (4), ule Muswada ambao ulikuwa *submitted* Bungeni hapa. Kuna Kifungu kinaeleza vizuri kabisa, Kifungu cha 4 ambapo kinasema kwamba: "Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko" kuleta majukumu yaliyokuwa yanatekelezwa na Bodi ya Pareto Tanzania, kuna *amendment.*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa tumeongeza majukumu yaliyokuwa yanatekelezwa na Bodi ya Pareto, nikasema hii haitakuwa *duplication* kama Bodi ya Pareto ilikuwa inafanya majukumu haya? Sasa majukumu haya yameletwa hapa katika *amendment section four,* lakini hapa inasomeka kama Kifungu cha 5 *"The Principal Act is Amended on Section Four"* na kuweka hayo majukumu yaliyokuwa yanatekelezwa. Kwa hiyo, nimehoji tu *is this not duplication?* Kule ambako majukumu yalikuwa yanafanywa awali ya pareto yataendelea ku-*exist* au hayata-*exist?*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine *amendment on section six,* hapa awali kulikuwa kuna neno *arbitrate* na sasa tunatoa *arbitration* na kuweka *resolve disputes*. Lazima tujue neno *arbitration* lina maana gani na ku-*resolve disputes* maana yake nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, unapozungumza *arbitration* ni *alternative dispute resolution* ambapo anahusika mtu wa tatu kutatua hilo tatizo, lakini sasa tumesema badala ya ku-*arbitrate* tuta-*resolve disputes,* ndani ya ku-*resolve disputes* kuna masuala ya *negotiations, mediation, court litigations* lakini pia *arbitration* nayo ni *subset* ya ku-*resolve disputes* kwa hiyo, hili ni jambo jema na naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukija *amendment* ya *section eleven* na *section twelve* kwa mujibu wa Muswada pale tumeeleza wazi kabisa kwamba sasa neno 'Bodi' linaondoka na kwa niaba ya neno "Bodi" kutakuwa na neno *'authority'*. Kwa hiyo nikasema tungeweza kuchanganya katika Muswada, Kifungu cha 7 na Kifungu cha 8 na tukasema *in sub section 7 and 8 by deleting the word Body wherever it appears, wherever it appears and substituting for it the word authority*.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hapa wataalamu wametuletea Kifungu cha 7, wamekieleza na Kifungu cha 8. Kwa hiyo wakati mwingine tunaweza tukapunguza maneno na kusema tu *wherever it appears,* lakini ni jambo zuri. Ninaunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine *amendment on section nineteen,* zamani kulikuwa hakuna rufaa katika ile sheria ya zamani. Inasema tu mtu anayetaka ku-*export* mazao au ku-*import* itabidi aombe kibali, lakini hapo wamesema endapo hajapata kibali sasa kuna uwezo wa mwananchi kukata rufaa kwa *Minister,* hiki ni Kifungu kipya. Kwa hiyo, nimpongeze Waziri, Kifungu hiki cha kukata rufaa kwa *Minister* ni jambo zuri na ni jambo ambalo linaleta maendeleo ya Muswada huu wa masuala ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni kifungu cha 10 ambacho ni *amendment of sub section 21,* pale tumesema *relevant authority* inasimama badala ya *Minister* na inasema kwamba *substituting them for the words may be determined by the relevant authority.*

Mheshimiwa Naibu Spika, zamani Waziri alikuwa ndiye mwenye mamlaka ya kupanga posho za Bodi, lakini sasa badala ya Waziri atakuwa *relevant authority* ambaye *relevant authority* ni *Treasury Registrar,* sasa mimi nasema ni vema tukasema kabisa ni *Treasury Registrar* kuliko *relevant authority.*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiweka *relevant authority* maana yake lazima kwenye *definition clause* tuonyeshe *relevant authority.* Nilipokwenda kwenye *definition clause* sijaona *definition* ya *relevant authority.* Kwa hiyo, tunaweza tukaweka *Treasury Registrar* au kama tutakubali tuweke *relevant authority, then we have to define the meaning of relevant authority.*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine hapa kifungu cha 12 ambacho ni *amendment* ya *section 31A,* hapa tumeongeza kifungu cha 33A ambacho kinasema *duty to ensure food security at family level.* Sasa hapa tumeeleza kwamba halmashauri inaweza ikaweka *bylaw* labda isiuze mazao nje au wananchi wasipike pombe, watunze mazao kama mahindi kwa ajili ya chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tumeeleza nini kinaweza kufanywa lakini *marginal note* inasema *duty to ensure food security*. Ningeomba wanasheria pamoja na kuelezea kila *duty put A, putting in place mechanism; B, making procedure; C, determine modality*. Tuweke Kifungu kingine ambacho hata kama hatujaonyesha *lists* hapa, kile Kifungu kitakata *for*. Kwa hiyo tunaweza kuongeza *performing any other activity to ensure food security at household level is maintained.*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati ninamalizia muda wangu, kifungu cha mwisho ni *amendment* ya kifungu cha 39A. Kifungu hiki ni kipya, kinasema kwamba kuna uwezekano wa kuwatoza faini watu wanaofanya makosa kwa mujibu wa sheria hii: "*Where the Director General compound an offence under this section, the person concerned shall not be liable to any prosecution in respect of such offence, and if any such prosecution is brought in the court, it shall be a good defence for such person to prove that such offence has been compounded under this section*".

Mheshimiwa Naibu Spika, yaani kuna makosa ambayo wanaweza kutoza faini na kosa hilo likitozwa faini likienda Mahakamani, Mahakama haiwezi ikamuadhibu huyu mtu kwa sababu ameshatozwa faini. Hapa nina maswali *what if* hili kosa ni kubwa na labda linahitaji *imprisonment,* huyu *director* hawezi kufanya *imprisonment* na B yake inawezekana mbele ya safari kisije kikatumika na watu watundu kujificha kwenye kichaka anajiona ana kosa kubwa la mazao. Amechukua mazao ambayo hayapaswi, anasema ninaomba nitozwe faini, kumbe anakwepa kwenda kuitika Mahakamani, kwa sababu anajua akishatozwa faini akienda Mahakamani ataonyesha *evidence,* nimeshatoza faini, lakini kumbe lile kosa kwa jinsi ya ukubwa wake, kuna *imprisonment*. Kwa hiyo, ninaomba kidogo ufafanuzi wa eneo hili *otherwise* ni sheria nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Balozi Dkt. Pindi Hazara Chana ahsante sana. Nilimwita Mheshimiwa Dickson Lutevele Villa

atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Regina Christopher Malima na Mheshimiwa Sigrada Wilhem Mligo ajiandae.

**MHE. DICKSON N. LUTEVELE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia marekebisho ya Muswada wa Sheria ya Pareto, Chai pamoja na Sukari. Kwanza kabisa, ninaomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi ya kuingia tena katika kikao hiki cha Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba niseme kwamba kwanza ninaunga mkono hoja ya mabadiliko ya sheria hii ambayo imeletwa mezani, lakini kama ambavyo wasilisho la Kamati limesema na maeneo ambayo Kamati inaona ni muhimu, ni vizuri Serikali ikatilia mkazo. Ninaomba nioneshe maeneo ambayo pengine tukiyajua majukumu yaliyokuwa majukumu ya wakala wa chai na haya ambayo yanahamishiwa kwa Bodi tutakuwa tuko kwenye eneo zuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza wakala wa chai, Wakala wa Maendeleo ya Wakulima wa Chai *(TSHTDA)* ilianzishwa kwa sheria Na. 3, sheria ambayo ilianza mwaka 1997, lakini yapo majukumu ambayo yameainishwa kwenye sheria hiyo nayo ni kama yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu la kwanza, lilikuwa ni kutoa huduma za ugani; jukumu la pili, lilikuwa ni kuhamasisha kusimamia vikundi vya ushirika *(AMCOS)* na jukumu la tatu, lilikuwa ni upatikanaji wa pembejeo za kilimo. Hii wakala ilikuwa inahakikisha kwamba wakulima wadogo wadogo wanapata pembejeo za kilimo. Jukumu la nne, lilikuwa ni kulinda maslahi ya wakulima katika masoko na bei na jukumu la tano lilikuwa ni kuendeleza miundombinu ya chai viwandani.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa wakala hii pamoja na kusuasua kwa zao la chai, ziko faida ambazo wakala imeleta ikiwemo kuwaunganisha wakulima wadogo wadogo ambao tangu mwaka 1997 ilipoanzishwa wakala hii mpaka sasa tunaona

wakulima takribani 32,000 wameunganishwa na wameendelea kunufaika na mambo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunaona pia kwamba wakala na yenyewe ilikuwa ikifanya kazi kubwa, lakini pia imesaidia sana kuhakikisha yale mashamba yaliyokuwa yametelekezwa yanafufuliwa. Kwa hiyo, tunaona kwamba wakala ilikuwa na kazi ambayo ilikuwa inafanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukichukua kazi ambayo wakala ilikuwa inafanya na ukachukua majukumu ambayo yameainishwa kikatiba, majukumu ya Bodi, unaona iko haja ya kuunga mkono hoja ya Mjumbe aliyepita kwamba pamoja na nia nzuri ya Serikali ya kuhamishia majukumu ya wakala kwenda kwa Bodi, lazima iundwe kurugenzi, kurugenzi itakayoshughulika moja kwa moja na wakulima wadogo wadogo mashambani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu kisheria Bodi ya Chai imepewa majukumu yake ambayo jukumu la kwanza kabisa ilikuwa ni ushauri na uwakilishi Serikalini; jukumu la pili la Bodi ni udhibiti wa soko na biashara; jukumu la tatu la Bodi ni usimamizi wa ubora na usindikaji; jukumu la nne ni ulinzi wa maslahi ya wakulima na wadau wa wakulima hasa wadogo wadogo na jukumu la tano ni takwimu na utafiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kama majukumu haya ya wakala yakihamishiwa kwenye Bodi na kisianzishwe chombo kingine ambacho kitashughulika na shughuli za kila siku za wakulima wadogo wadogo unaona kabisa wakulima wadogo wadogo wanakwenda kupotea na badala yake watabaki wakulima wakubwa wakubwa ambao Bodi ilikuwa inashughulika nao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nini ushauri wangu? Ninaishauri Serikali kupitia Wizara kwamba, ni kweli kwamba kama tunahamishia majukumu haya kwa Bodi ni lazima na ni takwa la muhimu kuanzisha kurugenzi itakayosimamia, kurugenzi itakayoundwa na wataalamu wa chai, lakini wale ambao wako tayari kwenda *site*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu wakulima wadogo wadogo wanayo mahitaji ya kila siku, wanayo mahitaji ya huduma za kiugani ambazo Bodi inaweza ikawa na wataalamu wa huduma za kiugani kwa ujumla, lakini kikiundwa chombo maalum kwa ajili ya wakulima wadogo wadogo tafsiri yake tutapata wataalamu waliobobea kwenye mazao ya chai. Kwa hiyo, ninaunga mkono hoja ya Wizara, lakini ninapendekeza kwamba lazima iundwe kurugenzi itakayoshughulika na maisha ya kila siku ya wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi nyingine ambayo ilikuwa ikifanywa na hii wakala ni kuwatafutia wakulima wadogo wadogo wawezeshaji, taasisi mbalimbali za kuwawezesha wakulima wadogo wadogo ambao kwa mujibu wa taratibu mara nyingi taasisi hizi zinajikita zaidi kuwasaidia wakulima wadogo wadogo wale *individuals* ama zile *AMCOS*.

Mheshimiwa Naibu Spika, *regulation* zao haziko kusaidia Bodi. Kwa hivyo sasa kwenye kumbukumbu ziko huku, ulikuwepo zamani Mfuko ambao ulikuwa unaitwa Wakfu, Mfuko huu ulikuwa unawasaidia wakulima na baadaye ukaja ukatolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaishauri Wizara kwamba pamoja na nia nzuri, lazima wahakikishe wanaanzisha mfuko wa wakulima wadogo wadogo utakaowawezesha kwa sababu baada ya majukumu ya wakala kuchukuliwa na Bodi, tayari wale wawezeshaji waliokuwa wanawawezesha wakiwa wakulima wadogo wadogo hawatakuwa tayari kuiwezesha Bodi ambayo inasimamiwa na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, lazima tuanzishe chombo ambacho kitawasaidia hawa wakulima wadogo wadogo pindi wanapokuwa wana mahitaji hasa ya fedha waweze kuchukua kutoka kwenye chombo hicho, ambacho zamani walikuwa na chombo chao kilikuwa kinaitwa Wakfu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninatambua nia nzuri ya Serikali, lakini pamoja na maboresho ambayo yanafanyika tunashauri, kwa mfano, ninatoka Wilaya ya Mufindi. Viwanda vya Mufindi

vimekufa, vimechoka, havifanyi kazi, wakulima wa chai Mufindi wanalalamika sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nia ya Serikali ni njema, lakini ninaishauri sana Serikali, ihakikishe viwanda vinafufuliwa kupitia hiyo Bodi kwa sababu, kama hatutakuwa na mlengo wa kufufua viwanda wakulima wetu wa Wilaya ya Mufindi, Wilaya ya Kilolo pamoja na Njombe hawataona mabadiliko kati ya wakala na huduma zinazotolewa na Bodi na tutakuwa tunafanya *the same thing* ama nitumie lugha ambayo imezoeleka itakuwa ni *white elephant*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunategemea kwamba hiki ambacho Wizara imekuja nacho utakuwa ni mpango bora na kabambe wa kuwawezesha wakulima hasa kuhakikisha wanalipwa malipo yao, chai yao inaendelezwa na mashamba ya chai yanaendelezwa. Tusipofanya hivyo mashamba ya chai ambayo yamechukua eneo kubwa sana katika Wilaya yetu ya Mufindi yanakwenda kupotea na kuwa vichaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maneno hayo, ninapenda kusema kwamba, ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Dkt. Regina Christopher Malima, atafuatiwa na Mheshimiwa Sigrada Wilhem Mligo na Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle ajiandae.

**MHE. DKT. REGINA C. MALIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nishukuru kwa kunipatia nafasi ili niweze kuchangia machache katika Muswada huu muhimu ambao umewasilishwa na viongozi wetu. Kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupatia nafasi ya uhai na sote kuwepo mahali hapa ili tuweze kujadili Muswada huu muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kuipongeza Wizara kwa sababu Muswada huu unalenga kuimarisha udhibiti, usimamizi na maendeleo ya sekta ya kilimo sambamba na Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2050.

Mheshimiwa Naibu Spika, maendeleo ya sekta ya kilimo si kuangalia taasisi pekee. Kuangalia taasisi ni jambo zuri sana, lakini suala lingine ni kumwangalia huyu mkulima je, yupo katika mfumo huu? Kwa maana hiyo, pamoja na kupongeza Muswada huu na kwamba umeletwa kwa muda muafaka, nina mambo mawili ya kushauri katika Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama wenzetu wataridhia basi ni vizuri kuangalia kuhusu uwakilishi wa mkulima. Kifungu cha 35(b)(1) kinachorekebisha *paragraph* ya 2(1) ya *schedule* ya Sheria ya Tasnia ya Chai. Muswada huu unapendekeza muundo mpya wa Bodi ya Chai na kutaja uwakilishi wa taasisi mbalimbali zinazohusika na utafiti wa kilimo na Serikali za Mitaa, lakini haujaweka wazi mwakilishi wa wakulima wadogo wa chai katika bodi kama chombo kikuu cha maamuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu kuu ni kwamba, katika mfumo huu ni vizuri kukawa na mwakilishi wa wakulima wadogo wa chai katika bodi ambao na wao watakuwa katika *decision making process* zote ambazo zitakuwepo. Hii itasaidia kuongeza tija kwa wakulima wetu ambao na wao wamekuwa ni sehemu kubwa ya masuala ya kilimo katika Taifa letu. Kwa maana hiyo, ninaendelea kushauri ili waone namna bora ya kuangalia katika kipengele hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho Taifa letu linategemea kilimo kwa asilimia kubwa na vijana wa Taifa hili ni sehemu ya nguvu kazi katika masuala ya kilimo. Muswada huu haujaainisha popote masuala ya vijana kama kundi mahsusi katika mnyororo mzima wa kilimo katika Taifa letu. Niombe suala la vijana katika mambo mbalimbali yanayohusu Taifa hili ni vizuri sasa yakawa yanapewa jicho la pekee, ili wao pia wawe ni sehemu katika masuala ya uzalishaji na masuala mbalimbali ambayo yanahusiana na kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hivyo ya kwangu yalikuwa ni hayo mawili. Uwakilishi wa wakulima katika bodi pia suala la vijana. Muswada huu uhakikishe kabisa kuna

jicho ambalo linamwangalia kijana kama mtendaji mkuu katika masuala mazima ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hivyo, ninaunga mkono hoja na ninaomba kuwasilisha. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Sigrada Wilhem Mligo, atafuatiwa na Mheshimiwa Edwin Enossy Swalle na Mheshimiwa Lutengano George Warioba ajiandae.

**MHE. SIGRADA W. MLIGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia sekta hii muhimu. Ni ukweli usiopingika kwamba, zaidi ya 70% ya wananchi wa nchi hii ya Tanzania ni wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitajikita kwenye mambo manne ya msingi. Jambo la kwanza, tunapojadili sheria hizi zinazohusu mambo ya kilimo hatuwezi kuacha kuzungumzia *issue* ya ruzuku. Hatuwezi kuacha kuzungumzia *issue* ya bei elekezi za mbolea. Hatuwezi kuacha kuzungumzia majukumu ya Serikali kwa wananchi kwenye mchakato wa ruzuku ya mambo ya mbolea.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka ninavyozungumza hivi sasa Serikali ya Chama Cha Mapinduzi inadaiwa zaidi ya shilingi 40,000,000,000 kwenye ruzuku ambazo makampuni na wafanyabiashara wa mbolea na mawakala wanaidai Serikali hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka ninavyozungumza sasa kuna viwanda vya mbolea vimefungwa zaidi ya miezi minne ikiwemo Kiwanda cha Mbolea cha Minjingu kwa sababu kinaidai Serikali fedha za ruzuku, kimeshindwa kuendesha kiwanda kile kwa ajili ya kuendelea ku-*produce* mbolea nyingine mpaka ninavyozungumza hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka ninavyozungumza sasa bei elekezi ya mbolea ni shilingi 80,000, lakini sasa mbolea inauzwa shilingi 135,000. Kwa nini mbolea inauzwa shilingi 135,000? Changamoto ni kwamba wale mawakala wanapata wakati

mgumu wa kuendesha biashara ya usambazaji wa mbolea, lakini…

**MHE. PHILLIPO A. MULUGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu.

**MHE. SIGRADA W. MLIGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, pia malalamiko yao ni kwamba, bei elekezi haijahusisha wadau na haiendani na kiwango ambacho Serikali imepanga.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sigrada, kuna Mheshimiwa…

**KUHUSU UTARATIBU**

**MHE. PHILLIPO A. MULUGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu. Nilikuwa ninamwomba Mheshimiwa mchangiaji asogeze *microphone* kidogo, ili angalau sauti itoke vizuri, masikio yanauma. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sigrada endelea na mchango wako.

**MHE. SIGRADA W. MLIGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Mpaka ninavyozungumza sasa mbolea ya kupandia ni shilingi 135,000, lakini mwongozo wa *TFRA* ni shilingi 80,000. Malalamiko ya wale wasambazaji wa mbolea wanadai gharama za usambazaji wa mbolea ni kubwa, pia hawana fedha za uendeshaji kwa sababu wanaidai Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, migogoro kati ya wawekezaji, wakulima na wafanyakazi. Mfano mzuri ni Mkoa wa Njombe. Mkoa wa Njombe ni miongoni wa mikoa ambayo kuna zao la chai. Waziri wa Kilimo yupo hapa anajua changamoto ambayo Njombe inakutana nayo. Mpaka ninavyozungumza hivi mwekezaji anayeitwa *DL* amewafukuza wafanyakazi walioita waandishi wa habari kwa ajili ya kulalamikia madai yao ambayo hawajalipwa kwa miaka nane mpaka sasa. Amewafukuza kazi wote na ushahidi ninao.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuwezi kuacha kujadili vitu vya msingi kama hivi, lakini huyu mwekezaji ni mtu ambaye ameua viwanda vyake vyote vya chai katika Mkoa wa Njombe ikiwemo Lupembe, Luponde na kwenye Jimbo la Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, atakuwa shahidi yangu namba moja. Pia, kila anayepambana kuhakikisha jambo hili linakaa; nimeshangaa sana leo nilikuwa ninasoma mwongozo wa mbolea nimekuta kuna bodi, sekretarieti za mikoa, Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kama hizi taasisi zipo na zinalipwa fedha ya wananchi hawa, hii migogoro inakosaje suluhisho. Mgogoro ambao hadi Rais mwenyewe alikuja kutoa maelekezo wakati wa kampeni mwaka jana, hakuna anayetekeleza. Kuna nini nyuma ya huyu Mwekezaji *DL?* Amepewa fedha na Serikali, amedhaminiwa Benki ya *CRDB,* amepeleka kwenye viwanda vyake vya Kenya, vya Njombe vimekufa. Kwa nini, Serikali inakuwa kimya dhidi ya huyu mwekezaji kama siyo na yenyewe ipo nyuma? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni Serikali kuchelewesha fedha ya waliopeleka mazao ya mahindi Serikalini.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**MHE. SIGRADA W. MLIGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, *NFRA* inakusanya mahindi ya wakulima wa nchi hii, lakini hii *NFRA* inakaa zaidi ya miaka miwili au mwaka mmoja na nusu haijawalipa. Mpaka watu wanaingia kwenye hatua ya kulima mahindi waliikopesha Serikali haijawalipa, mpaka ninavyozungumza hapa Nyanda za juu Kusini kama Songea, Njombe na Ruvuma kuna wakulima wanaidai Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa, tunavyozungumza sheria muhimu kama hizi hatuwezi kuacha kuzungumzia vitu muhimu kama hivi, lakini cha ajabu zaidi huu mchakato *serious* wa ruzuku mpaka ninavyozungumza hivi hauna sheria. Ndiyo maana wanaodai ruzuku Serikalini, wanadai kwa kupiga simu. Watampigia simu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Chongolo, sijui

watampigia simu Mbunge hawana sheria maalum inayowaongoza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisoma huu mwongozo unasema; msambazaji wa mbolea akishasambaza atatuma taarifa kwa hawa watu wa *TFRA*. *TFRA* wanatakiwa kufanya malipo ndani ya siku 14. Ninapozungumza hivi kuna wasambazaji wa mbolea wa 2021 hawajalipwa, lakini mwongozo unasema wanatakiwa walipwe ndani ya siku 14. Huo ndiyo ukweli, kama mimi ni mwongo wanipige taarifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaendelea jambo lingine…

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**MHE. SIGRADA W. MLIGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ninaweza kuzungumza, Wizara nyeti kama hii ambayo inagusa maisha ya wananchi, tunaomba itengenezwe sheria inayomruhusu huyu msambazaji wa mbolea iwe ni kampuni au binafsi, inayowaongoza wakicheleweshewa malipo yao Serikali watachukua hatua gani na siyo kubaki kwenye mwongozo ambao siyo msingi wa kisheria. Huyu msambazaji hata akicheleweshewa fedha zake miaka mitatu, hana sheria maalum inayompa uhuru wa nini akifanye zaidi wanaishia kuwapigia simu Mawaziri, Naibu Mawaziri, Wabunge, Wakuu wa Mikoa na wao hawana kauli thabiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni yangu yalikuwa ni hayo kwa leo ninaomba Wizara ya Kilimo ikae, ione namna gani ita-*deal* na wawekezaji ambao wameshafilisika, hawawezi tena kufufua viwanda, walete wawekezaji wengine *especially* huyu *DL*, Mwekezaji wa Njombe. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Edwin Enossy Swalle, atafuatiwa na Mheshimiwa Lutengano George Mwalwiba, mtoa hoja ajiandae.

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na ninaomba niungane na Wabunge wenzangu wa Kamati ya Kilimo kuchangia Muswada huu muhimu sana mchana huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama hapa kuongea mambo matatu. Jambo la kwanza, nimesimama kupongeza kazi nzuri sana inayofanywa na Serikali kupitia Wizara ya Kilimo. Pili, nimesimama kueleza changamoto kubwa ya sekta ya chai nchini. Tatu, mapendekezo ambayo ninayo kwenye Muswada ambao umeletwa hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, kaka yangu Daniel Godfrey Chongolo na Naibu Waziri wake Mheshimiwa Silinde. Sisi kama wakulima wa chai na wakulima kwa ujumla tulishukuru kuhusu huu Muswada ambao umeletwa hapa leo. Wakati tumesikia kwamba, kuna Muswada unarekebisha Tasnia ya Chai, kwa sababu mwezi Juni ndani ya Bunge, Wabunge tuliongea sana kuhusu kero za chai, tulikuwa na hamu ya kuona majibu pengine ya kutibu changamoto ya chai nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri Chongolo anajua vizuri sana. Nimpongeze kwamba ameanza kuchukua hatua tangu ameingia kwenye hii Wizara. Changamoto kubwa ambayo ipo kwa wakulima katika sekta ya chai; kwanza, ni masoko ambayo ni shida kubwa sana. Wanachuma chai kwenye mvua nyingi lakini hawalipwi kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, masoko ya kulipa chai ni changamoto, mashamba mengi yametelekezwa porini, wananchi wamekata tamaa sana. Sasa wakati ninatazama huu Muswada ambao umeletwa hapa, ambao unapendekeza Wakala wa Wakulima wadogo wa chai afutwe ibaki Bodi ya Chai peke yake, nilikuwa ninajiuliza je, huku ndiyo kujibu matatizo ya wakulima wa chai nchini? Majibu ya swali hili ni kwamba, hapana. Kinachopendekezwa hapa siyo kujibu kero ya wakulima wa chai nchini. Kwa unyenyekevu mkubwa sana Bodi ya Chai ni *regulator* siyo mtetezi wa wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mtetezi wa wakulima nchini; na watu wafahamu historia, zamani zao la chai lilikuwa ni zao la uchumi wa kikoloni. Wakulima wadogo wamewezeshwa na huyu wakala wapate uwezo na wao kuwa na mashamba yao ya chai. Kwa hiyo, kumweka mkulima mdogo na hawa *cartels* katika kapu moja haiwezi kuwa sawasawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, pamoja na kwamba ninapongeza kazi nzuri ya Serikali na ninapongeza mahsusi kwa sababu Mheshimiwa Waziri wa Kilimo nimeambiwa alikuwa msikivu sana kwenye Kamati na kukubali ushauri wa Kamati ya Kilimo. Hapa nimpongeze Mheshimiwa Deo Mwanyika, Mbunge wa Njombe Mjini kwa kazi kubwa ambayo amefanya kwenye hiyo Kamati yao ya Kilimo kwamba, wamesimama kama Wabunge kuhakikisha kwamba mkulima wa Tanzania anapata mtetezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wasiwasi wangu kwa sababu wamependekeza na Wizara imekubali kwamba, ataanzishwa Mkurugenzi kwa maana ya kurugenzi ndani ya Bodi ya Chai, mimi wasiwasi wangu hii kurugenzi haitakwenda kufanya kazi, itawekwa hapo itaenda kufia huko. Kwa hiyo, nina mapendekezo pamoja na kwamba nia ni njema na ninaunga mkono jambo hili. Mambo matatu ninaomba kwenye hii Kurugenzi ya Bodi ya Chai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, moja; ninaunga mkono Kamati kwamba, Mkurugenzi huyu apatikane mwenye sifa, lakini nyongeza ni kwamba apatikane kwa ushindani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili; kwa sababu Serikali imeahidi kwenda kuandaa kanuni za namna kurugenzi itafanya kazi ya kutetea wakulima, ninapendekeza; hizo kanuni ziainishe pia *source of funds* za kuisaidia hii kurugenzi. Tukimwacha huyu Mkurugenzi kuwa chini ya bodi atakwenda kufia pale atakuwa anashinda ofisini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri wa Kilimo kwa unyenyekevu mkubwa sana kwa kuwa amebeba

matumaini ya wakulima wa chai mabegani mwake, ninaomba Katibu Mkuu pamoja na Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Chai, jambo hili kwa kuwa wamelikubali lisiwe limekubaliwa ili kusudi tuweze kumaliza. Likubaliwe na likafanyiwe kazi ili hii kurugenzi ifanye kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu; ninataka nitoe ushauri wa jumla kwa Mheshimiwa Waziri, kule kwenye zao la chai wakulima wanahangaika sana juu ya upatikanaji wa fedha. Juzi kule kwangu Lupembe mfano, wamejitokeza watu wenye viwanda wanawakopesha wakulima fedha wakasafishe mashamba. Ninaunga mkono sana hoja ambayo imesemwa na Mheshimiwa Vila kwamba ni muhimu sana hii kurugenzi ikapewa *source of funds;* mfuko maalum wa kusaidia wakulima wadogo wa chai nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine kwa kuwa lengo ni kusaidia zao la chai na tumeona wawekezaji wengi hawana uwezo, changamoto kubwa ni utitiri wa kodi na ushuru. Nimwombe Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, wakae ofisini waangalie namna ya kuondoa ushuru usio wa lazima kwenye sekta ya chai. Tuwasaidie wawekezaji wa kilimo hiki kwenye chai wapate uwezo wa kufanya biashara kuwasaidia wakulima wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ningeomba pia ziwekwe *incentives* maalum kwenye hili zao kwa sababu ni ukweli ambao upo wazi kwamba, zao la chai ni kati ya mazao yaliyo taabani hapa nchini. Kwa hiyo, Wizara hii wakatafute *mechanism* maalum ya kuweka *special incentives* kwa wawekezaji wa zao la chai nchini, watakuwa wametusaidia sana watu wa kilimo cha chai hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo kwa mchana huu, ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge kwa mujibu wa Kanuni 36(2) ninaongeza muda tumalize shughuli iliyopo mbele yetu. Ninamwita Mheshimiwa Lutengano George

Mwalwiba atafuatiwa na Mtoa hoja, Mheshimiwa Waziri wa Kilimo.

**MHE. LUTENGANO G. MWALWIBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia eneo hili muhimu sana ambalo limeletwa na Muswada wa Mabadiliko ya Sheria hasa katika Tasnia ya Chai. Nitaongelea mabadiliko yanayoelezewa katika Sheria Na. 275. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri na timu yao yote kwa kuleta mabadiliko haya ambayo ninaamini wameyachakata na kuona lipo jambo ambalo linaweza likaleta tija katika sekta ya chai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuelezea kwamba, haya mabadiliko ya sheria ambayo yameletwa mbele yetu lengo ni kuinua sekta ya chai, ili kuweza kuboresha maisha ya wakulima wa chai katika maeneo wanayotoka wakulima wa chai, lakini kuweza kuongeza mchango wa chai katika pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi hali iliyopo ni kwamba pamoja na nia njema ya kuleta hizi sheria, bado hali ya zao la chai nchini siyo nzuri. Kwa hiyo, ndiyo maana ninaunga mkono mawazo yaliyoletwa na Mheshimiwa Mtoa hoja, pia ninaunga mkono mawazo mazuri yaliyoletwa na wenzetu wa Kamati ya Kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini ninaunga mkono? Ni kweli wamependekeza vizuri katika sheria hii kama kweli wanakwenda kufuta Wakala wa Maendeleo ya Wakulima Wadogo wa Chai Tanzania, lakini basi kuwe na *directorate* maalum ndani ya Bodi ya Chai ambayo itashughulika mahsusi na wakulima wadogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaposema hivi wala hatuna shaka na hatuna wasiwasi na utendaji wa Bodi ya Chai. Bodi ya Chai yapo mambo ambayo wanayafanya vizuri wanayasimamia. Tunadhani Bodi ya Chai wanalo jukumu la msingi la kufanya

udhibiti ambapo ni kuhakikisha bado pia tunaendelea kupata faida ya kushughulikia masuala na matatizo yaliyopo katika Tasnia ya Chai.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachopenda kushauri hapa, tutakapoanzisha hiyo *directorate* chini ya Bodi ya Chai, ninaomba sana kwamba tuone umuhimu wa sasa, hivi viwanda visimamiwe na wakulima wadogo wenyewe siyo hawa wawekezaji. Tuweke nguvu; wamesema kwamba lengo la kuanzisha ni kupunguza gharama ya uendeshaji, lakini kuongeza ufanisi wa kusimamia wakulima wadogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba sana sasa hivi tujitahidi kuona kwamba hivi viwanda vinasimamiwa na wakulima wadogo wenyewe. Hawa wawekezaji kama wafanyabiashara wanayo maslahi yao ya kibiashara. Ndiyo maana tumeona baadhi ya maeneo mengine wanatelekeza mashamba ya chai. Yale mashamba ya chai yakitelekezwa hasara inakuja kwa wakulima wa chai na hawa wakulima wadogo wadogo. Leo tukipeleka nguvu ya kuwasaidia na kuwadhamini wakulima wadogo wadogo. Ninayo hakika kwamba viwanda hivi vinawezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wasemaji waliotangulia wamesema. Tumeona katika Nchi ya Kenya, tumeona wenzetu wa Uganda, tumeona wenzetu wa Sri Lanka. Mafanikio makubwa ambayo viwanda viko chini ya wakulima wadogo jinsi ambavyo wanapata faida na tija kubwa ya kuendelea mbele na kusimamia tasnia hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu kimsingi katika eneo hilo, ninaomba tuachane na biashara ya kuuza majani mabichi, haitatutoa hapa tulipo. Sasa hivi tuanze kufikiria kuchakata chai na kuuza chai iliyosindikwa. Hivyo ndivyo itakuwa tumemkomboa mkulima mdogo wa Tanzania pamoja na wakulima wote wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, sina shaka na Mheshimiwa Waziri, yeye ni mtoto wa wakulima wa chai. Amesomeshwa na chai,

anajua zao la chai, tungefanya kitu kipindi hiki. Ninaamini imani kubwa ambayo Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amekupa, ninafikiri kipindi chako ni kipindi ambacho tunataka kuona jambo linafanyika katika eneo hili la sekta ya chai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi ninavyozungumza, viwanda kwa sehemu kubwa karibu nchi nzima vimekufa. Hawa watu hata tukisema tunaenda kuongeza tija, tunaenda kuongeza huduma za ugani, lakini hawana soko la uhakika kwa sababu viwanda vimekufa. Viwanda kule Rungwe Mwakaleli, viwanda kule Rungwe *WATCO* pale mjini, lakini mashamba yametelekezwa kule Msekela.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii yote tunaweza tukaja na sheria nzuri ambayo haitusaidii kwa sababu mwisho wa siku ni matokeo. Watu wanataka kuona matokeo. Sasa hivi imefikia hatua watu wanateketeza mashamba ya chai. Wakulima wameanza kung'oa chai kwa sababu wamepoteza imani kama wanaweza wakapata soko la uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa inawezekana katika hili Bunge tukakaa tukaleta mawazo mazuri ambayo baadaye yasituletee tija, kwa sababu zao lenyewe la chai tunaweza tukakuta wakati tunaleta hii sheria na mipango mizuri, tayari limeteketezwa. Kwa hiyo, ninaomba sana Mheshimiwa Waziri, kwa huu ushauri tulioutoa na sina shaka na usikivu wake, basi twende tufanye kitu kwenye chai. Kwa dhati ninamwomba Mheshimiwa Waziri tufanye kitu kwenye chai. Kule Rungwe ni mwaka wa pili sasa hivi wakulima hawajauza chai, wanapata hasara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo mengine Njombe, Mufindi, huku kote shida ipo. Kwa hiyo, ninaomba sana kwa unyenyekevu mkubwa tufanye jambo kwenye tasnia ya chai ili kumkomboa mkulima wa zao hili la chai. Tayari Mheshimiwa Rais ametoa maelekezo mahsusi ya kuona namna gani tunaboresha hii tasnia ya chai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa mchango wangu huo, ninaomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa George. Sasa nimwite mtoa hoja, Mheshimiwa Waziri wa Kilimo. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nirejee tena kukushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuhitimisha hoja niliyoiwasilisha leo asubuhi. Pia, niruhusu nichukue nafasi hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia Muswada wa Sheria ya Mabadiliko ya Sheria ya Kilimo wa Mwaka 2026. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge nimewasikia, nimepokea maoni yao na nimeyazingatia. Niruhusu sasa nijibu baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge kwa kuanza na eneo la chai.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye chai Waheshimiwa Wabunge wameeleza vyema, wamechangia na wametoa maoni yenye kuthibitisha dhamira yao ya uwakilishi wa wananchi ambao wamepewa kuitekeleza ndani ya Bunge hili Tukufu. Niseme tu, nimewasikia wote wakiongozwa na Mheshimiwa Swalle ambaye ndiye balozi wa zao hili la chai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye eneo hili la chai, dhamira ya Serikali ya kuunganisha majukumu ya Wakala wa Wakulima Wadogo wa Chai nchini na kupeleka kwenye Bodi yetu ya Chai, yamebeba dhamira kubwa sana. Dhamira ya kwanza ni kuweka msukumo wa kuhakikisha wakulima wakubwa na wakulima wadogo wanasimamiwa kwenye eneo moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa wakulima wakubwa wanaanzia shambani mpaka mezani, ni kuweka msukumo pia na wakulima wadogo waanzie shambani mpaka mezani. Hilo linawezekana na Waheshimiwa Wabunge wametoa mifano ya wazi kabisa hapa. Sri Lanka wameweza, jirani zetu Kenya wameweza na sisi tunaweza. Mfano ambao tunaenda kujifunza kwenye eneo hili ni mfano ambao tumeamua Serikali kupitia

Wizara yetu kuwawezesha wakulima wa Wilaya ya Korogwe, pamoja na sehemu za Lushoto na Muheza, kwa kuwawezesha kupata kiwanda ambacho watakiendesha wenyewe kwenye eneo lao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wao wanalima, lakini wanalima wakitegemea kuuza majani mabichi kwa wachakataji wakubwa. Sasa, msukumo ni kuwawezesha kuchakata wenyewe ili wahitimishe zoezi la upatikanaji wa chai na kuwafanya wanufaike moja kwa moja, kwa sababu usindikaji ndiyo unaoongeza thamani na ndiyo unaowahakikishia kupata fedha za uhakika na fedha zenye faida ya uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye eneo la kurugenzi; niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge, kwenye kurugenzi ya wakulima wadogo ambayo itaundwa ndani ya Bodi ya Chai, tutahakikisha tunaitengenezea mazingira ya kutekeleza wajibu wake bila kukwamishwa kwa namna yoyote. Sababu za msingi zipo. Tumeua wakala, lazima tutengeneze msukumo wa kuonesha tofauti na kuonesha dhamira ya kweli ya Serikali kupitia kurugenzi hii kwa kuonesha matokeo. Tutaandaa kanuni na yote waliyotushauri tutayazingatia kupitia kanuni hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme kwenye hili la wakulima wakubwa, baadhi ya Wabunge wameonesha kutoridhishwa na mwenendo wa uwekezaji kwenye eneo hili. Niseme, hapa tunapozungumzia wakulima wakubwa wa chai tunazungumzia wachache sana. Kwa kuanzia na historia ya *Queen Elizabeth* kupitia *Brook Bond* kwa Mufindi, baadaye *Unilever,* akaja *EKATERRA* na wengineo mpaka sasa yupo *Brown*. Ukweli ni kwamba, kupitia uwekezaji wa *Brown* kazi inaenda vizuri na hatuna changamoto ambazo tunazipigia kelele na tunampongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna changamoto kwenye uwekezaji wa *Mufindi Tea Company (MTC)* ambayo baadaye ilikuja kuchukuliwa na *DL* ambaye sasa hivi ndiyo anamiliki viwanda vya Mufindi, Kibena na Luponde. Kwa kweli huko ndiyo

bado uchakataji haujafikia kwenye kiwango ambacho kinaridhisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kufanya kazi na tumeleta haya marekebisho. Lengo ni kuendelea kuipa nguvu Bodi ya Chai Nchini, ili itutafutie matokeo tunayoyakusudia kwenye zao hili nchini. Ninawatoa hofu Waheshimiwa Wabunge. Sheria ndiyo lakini dhamira ni muhimu zaidi kwenye kutafuta matokeo na sisi tumedhamiria kuhakikisha matokeo hayo tunayatafuta kwa udi na uvumba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye upande wa sukari; hapa kuna maeneo mawili ya msingi. Eneo la kwanza ni hili la kuchakata sukari ya viwandani nchini. Waheshimiwa Wabunge wameeleza vizuri sana kwenye eneo la sukari ya viwandani. Matumizi yetu nchini ni tani 300,000 na kidogo, lakini uchakataji wa sukari hiyo hapa ndani sasa hivi ndiyo umefikia kama tani 30,000, ambayo ni kama 10% ya uhitaji mzima wa sukari inayotakiwa kuchakatwa au kutumika kwenye viwanda vyetu nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwetu kuendelea kuagiza sukari ghafi, sukari ambayo ni ya viwandani moja kwa moja ni kujinyima fursa ya kuwekeza kwenye uchakataji wa sukari hiyo hapa nchini. Kwa hiyo, eneo mahsusi ambalo tumeliwekea msukumo kwenye mabadiliko haya ni kutoa fursa kwa Watanzania na wawekezaji kuja kuwekeza kwenye ujenzi wa viwanda vya kuchakata sukari ya viwandani nchini na kutoa fursa ya wao kuingiza *raw sugar* ili waje kuichakata nchini, kwa sababu kwetu tutakuwa tumevutia mtaji, tumevutia ajira, tumevutia kodi, lakini tumevutia na udhibiti wa fedha za kigeni kwenda nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, hilo ndiyo lengo kuu na kwa kweli ninawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao ambayo imejielekeza kuweka msukumo huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ni hili la vifungashio. Lengo ni kutengeneza uratibu na usimamizi wa eneo hili. Kwa sababu, sasa hivi ukienda kwenye maeneo kama kwenye *SGR*, kwenye ndege,

kwenye hoteli kubwa na maeneo mengine ya huduma, ufungashaji wa hizo sukari umeshaanza kufanyika na ndizo zinazotumika kwa kiwango kikubwa. Tukasema hatuwezi kuacha jambo hilo lifanywe bila kufuata sheria au kwa mujibu wa sheria. Kwa hiyo, tukaweka mapendekezo ya marekebisho ili kuliingiza eneo hilo kuratibiwa kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kubwa ninawahakikishia Waheshimiwa Wabunge, sukari itakayofungashwa kwenye ujazo huo kuanzia sifuri mpaka isiyozidi gramu 100, itakuwa ni sukari ya ndani. Hilo tutahakikisha tunalisimamia na ufungashaji huo lazima uoneshe anayefungasha na sukari imezalishwa na nani katika vifungashio ili *traceability* yake iwe rahisi na tuweze kuratibu kwa urahisi eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hayo ndiyo maeneo ya msingi ambayo tumeomba na ninashukuru tena Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru tena wewe kwa kunipa nafasi hii na kutuongoza vyema. Ninawasisitiza, michango yao tumeichukua na tutakwenda kuhakikisha tunaiwekea msukumo ili kutafuta kile ambacho ni matarajio ya Waheshimiwa Wabunge na Watanzania waliotupa dhamana ya kuwawakilisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Hoja imetolewa na imeungwa mkono.

Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:**

**27 AGOSTI, 2026**

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Kilimo wa Mwaka 2026 *(The Agricultural (Amendments) Bill, 2026)***

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:**

Kifungu cha 1
Kifungu cha 2
Kifungu cha 3

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 4
Kifungu cha 5

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 6
Kifungu cha 7
Kifungu cha 8
Kifungu cha 9
Kifungu cha 10

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 11

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya*

*Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 12
Kifungu cha 13
Kifungu cha 14
Kifungu cha 15
Kifungu cha 16
Kifungu cha 17

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 18

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 19
Kifungu cha 20
Kifungu cha 21

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 22
Kifungu cha 23
Kifungu cha 24

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Kifungu cha 25
Kifungu cha 26
Kifungu cha 27
Kifungu cha 28
Kifungu cha 29
Kifungu cha 30
Kifungu cha 31

Kifungu cha 32

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 33
Kifungu cha 34
Kifungu cha 35
Kifungu cha 36

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Bunge Zima imekamilisha kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirejea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tukae.

Mtoa hoja, taarifa.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Bunge hili imeipitia sheria kifungu kwa kifungu. Sasa ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaafiki.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Hoja imetolewa na imeungwa mkono, ahsanteni sana.

Waheshimiwa Wabunge, ninaomba niwahoji kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Kilimo wa Mwaka 2026.

Waheshimiwa Wabunge, walioafiki wameshinda. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**NAIBU SPIKA:** Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:**

**Muswada wa Sheria kwa ajili ya kufanya Marekebisho katika Sheria za Kilimo kwa lengo la Kuboresha Kanuni, Usimamizi na Maendeleo ya Sekta ya Kilimo pamoja na Masuala Mengine Yanayohusiana na hayo *(A Bill for an Act to Amend Certain Agricultural Laws with the View to Improving the Regulation, Administration and Development of Agricultural Sector and Related Matters)***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

*(Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Kilimo wa Mwaka 2026 Ulipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, kwa muktadha huo basi, Bunge tayari tumeshapitisha Muswada huu wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Kilimo wa Mwaka 2026. Hatua iliyobaki ni kwenda kwa Mheshimiwa Rais kwa ajili ya kupata kibali chake. Kwa muktadha huo, ninachukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wetu wa Kilimo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote kwa kazi hii kubwa mliyofanya. Tunategemea kwamba sheria mtaisimamia kwa ajili ya maslahi mapana ya wakulima wa Taifa hili. *(Makofi)*

Ninawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wakiongozwa na Kamati yetu ya Bunge ya Viwanda, Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati, Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wote wa Kamati hii kwa kazi kubwa mliyofanya. Pia Waheshimiwa Wajumbe mliopata nafasi ya kuchangia kwenye muswada huu kwa ujumla wenu

wote ninawashukuruni sana kwa kazi kubwa hii mliyoifanya. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya maelezo haya, basi ninaahirisha Shughuli za Bunge hadi kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 7.20 Mchana Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Ijumaa, Tarehe 28 Agosti, 2026 Saa Tatu Asubuhi)*

PARLIAMENT OF TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA